# TUME YA KUREKEBISHA SHERIA ZANZIBAR

## RIPOTI YA UTAFITI WA SHERIA YA WATOTO NAM 6 YA MWAKA 2011

## NAMBA 8/ MWAKA 2023

**INAWASILISHWA KWA MHESHIMIWA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA**

**Contents**

Contents ........ i

SHUKRAN ........ vii

MUHTASARI ........ x

Dira ya Maendeleo Zanzibar ya 2050 ........ xvii

Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020-2025 ........ xvii

Sera ya Afya ya mwaka 2011 ........ xvii

Sera ya Ajira Zanzibar ya mwaka 2009 ........ xvii

Sera ya Hifadhi ya Jamii Zanzibar ya mwaka 2014 ........ xvii

Sera ya Michezo ya Mwaka 2018 ........ xvii

Sera ya Uhakika wa Chakula na Lishe ya Zanzibar ya mwaka 2008 ........ xvii

Sera ya Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2018 ........ xvii

1.0 UTANGULIZI ........ 1

1.1. Mamlaka ya Tume ........ 1

1.2. Chimbuko la Utafiti ........ 2

1.3. Maelezo ya Tatizo ........ 3

1.4. Historia ........ 3

1.5. Hadidu Rejea .......... 10

1.6. Malengo ya Utafiti .......... 11

1.7. Njia zilizotumika katika Utafiti .......... 12

2.0 DHANA YA HAKI NA ULINZI WA MTOTO .......... 13

2.1. Maana ya Neno Mtoto .......... 13

2.2. Haki za Watoto .......... 14

2.3. Matunzo na Ulinzi wa Mtoto .......... 15

2.4. Mfumo wa Ulinzi wa Watoto .......... 15

2.5. Unyanyasaji wa Mtoto .......... 17

3.0 MIPANGO YA KITAIFA, SERA NA SHERIA MBALI MBALI .......... 19

3.1. Utangulizi .......... 19

3.2. Mipango Mikuu ya Nchi .......... 19

3.2.1. Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) 2020-2025 .......... 19

3.2.2. Dira ya Maendeleo Zanzibar ya 2050 .......... 22

3.3. Sera .......... 23

3.3.1. Sera ya Uhakika wa Chakula na Lishe ya Zanzibar ya mwaka 2008 23

3.3.2. Sera ya Michezo ya Mwaka 2018 .......... 24
3.3.3. Sera ya Hifadhi ya Jamii Zanzibar ya mwaka 2014 .......... 26
3.3.4. Sera ya Ajira Zanzibar ya mwaka 2009 .......... 27
3.3.5. Sera ya Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2018 .......... 29
3.3.6. Sera ya Afya ya mwaka 2011 .......... 29
3.4. Sheria .......... 30
3.4.1. Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984 .......... 30
3.4.2. Sheria ya Watoto Nam. 6 ya Mwaka 2011 .......... 32
3.4.3. Sheria ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar, Nam.3 ya mwaka 2018 .......... 38
3.4.4. Sheria ya Kuwalinda Wari na Watoto wa Mzazi Mmoja, Nam. 4 ya 2005 39
3.4.5. Sheria ya Adhabu Nam. 6 ya Mwaka 2018 .......... 40
3.4.6. Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Nam. 7 ya mwaka 2018 44
3.4.7. Sheria ya Ushahidi Nam.9 ya mwaka 2016 .......... 45
3.4.8. Sheria ya Msaada wa Kisheria Nam. 13 ya mwaka 2018 .......... 47
3.4.9. Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu Nam. 6 ya mwaka 2008 .......... 49

3.4.10. Sheria ya Elimu Nam.6 ya mwaka 1982 ........ 50

3.4.11. Sheria ya Mahakama ya Kadhi Nam. 9 ya mwaka 2017 ........ 52

3.4.12. Sheria ya Makosa ya Mtandao Nam. 14 ya mwaka 2015 ........ 52

3.4.13. Sheria ya Ajira Nam.11 ya mwaka 2005 ........ 53

4.0 MAONI YA WADAU ........ 55

4.1. Utangulizi ........ 55

4.2. Maoni ya Kisheria ........ 56

4.3. Maoni ya kiutendaji ........ 63

5.0 MIKATABA YA KIMATAIFA NA UZOEFU KATIKA NCHI NYENGINE ........ 67

5.1. Utangulizi ........ 67

5.2. MIKATABA YA KIMATAIFA ........ 67

5.2.1. Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu la Mwaka 1948. ........ 67

5.2.2. Mkataba wa Haki za Mtoto wa Mwaka 1989 ........ 68

5.2.3. Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa wa Mwaka 1966 69

5.2.4. Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni wa Mwaka 1966 ........ 70

5.2.5. Mkataba wa Ajira Mbaya zaidi kwa Watoto, wa Shirika la Kazi Duniani (ILO) Nam. 182 wa Mwaka 1999. .......... 72
5.2.6. Mkataba wa Umri wa Chini wa Shirika la Kazi Duniani (ILO) Nam. 138 wa Mwaka 1973.......... 73
5.3. MIKATABA YA KIKANDA .......... 74
5.3.1. Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu wa Mwaka 1981 74
5.3.2. Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto wa Mwaka 1990. 74
5.3.3. Mkataba wa Baraza la Ulaya juu ya Ulinzi wa Watoto dhidi ya Unyanyasaji na Udhalilishaji wa Kijinsia wa Mwaka 2007 .......... 78
5.4.1 JAMHURI YA KENYA .......... 79
1. MAURITIUS .......... 89
2. NEPAL.......... 96
3. LESOTHO .......... 102
6.0 MATOKEO YA UTAFITI .......... 107
6.1. Utangulizi .......... 107
6.2. Njia Zilizotumika katika Utafiti.......... **Error! Bookmark not defined.**

6.3. Makundi ya Wadau (Sampuli ya utafiti) na Uchambuzi wa Takwimu 107
6.4. Matokeo ya Utafiti ........ 119
6.4.1. Matokeo ya Kisheria. ........ 119
6.4.2. Matokeo ya kiutendaji........ 125
7.0 MAPENDEKEZO NA HITIMISHO ........ 128
7.1. Utangulizi ........ 128
7.2. Mapendekezo ya Kisheria ........ 128
7.3. Mapendekezo ya kiutendaji ........ 137
7.4. Hitimisho ........ 139

## SHUKRAN

Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar imefanikiwa kukamilisha utafiti wa mapitio ya Sheria ya Watoto, Nam. 6 ya mwaka 2011 kwa lengo la kubaini changamoto na mapungufu yaliopo katika usimamizi na uimarishaji wa ustawi wa watoto nchini kupitia Sheria hii ya Watoto na kutoa mapendekezo ya kisheria na kiutendaji Serikalini yatakayoimarisha ustawi wa watoto nchini. Ni Imani yetu kuwa mapendekezo yaliyotokana na utafiti uliofanywa wakati wa mapitio ya Sheria hii, yatasaidia kuimarisha usimamizi wa watoto wa Zanzibar na hivyo kutekeleza matakwa ya haki za binadamu na haki za watoto kama yalivyoainishwa katika mikataba ya kimataifa na katika Katiba ya Zanzibar ya 1984, pamoja na Dira ya Maendeleo Zanzibar ya 2050.

Tume inapenda kutoa shukrani za pekee kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa uongozi wake wenye kutambua misingi ya haki za Binaadamu ikiwemo kulinda haki za watoto. Tunampongeza mheshimiwa Rais kwa kuhimiza kufanywa marekebisho ya sheria mbali mbali, ambayo ni sehemu ya chimbuko la Sheria hii kufanyiwa mapitio.

Aidha, shukrani za dhati zimwendee Mheshimiwa Mwalim Haroun Ali Suleiman, Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa juhudi zake katika kusimamia utawala wa sheria, utawala bora na misingi ya haki za binadamu. Miongozo yake kwa Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar imesaidia Tume katika kazi za mapitio ya sheria mbali mbali ikiwemo Sheria hii ya Watoto. Aidha, Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar inapenda kuwashukuru Viongozi wote na watendaji wa Ofisi ya Rais, Katiba Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa ushirikiano na msaada mkubwa katika kufanikisha utafiti na mapitio ya Sheria hii.

Aidha, Tume inatoa shukrani kwa taasisi mbali mbali ikiwemo Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Shirika la kimataifa la ''Save the Children'' na Jumuiya ya Wajane Zanzibar (ZAWIO) ambazo zilishirikiana na Tume katika kushughulikia uratibu wa vikao vya kukusanya maoni kutoka kwa wananchi na taasisi mbali mbali kwa kuchangia rasilimali fedha zilizofanikisha kufanyika kwa vikao hivyo. Kufanyika kwa vikao hivyo vya kukusanya maoni kumesaidia sana katika kufanikisha mapitio ya Sheria hii. Tume pia inazishukuru taasisi nyengine za Serikali, sekta binafsi, asasi za kiraia na makundi mbali mbali ya wananchi kwa kusaidia katika kufanikisha mapitio ya Sheria hii na kukamilika kwa ripoti yake.

Shukrani pia zinatolewa kwa wataalam mbali mbali wa masuala ya watoto, maafisa ustawi wa Wizara inayohusika na masuala ya watoto, wataalamu kutoka taasisi mahsusi zinazosimamia masuala ya watoto kwa upande wa Unguja na Pemba, kwa jitihada zao za kuisaidia Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar katika kukamilisha utafiti wa Sheria hii ya Watoto na hatimaye kutayarisha Ripoti hii. Maoni na utaalamu wao umeisaidia sana Tume katika kufanikisha ripoti hii.

Aidha, shukrani ziende kwa Katibu wa Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar Ndg. Mussa Kombo Bakari na wataalam wa Sheria, Utafiti na Mipango, walioongoza zoezi la utafiti na kufanya uchambuzi yakinifu wa taarifa na uandishi wa ripoti hii.

Ahsante.

Khadija Shamte Mzee,

## MUHTASARI

Watoto ni kundi muhimu katika taifa lolote lile hapa duniani linalopaswa kuendelezwa na kulindwa dhidi ya vitendo viovu vinavyoweza kuathiri maendeleo ya watoto hao. Moja ya nyenzo muhimu katika ulinzi wa haki na maendeleo ya watoto ni kuwa na mfumo imara na madhubuti wa kisheria, utakaoweka ulinzi wa kutosha na kuimarisha ustawi wa watoto. Hivyo, Sheria ya Watoto ni moja kati ya sheria muhimu katika kusaidia kuwalinda na kuwakuza watoto katika mazingira mazuri. Taifa lenye watoto waliowekewa ulinzi imara kupitia mfumo wa kisheria, lina nafasi nzuri ya kuwa na ustawi mzuri wa watu wake na hivyo kuchochea maendeleo katika kila Nyanja.

Watoto wana haki nyingi ambazo zimeoneshwa katika mikataba mbali mbali ya kimataifa na kikanda ili kuhakikisha wanalindwa kutokana na kuwa wapo hatarini zaidi ya kuvunjiwa haki zao kutokana na umri wao mdogo. Kwa kutambua mazingira hayo, Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar imefanya mapitio ya Sheria ya Watoto, Nam. 6 ya mwaka 2011 ili kuangalia utekelezaji wa Sheria hiyo, changamoto ziliopo na kupendekeza marekebisho ya Sheria hiyo pamoja na mapendekezo mengine yatakayosaidia kuweka ustawi mzuri wa watoto nchini.

Katika kuifanya mapitio sheria hii, njia mbali mbali zimetumika ikiwemo kupitia rejea mbali mbali za ndani na nje ya nchi, kuangalia mikataba ya kimataifa na kikanda pamoja na Sheria za nchi nyengine, kupitia katiba ya Zanzibar, Sera na Sheria mbali mbali za ndani ya nchi, pamoja na kukusanya maoni ya wadau na wataalamu wengine wanaosimamia Sheria ya Watoto.

Aidha mapitio ya sheria hii yameonesha maeneo muhimu ambayo yanapaswa kuangaliwa na kufanyiwa marekebisho ili kuhakikisha ulinzi kwa watoto unaimarika.

Katika kuzingatia maslahi bora ya mtoto na kuimarisha ulinzi wa watoto mapitio ya utafiti huu yamebainisha baadhi ya maeneo ya kuimarishwa zaidi ikiwemo Wajibu wa Jamii kumlinda mtoto dhidi ya ukiukwaji wa haki zake, badala ya Sheria kuweka wajibu kwa taasisi mahsusi zinazosimamia masuala ya watoto pekee. Aidha, mapitio haya yameonyesha udhaifu uliopo katika eneo hilo na kupendekeza marekebisho ya Sheria, ikiwemo kuchukuliwa kwa hatua kwa wanajamii watakaoshindwa kutekeleza wajibu wa kumlinda mtoto.

Eneo jengine lililobainika katika mapitio ya Sheria ya Watoto ni kutokuwepo kwa mfumo imara na wa uwazi katika kuwalinda watoto dhidi ya makosa ya kimtandao kwani kwa Sheria ilivyo kwa sasa, haikuweka ulinzi madhubuti wa watoto kutokana na makosa hayo. Kwa msingi huo, Ripoti hii imependekeza

kurekebishwa kwa Sheria ya Watoto ili kuweka wazi masharti hayo ya kuwalinda watoto dhidi ya makosa udhalilishaji wa kimtandao.

Pia Tume katika mapitio ya Sheria hii imebaini kuwa suala la ulinzi wa watoto linahitaji gharama kubwa na baadhi ya nchi zimeanzisha Mifuko ya Maendeleo ya Watoto katika sharia zao ili kuwa na fedha za kutosha za usimamizi wa watoto. Kwa kutambua umuhimu huo, Tume imependekeza Sheria hii ya Watoto irekebishwe ili nayo itambue kuanzishwa kwa Mfuko huo wa Maendeleo ya Watoto, pamoja na kuweka vyanzo vya fedha vya Mfuko huo na namna ya kuusimamia ili malengo yaliyokusudiwa yaweze kufikiwa.

Katika mapitio ya Sheria hii ya Watoto, pia limejitokeza suala la haja ya kuanzishwa kwa Idara mahsusi ya Watoto, itakayosimamia kwa ukaribu zaidi masuala ya watoto. Mapendekezo hayo yanatokana na hoja kwamba kwa muundo wa sasa, masuala ya watoto yanasimamiwa na Idara moja na mambo mengine kadha na hivyo kupunguza nguvu ya usimamizi mzuri wa watoto.

Pia Tume imebaini kuwa jukumu la kutetea haki na ustawi wa watoto pamoja na kuwalinda watoto dhidi ya uvunjaji wa haki za zao, ni jukumu kubwa linalopaswa kushirikisha taasisi mbali mbali. Kwa muktadha huo, Tume imependekeza Sheria izitambue mamlaka za Serikali za mitaa katika ulinzi wa watoto na kuimarisha ustawi wao. Tume imependekeza kujumuishwa kwa

Serikali za mitaa kutokana na nafasi yake katika maendeleo ya maeneo wanayosimamia na kwa kuzingatia kuwa mamlaka hizo zipo karibu zaidi na wananchi.

Aidha, mapitio ya Sheria hii ya Watoto imebaini kuwa hakuna utaratibu mzuri wa kisheria wa kupokea na kusikiliza na kutatua malalamiko yanayojitokeza kuhusiana na masuala ya watoto. Tume imebaini kuwa, kuwepo kwa utaratibu wa kisheria wa kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko hayo, kunaweza kusaidia kutatua changamoto nyingi katika uimarishaji wa ustawi wa watoto nchini. Hivyo, Tume imependekeza kurekebishwa kwa Sheria ya Watoto kwa kuingizwa masharti yanayohusu upokeaji na ushughulikiaji wa malalamiko kuhusiana na masuala hayo ya watoto.

Mbali na maeneo hayo ya kisheria ambayo Tume imependekeza kurekebishwa kwa Sheria hiyo ya Watoto, pia maeneo mbali mbali ya kiutendaji yamependekezwa kutekelezwa ili Sheria hiyo ya Watoto iweze kufanyiwa kazi vizuri. Miongoni mwa maeneo hayo ya kiutendaji yaliyopendekezwa ni pamoja na kutungwa kwa Kanuni za Sheria hiyo hasa katika maeneo ambayo bado hayajatungiwa Kanuni, kuanzishwa kwa Skuli za Marekebisho, ambazo zimetajwa kwenye Sheria ya Watoto na kutolewa kwa elimu ya kutosha kwa

wananchi kuhusu ulinzi wa watoto na kuhamasisha utekelezaji wa haki za watoto.

Tume inaamini kuwa matokeo na mapendekezo ya utafiti huu iwapo yatafanyiwa kazi, yatasaidia kuondosha changamoto zilizopo hivi sasa katika ulinzi wa watoto Zanzibar.

**REJEA**

Abbott, G. What can we do about child abuse? The Office of the Attorney General with the cooperation of Texas CASA, Inc. 2004

Cleland, A. Child abuse, child protection and the Law 1st Edition, W.Green&son Ltd, London (2008)

Mashamba,C.J.The Justice Review Special Commentary on the Tanzanian Law of the Child Act 2009, Volume 8 no.2. 2009 National Organisation for Legal Assistance, Dar es Salaam (2009)

Mohammed, H and. Mashamba, C.J. Child Rights and the Law in East Africa, Lawafrica Publishing Co. (T) Ltd, Dar es Salaam (2014)

Mrisho, F. Sexual Abuse Report: The magnitude, risk factors and social cultural dynamics for Sexual Abuse and Early Sexual debut among In and out of School Adolescents in Tanzania (2010)

Mwafisi, M. J. Agenda 66 on Promotion and Protection of the Rights of Child. Permanent Secretary, Ministry of Community Development, in the third committee of the 6 session of the General Assembly (2007)

Plan International. Child Protection Programming: Thematic Review on Child Protection, New Image Publishers, New York (2012)

Save the Children, (2012). Desk Review and Analysis of Literature on Child Protection System in the Eastern Africa Region (Unpublished) at pp. 37-38

67Violence against children in Tanzania: Findings from a National Survey, 2009, Dar es Salaam, UNICEF

Shivji, I, Majamba, H, Makaramba, R and Maina, C. . Constitutional and Legal System of Tanzania, A Civil Sourcebook. Mkuki na Nyota Publishers Ltd, Dar es Salaam (2004).

Tanzania Human Rights Report, 2013

UNICEF – Update of the Analysis of Women and Children in Zanzibar, 2006 Zanzibar (Unpublished).

United Nations Children's Fund, *Measuring and Monitoring Child Protection Systems: Proposed Core Indicators for the East Asia and Pacific Region,* Strengthening Child Protection Series No. 1. UNICEF EAPRO, Bangkok (2012)

**MIPANGO NA SERA**

Dira ya Maendeleo Zanzibar ya 2050

Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020-2025

Sera ya Afya ya mwaka 2011

Sera ya Ajira Zanzibar ya mwaka 2009

Sera ya Hifadhi ya Jamii Zanzibar ya mwaka 2014

Sera ya Michezo ya Mwaka 2018

Sera ya Uhakika wa Chakula na Lishe ya Zanzibar ya mwaka 2008

Sera ya Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2018

**SHERIA**

Katiba ya Zanzibar ya 1984

Sheria ya Adhabu Nam. 6 ya Mwaka 2018

Sheria ya Adhabu, Sura ya 13 ya mwaka 1934

Sheria ya Ajira Nam.11 ya mwaka 2005

Sheria ya Ajira kwa Watoto na Vijana (kukataza) Sura ya 56 ya Mwaka 1952

Sheria ya Elimu Nam.6 ya mwaka 1982

Sheria ya Kuasili Watoto, Sura ya 55 ya Mwaka 1951

Sheria ya Kuwalinda Wari na Watoto wa Mzazi Mmoja, Nam. 4 ya 2005

Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu Nam. 6 ya mwaka 2008

Sheria ya Mahakama ya Kadhi Nam. 9 ya mwaka 2017

Sheria ya Mahakama Za Mahakimu, Nam. 6 ya 1985

Sheria ya Makosa ya Mtandao Nam. 14 ya mwaka 2015

Sheria ya Msaada wa Kisheria Nam. 13 ya mwaka 2018

Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Nam. 7 ya mwaka 2018

Sheria ya Skuli za Kurekebisha Tabia, Sura ya 59 ya mwaka 1945

Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar Nam. 16 ya mwaka 1986

Sheria ya Ushahidi Nam.9 ya mwaka 2016

Sheria ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar, Nam.3 ya mwaka 2018

Sheria ya Wahalifu Vijana, sura ya 22 ya mwaka 1935

Sheria ya Watoto Nam.6 ya Mwaka 2011

Sheria ya Watoto na Vijana Wadogo, Sura ya 58 ya waka 1952

Sheria ya Mtoto ya Jamhuri ya Kenya Nam.29 ya Mwaka 2022.

Sheria ya Watoto ya Mauritius Nam.13 ya Mwaka 2020

Sheria inayohusiana na Watoto ya Nepal Nam.23 ya Mwaka 2018.

Sheria ya Ulinzi na Ustawi wa Watoto ya Lesotho Nam.7 ya Mwaka 2011

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1. Mamlaka ya Tume

Tume ya Kurekebisha Sheria ya Zanzibar imeundwa na Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar, Nam.16 ya Mwaka 1986. Sheria hiyo inaipa uwezo Tume ya Kurekebisha Sheria kuzifanyia mapitio Sheria zote za Zanzibar kwa nia ya kupendekeza marekebisho ili ziende sambamba na maendeleo na mabadiliko ya kimfumo.[1]

Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar katika kufanya mapitio ya Sheria inaweza kufanya mapitio kwa kutumia njia tatu zilizoainishwa katika Sheria yake. Njia ya kwanza, Tume inaweza kufanya mapitio ya Sheria ikiona ipo haja ya kufanya hivyo,[2] njia ya pili ni kwa maelekezo ya Waziri anaehusika na mambo ya Sheria,[3] na njia ya tatu ni kwa maelekezo ya Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar.[4]

---

[1] Kifungu cha 4(1) cha Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar Nam. 16 ya mwaka1986

[2] Ibid, kifungu 9

[3] Ibid, Kifungu cha 7

[4] Ibid, kifungucha 8

Kutokana na uwezo iliyopewa kwa mujibu wa Sheria, na katika kutekeleza majukumu yake ya msingi, Tume imeamua kufanya mapitio ya Sheria ya Watoto[5] kwa ajili ya kuainisha mapungufu ya Sheria hiyo na kupendekeza Serikalini marekebisho yake.

Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar, ikiwa kama chombo kinachojitegemea[6] kilichopewa mamlaka ya kutafiti na kupitia Sheria zote za Zanzibar, inafanya mapitio haya kwa madhumuni ya kutambua mapungufu na kupendekeza marekebisho katika Sheria ya Watoto ili kuimarisha ustawi wa watoto na kutekeleza matakwa ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, mikataba mbalimbali ya kimataifa na kikanda katika kulinda maslahi bora ya mtoto.

### 1.2. Chimbuko la Utafiti

Chimbuko la utafiti huu ni maombi yaliyoletwa Tume ya Kurekebisha Sheria kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kuhusu kuifanyia mapitio Sheria ya Watoto Nam.6 ya mwaka 2011. Aidha, kutokana na umuhimu mkubwa wa kuwalinda watoto kama moja ya makundi muhimu kwenye jamii kundi ambalo limekuwa likipitia changamoto nyingi kutokana na mazingira yake, Tume ililazimika kufanya mapitio ya Sheria hii ya Watoto.

---

[5] Sheria ya Watoto, Nam.6 ya 2011

[6] *Op cit* kifungu cha 12

### 1.3. Maelezo ya Tatizo

Kutungwa kwa Sheria ya Watoto ya Mwaka 2011 kulidhamiria kusaidia katika kumlinda mtoto wa Zanzibar kutokana na udhalilishaji na kuhakikisha upatikanaji wa haki na ustawi mzuri. Hata hivyo watekelezaji wa Sheria hiyo na wadau wengine wa masuala ya watoto wameonesha kuwepo kwa baadhi ya changamoto ambazo zinahitaji kufanyiwa kazi ili kusimamia maslahi ya mtoto wa Zanzibar. Mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia na jamii yameleta mabadiliko makubwa duniani, pamoja na athari ambazo zinaathiri ustawi mzuri wa mtoto. Hivyo uwepo wa changamoto hizo unapelekea umuhimu wa kuipitia Sheria hii ili malengo yaliyokusudiwa wakati wa kutungwa kwake yaweze kufikiwa.

### 1.4. Historia

Katika miaka iliyopita, hakuna mtu aliyefikiria kutoa ulinzi maalum kwa watoto.[7] Mpaka kufikia katikati ya karne ya 19, Ufaransa iliona ipo haja ya kuwapa watoto ulinzi maalum na maendeleo endelevu kwa "haki za watoto." Kuanzia mwaka 1841, Sheria za nchini Ufaransa zilianza kutoa ulinzi kwa watoto katika sehemu zao wanazofanyia kazi. Vile vile, mwaka 1881 Sheria za Ufaransa pia zilitambua haki ya elimu kwa watoto na hivyo watoto kuwa na

[7] Children's Rights History - Humanium

uhakika wa kupata elimu.[8] Mwanzoni mwa karne ya 20, ulinzi wa watoto ulianza kuboreshwa zaidi na kuwekwa katika nyanja za matibabu, kijamii na katika kupata haki kupitia njia mbali mbali ikiwemo mahakama. Ulinzi wa aina hii kwa watoto ulioanzia Ufaransa, baadae ulienea Bara lote la Ulaya.[9]

Kufuatia matokeo mabaya ya vita vya dunia vya karne ya 20 na athari zake za kisaikolojia na kimwili kwa watoto, Umoja wa Mataifa uliona kwamba haki za binadamu za watoto zinahitaji ulinzi maalum[10] na kutayarisha mkataba wa Ulimwengu wa Haki za Kibinadamu ambao ulijumuisha haki ya kuishi, chakula, malazi, elimu, uhuru wa kujieleza na kuabudu, haki na amani. Kwa kutambua kwamba watoto walikuwa hatarini zaidi, Umoja wa Mataifa ulikubali kupitisha Tamko la Geneva kuhusu Haki za Watoto mwaka wa 1924, ambalo lilikuwa ni tamko la kwanza mahsusi la kimataifa lililotambua na kuthibitisha kwa mara ya kwanza kuwepo kwa haki maalum kwa watoto na wajibu wa watu wazima kwa watoto.[11] Tamko hilo lilikuwa na mambo makuu matano tu, lakini liliainisha majukumu dhidi ya watoto ambao wapo katika mazingira magumu.

---

[8] ibid

[9] HISTORICAL BACKGROUND AND EVALUATION OF RIGHTS OF CHILDREN (ijirl.com)

[10] Child Rights - History, Facts and How To Protect Them | World Vision Australia

[11] Geneva Declaration of the Rights of the Child, 1924 - Humanium

Baada ya Vita vya Pili vya Dunia, Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa lilikubaliana na Azimio la Geneva kuhusu Haki za Mtoto. Azimio hili lilifungua njia ya kupitishwa kwa Mkataba wa Haki za Mtoto wa 1989,[12] ambao ni mkataba wa kwanza wa kimataifa wenye nguvu za kisheria katika kulinda haki za watoto.

Misingi mikuu ya mkataba huu ni pamoja na kutaka watoto kutobaguliwa katika maamuzi yote yanayohusu watoto, kuzingatiwa kwa maslahi yao, Watoto kuwa na haki ya kuishi na kukua kiafya, na Watoto kuwa na haki ya kutoa maoni ambayo yatazingatiwa katika masuala yanayowahusu. Mkataba huu una lengo la kuwalinda watoto kutokana na madhara, ukuaji na maendeleo yao, na kukuza ushiriki wao katika jamii.[13]

Zanzibar nayo ilipitia hatua mbali mbali katika kumlinda mtoto kutokana na kukosa haki na kupata ulinzi wa kutosha. Hii inajionesha kupitia Sheria mbali mbali ambazo asili yake, haikuwa Zanzibar bali zilikuja Zanzibar kupitia wakoloni waliokuja kutawala Zanzibar. Sheria za mtoto zililetwa maalum kwa lengo la kuwalinda watoto kutokana na mambo mbali mbali ambayo yanaweza kupelekea kunyanyasika au kudhalilika kwa sababu tu ya utoto wao. Miongoni

[12] Convention on the Rights of the Child | OHCHR
[13] Children's Human Rights - Amnesty International

mwa Sheria hizo kwa Zanzibar ni Sheria ya Adhabu[14] ambayo ilibainisha makosa mbalimbali yanayoweza kufanyiwa watoto pamoja na adhabu zake. Makosa hayo yaliyoainishwa katika Sheria hii ni pamoja na ubakaji,[15]kutorosha mtoto wa kike chini ya miaka 16,[16] shambulio la aibu na kumtukana mwanamke au mtoto wakike,[17] na kunajisi mtoto wa kike chini ya miaka 14 au aliekua hajapata ukubwa.[18] Makosa mengine dhidi ya mtoto yaliyobainishwa katika Sheria hiyo ni kumzuia mwanamke au mtoto wa kike katika danguro au penginepo,[19] kufanya maingiliano ya kingono na maharimu,[20] kutoa mimba[21] Shambulio la aibu kwa mtoto wa kiume,[22] kutelekeza mtoto[23] au kuiba mtoto.[24]

---

[14] Sheria ya Adhabu, Sura ya 13 ya mwaka 1934

[15]Ibid, Kifungu 120&121

[16] Ibid, Kifungu 123

[17] Ibid, Kifungu cha124

[18] Ibid, vifungu vya 125, 126, 128 & 130

[19]Ibid, Kifungu cha 131

[20]Ibid, vifungu vya 147 & 148

[21] Ibid, vifungu vya 138, 139 & 140

[22] Ibid, Kifungu cha 144

[23] Ibid, vifungu vya 154 & 155

[24] Ibid, kifungu cha 157

Aidha, Sheria ya Skuli za Kurekebisha Tabia[25] ambayo ilitungwa kwa lengo la kuanzisha vituo vya kurekebisha tabia na kuwasimamia vijana waliofanya makosa au wazururaji ilipitishwa mnamo mwaka 1945. Vituo hivyo vilipewa jukumu la kupokea watoto ambao wamefanya makosa ambayo hukumu yake ilikuwa ni kifungo.[26] Sheria nyengine ambayo ilianzishwa kipindi hicho ni Sheria ya Kuasili Watoto[27] (Adoption of Children Decree) ambayo ilitungwa kwa lengo la kuweka masharti ya kuasili watoto na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Vile vile, Sheria nyengine kuhusiana na watoto iliyopitishwa ni Sheria ya (kuweka vizuizi) ajira kwa watoto na vijana wadogo,[28] Sheria hii iliweka vizuizi katika kuajiri watoto[29] na vijana kwa baadhi ya kazi.[30] Aidha, Sheria hii ilieleza kuwa ajira kwa watoto haiwezi kukubaliwa mpaka kuwe na ruhusa ya mzazi wa mtoto husika.[31]

---

[25] Sheria ya Skuli za Kurekebisha Tabia, Sura ya 59 ya mwaka 1945

[26] Ibid, Kifungu cha 3

[27] Sheria ya Kuasili Watoto, Sura ya 55 ya Mwaka 1951

[28] Employment of Children, Young Person and Adolescents (Restriction) Decree, Sura ya 56 ya mwaka 1952

[29] Ibid, Kifungu cha 3

[30] Ibid, Kifungu  cha 4

[31] Ibid, kifungu cha 5

Katika kusimamia mfumo wa kisheria unaosimamia masuala ya watoto, Zanzibar pia iliwahi kutunga Sheria ya Wahalifu Vijana (Juvinile Offenders Decree) [32] ambayo ilianzisha Mahakama ya Watoto iliyoundwa sawa na Mahakama ya Watoto ya Kiingereza. Sheria hiyo iliweka kipengele cha ulinzi wa watoto walio chini ya umri wa miaka kumi na sita, na taratibu katika kesi ya mtoto huyo kwa mashtaka ya jinai. Vile vile Sheria hiyo ilianzisha Mahakama ya Watoto (kama mahakama tofauti) katika ngazi ya Mahakama ya Mkoa kwa madhumuni ya kusikiliza na kuendesha kesi zote dhidi ya watu walio chini ya umri wa miaka 18. Baadae Sheria hii ilifutwa na Sheria ya Watoto na Vijana Wadogo.[33]

Baada ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar ya mwaka 1964, Zanzibar iliendelea kufuata mfumo uleule wa Mahakama ya Watoto uliokuwepo pamoja na Mahakama ya Hakimu Mkaazi.[34] Kifungu cha 22 kilibainisha kuwa Mahakama ya Watoto itaongozwa na Hakimu. Zanzibar iliendelea kumlinda mtoto kupitia haki za binaadamu zilizomo katika Katiba[35] wakati ikiendelea na mipango na mikakati ya kuhakikisha mtoto analindwa kwa upekee. Mwaka 1984, Baraza la

---

[32] Sheria ya Wahalifu Vijana, sura ya 22 ya mwaka 1935

[33] Sheria ya Watoto na Vijana Wadogo, Sura ya 58 ya waka 1952

[34] The Magistrare Court Act, Nam. 6 ya 1985

[35] Katiba ya Zanzibar ya 1984

Wawakilishi la Zanzibar liliifuta Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1979 na kupitisha Katiba ya Zanzibar ya 1984 inayotumika hadi sasa. Katiba hii imeweka Sura ya Tatu inayoelezea masharti kuhusu haki za binadamu na hivyo mtoto naye kulindwa na masharti ya haki hizo za binadam kwa kuwa haki hizo zinamgusa kila mtu bila ya kujali umri wake.[36]

Katiba hii haikutaja haki za kila kundi bali ilitaja haki za jumla za binaadamu zinazolinda watu wote, ikiwemo watoto na msingi wa kugusa makundi yote katika jamii umewekwa na Katiba hiyo.[37] Miongoni mwa haki zilizoelezwa katika Katiba hiyo ya Zanzibar ni pamoja na haki ya kuwa hai,[38] haki ya uhuru wa mtu binafsi,[39] haki ya faragha ya mtu na usalama wake,[40] kinga ya uhuru wa kwenda,[41] uhuru wa maoni,[42]uhuru wa mtu kuamini dini atakayo,[43] uhuru wa kushiriki shughuli za umma, haki ya kufanya kazi na kupata ujira[44] wajibu wa

---

[36] Ibid, kifungu cha 11 hadi kifungu cha 21, vimeweka haki na uhuru wa kila binaadamu bila kujali umri au hali yoyote na hivyo watoto nao wanastahiki haki hizo za kikatiba.

[37] Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, ambapo kifungu cha 11 cha Katiba hii kinaeleza kuwa binaadamu wote huzaliwa huru, na wote ni sawa.

[38] Ibid, kifungu cha 13

[39] Ibid kifungu cha 14

[40] Ibid, kifungu cha 15

[41] Ibid, kifungu cha 16

[42] Ibid, kifungu cha 18

[43] Ibid, kifungu cha 19

[44] Ibid, kifungu cha 21

kushiriki kazini[45], wajibu wa kutii sheria za nchi, kulinda mali ya umma na ulinzi wa taifa.[46]

Mnamo mwaka 2007, Zanzibar ilianzisha mchakato wa kurekebisha Sheria zinazosimamia haki za watoto. Marekebisho hayo yalitimizwa mwaka 2011 ambapo Sheria hii haina maelezo katika historia, imejitokeza hapo katika kufutwa pekee ilifutwa na nafasi yake kuchukuliwa na Sheria ya Watoto Nam. 6 ya mwaka 2011. Vile vile, Sheria ya Watoto imefuta Sheria ya Kuasili Watoto na Sheria ya Shule za Marekebisho ya Tabia.

## 1.5. Hadidu Rejea

Katika kufanya utafiti huu, Hadidu Rejea zifuatazo zilizingatiwa:

(a) Kufanya utafiti wa kina katika Sheria na Sera zinazohusu ulinzi na uhifadhi wa mtoto;

(b) Kuangalia uzoefu wa Sheria za nchi mbalimbali kuhusiana na masuala ya watoto na kuangalia namna uzoefu huo unavyoweza kutumika kwa mazingira ya Zanzibar;

---

[45] Ibid, kifungu cha 22

[46] Ibid, kifungu cha 23

(c) Kukusanya maoni ya wadau mbalimbali wanaohusika na masuala ya ulinzi wa haki za watoto kwa ajili ya kupata maoni yao na kuchangia katika kuimarisha Sheria ya Watoto na usimamizi wake na hivyo kuimarisha maendeleo ya watoto wa Zanzibar.

(d) Kupitia Mikataba ya Kimataifa, Maazimio na Miongozo inayohusiana na eneo hili la utafiti na kuangalia mambo ya msingi yanayoweza kuzingatiwa katika marekebisho ya Sheria hii.

(e) Kutoa mapendekezo ya kisheria, kiutendaji na kisera kwa ajili ya kuimarisha masuala ya ulinzi wa watoto Zanzibar.

### 1.6. Malengo ya Utafiti

Lengo la kufanya utafiti huu ni kuangalia mapungufu ya Sheria ya Watoto Nam. 6 ya mwaka 2011 na kupendekeza marekebisho yake Serikalini. Mapendekezo hayo yatazingatia:

(a) Kupendekeza utaratibu mzuri wa kisheria ili kuziwezesha taasisi za Serikali na zisizokua za Serikali zinazoshughulikia masuala ya watoto ziweze kuendesha shughuli zake kwa ufanisi zaidi;

(b) Kuboresha mfumo wa kisheria na kitaasisi katika kuwalinda watoto kutokana na mazingira yanayowazunguka na upatikanaji wa haki zao.

## 1.7. Njia zilizotumika katika Utafiti

Katika utafiti huu, njia mbali mbali zimetumika ambazo zimeweza kusaidia kupata taarifa na kuweza kufanikisha malengo yaliyokusudiwa katika utafiti huu. Njia hizo ni pamoja na kupitia rejea za ndani na nje ya nchi ikiwemo mikataba na miongozo ya kimataifa na uzoefu wa sheria za nchi nyengine, Katiba, Sera na Sheria mbali mbali. Njia nyengine iliyotumika katika utafiti huu ni kufanya vikao vya kukusanya maoni ya wadau na washirika muhimu katika eneo la ulinzi na uhifadhi wa mtoto

# SURA YA PILI

## 2.0 DHANA YA HAKI NA ULINZI WA MTOTO

### 2.1. Maana ya Neno Mtoto

Nyaraka mbali mbali zimemtafsiri mtoto kwa maana ya mtu yeyote aliye chini ya umri wa miaka 18.[47] Kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto (2009), inayotumika Tanzania Bara, na katika Sheria ya Watoto (2011), ambayo inatumika Zanzibar mtoto ni mtu yeyote aliye chini ya umri wa miaka 18. Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto nao umemtambua mtoto kama kila mwanadamu aliye chini ya umri wa miaka 18 isipokuwa, chini ya Sheria inayotumika kwa mtoto. Kulingana na Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto (1999), Kifungu cha 2 kimefafanua mtoto kuwa ni kila binadamu aliye chini ya umri wa miaka 18.[48]

[47] Law of the Child Act, 2009 49 African Charter on the Rigths and Welfare of the Child (ACRWC), 1990 50 Convention on the Rights of the Child (CRC), 1989 51 Tanzania Human Rights Report, 2013(supra) at p. 164

**[48] African Charter on the Rights and Welfare of the Child, OAU Doc. CAB/LEG/24.9/49 (1990), entered into force Nov. 29, 1999.**

## 2.2. Haki za Watoto

Haki za watoto ni miongoni mwa haki za binadamu, na zinalindwa kisheria, katika ngazi ya kitaifa na kimataifa. Haki za watoto ni haki ambazo zimewekwa ili kumfanya mtoto afurahie ustawi wake.[49]

Haki za watoto zimefafanuliwa na kulindwa katika Mkataba wa Haki za Mtoto na zinajumuisha haki za kijamii na kiuchumi, mitazamo ya kidini na kitamaduni ya mtoto, na jukumu la mtoto katika familia na jamii kwa ujumla.[50] Haki za watoto hazipaswi kutafsiriwa kwa kuzingatia muktadha wao kama watoto tu, lakini lazima zizingatie umuhimu wa mila na maadili ya kitamaduni ya kila watu maalum kwa ajili ya ulinzi na usawa wa maendeleo ya mtoto.[51]

Watoto wana haki kama binadamu yeyote ingawa haki zao kwa namna fulani ni za kipekee kwa kuzingatia kuwa watoto ni miongoni mwa makundi maalum katika jamii. Watoto wana haki zifuatazo; haki ya kuishi, haki ya kuishi bila ubaguzi wowote, haki ya kulindwa na kuheshimiwa, haki ya jina na utaifa, haki ya afya, haki ya elimu na haki ya utu nakadhalika.[52] Ikiwa watoto

---

[49] Shivji, I, Majamba, H, Makaramba, R and Maina, C. (2004). Constitutional and Legal System of Tanzania, A Civil Sourcebook. Mkuki na Nyota Publishers Ltd, Dar es Salaam katika ukurasa wa 157.

[50] ibid

[51] Mohammed, H and. Mashamba, C.J. (2014). Child Rights and the Law in East Africa, Lawafrica Publishing Co. (T) Ltd, Dar es Salaam ukurasa wa 22

[52] Ibid, ukurasa wa 29-35

wananyanyaswa kingono basi baadhi ya haki zilizotajwa hapo juu zinakiukwa pia.[53]

### 2.3. Matunzo na Ulinzi wa Mtoto

Neno ulinzi wa mtoto hutumiwa kuelezea huduma zinazoendeshwa na serikali katika kulinda watoto na kuhimiza utulivu wa familia. Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia maswala ya Watoto (UNICEF) linatumia neno ulinzi wa mtoto kwa maana ya kuzuia na kukabiliana na udhalilishaji, unyonyaji na unyanyasaji dhidi ya watoto ikiwa ni pamoja na unyonyaji wa kibiashara wa kingono, usafirishaji haramu wa Watoto, utumikishwaji wa watoto na madhara yanayotokana na mila, kama vile ukeketaji na ndoa za utotoni.[54]

### 2.4. Mfumo wa Ulinzi wa Watoto

Mfumo wa ulinzi wa watoto unahusisha za kina na endelevu za kuzuia na kukabiliana na unyanyasaji dhidi ya watoto, zinazojumuisha Sheria, Sera, Kanuni na huduma zinazohitajika katika sekta zote za kijamii, hasa ustawi wa

[53] Plan International, (2012). Child Protection Programming: Thematic Review on Child Protection, New Image Publishers, New York katika ukurasa wa 7

[54] Mashamba,C.J. (2009) .The Justice Review Special Commentary on the Tanzanian Law of the Child Act 2009, Volume 8 no.2.2009, National Organisation for Legal Assistance, Dar es Salaam katika ukurasa wa63

jamii, elimu, afya, usalama na haki.[55] Mfumo wa ulinzi wa mtoto unalenga kushughulikia unyanyasaji au udhalilishaji dhidi ya watoto, ili kuimarisha mwitikio dhidi ya unyanyasaji wa watoto (unaojumuisha unyanyasaji wa kijinsia) na kuwezesha Serikali kuendeleza ulinzi wa kina wa watoto kitaifa.[56]

Katika ngazi ya jamii, kuna haja ya kubadili mitazamo na Kanuni katika jamii yoyote, na kuwa mstari wa mbele dhidi ya unyanyasaji wa watoto ili kuimarisha ulinzi wao. Aidha, kuna haja ya kurekebisha Kanuni na tabia za kijamii na kitamaduni zilizowekwa kwa kina, kuhimiza watoto kutafuta usaidizi bora wa kitaaluma na kuripoti matukio ya ukatili kwa taasisi za Serikali.[57] Bila ya Sera madhubuti inayoungwa mkono na Sheria, programu na mikakati inayowekwa ni vigumukufanikiwa. Jitihada za kukabiliana na ukatili dhidi ya watoto zinahitaji uratibu madhubuti kutoka kwa Taifa, Wilaya na kila eneo ili hatua madhubuti za ulinzi wa watoto ziweze kusimamiwa.[58]

---

[55] United Nations Children's Fund, (2012). *Measuring and Monitoring Child Protection Systems: Proposed Core Indicators for the East Asia and Pacific Region,* Strengthening Child Protection Series No. 1. UNICEF EAPRO, Bangkok, 2012

[56] Save the Children, (2012). Desk Review and Analysis of Literature on Child Protection System in the Eastern Africa Region (Unpublished) at pp. 37-38 67Violence against children in Tanzania: Findings from a National Survey, 2009, Dar es Salaam, UNICEF at pp. 15-20

[57] UNICEF – Update of the Analysis of Women and Children in Zanzibar, 2006 Zanzibar (Unpublished).

[58] Mwafisi, M. J. (2007). Agenda 66 on Promotion and Protection of the Rights of Child. Permanent Secretary, Ministry of Community Development, in the third committee of the 6 session of the General Assembly.

## 2.5. Unyanyasaji wa Mtoto

Unyanyasaji wa mtoto ni ukiukaji wa haki za mtoto unaojumuisha madhara ya kimwili, unyanyasaji wa kihisia au kisaikolojia kwa mtoto, na wakati mwengine unyanyasaji wa kijinsia kwa mtoto ambao hufanywa kwa makusudi na watu wazima na wakati mwengine huhusisha uhusiano wa Kifamilia.[59] Wanaume na wanawake huwanyanyasa watoto kwa takriban katika matukio yanayokaribiana kwa sababu mara nyingi, mtoto anapojeruhiwa, mhalifu ni mtu anayejulikana kwa mtoto kama mzazi wa mtoto, mlezi au mhifadhi; mtu mwengine wa kaya au familia; au mtu mwengine mwenye uwezo wa kumfikia mtoto mara kwa mara.[60]

Ulinzi wa watoto maana yake ni kumlinda mtoto dhidi ya unyanyasaji wa watoto au kutelekezwa. Vile vile, katika hali ambayo mtoto anaweza kuwa amenyanyaswa au kupuuzwa, hatari ya unyanyasaji wa siku zijazo haijatambuliwa, mtoto na familia yake wanaweza kuhitaji usaidizi na huduma ili kuhakikisha ulinzi wa mtoto.[61]

---

[59] Mrisho, F. (2010). Sexual Abuse Report: The magnitude, risk factors and social cultural dynamics for Sexual Abuse and Early Sexual debut among In and out of School Adolescents in Tanzania.

[60] Abbott, G. (2004). What can we do about child abuse? The Office of the Attorney General with the cooperation of Texas CASA, Inc.

[61] United Nations Children's Fund, (2012). *Measuring and Monitoring Child Protection Systems: Proposed Core Indicators for the East Asia and Pacific Region,* Strengthening Child Protection Series No. 1. UNICEF EAPRO, Bangkok, 2012

Ulinzi wa mtoto ni neno pana la kuelezea falsafa, viwango, miongozo na taratibu za kulinda watoto dhidi ya madhara ya kukusudia au bila kukusudia. Ulinzi wa mtoto pia unawekwa ili kuhakikisha kuwa shughuli zozote zinazofanywa hazidhuru ustawi wa watoto.

Mfumo wa kisheria na Sera zinazolinda unyanyasaji na ukatili wa watoto inabidi kutambua kwamba watoto wana haki ya kulindwa, kuwezeshwa na kuchukua jukumu la kuzuia na kukabiliana na ukatili dhidi yao.[62]

[62] Cleland, A. (2008). Child abuse, child protection and the Law 1 st Edition, W.Green&son Ltd, London katika ukurasa wa 169

# SURA YA TATU

## 3.0 MIPANGO YA KITAIFA, SERA NA SHERIA MBALI MBALI

## 3.1. Utangulizi

Sura hii ya Tatu inaelezea Mipango Mikuu ya Kitaifa kama vile Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya 2020 - 2025 na Dira ya Maendeleo Zanzibar 2050 ambayo inatoa miongozo juu ya misingi ya haki, ulinzi na utunzaji wa watoto katika jamii. Aidha, sura hii imeeleza juu ya mitazamo ya Sera na Sheria mbali mbali ambazo kwa namna moja ama nyengine zinatoa muongozo wa kusimamia masuala yanayohusiana na haki pamoja na ulinzi kwa watoto.

Suala la kulinda na kusimamia haki za watoto limeguswa katika Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, Sheria na Sera mbali mbali ikiwemo Sera ya Uhakika wa Chakula na Lishe ya Zanzibar, Sera ya Michezo, Sera ya Hifadhi ya Jamii Zanzibar, Sera ya Ajira, Sera ya Watu Wenye Ulemavu pamoja na Sera ya Afya.

## 3.2. Mipango Mikuu ya Nchi

### 3.2.1. Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) 2020-2025

Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya 2020-2025 inatambua kuwa watoto wanayo haki ya kuishi, kutoa mawazo, kupata lishe bora, malezi, ulinzi, elimu na kutobaguliwa kwa namna yoyote.[63] Ilani hii kupitia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanikiwa kuimarisha haki za watoto kwa kutoa uelewa juu ya biashara ya usafirishaji haramu wa binadamu kwa Taasisi za Serikali na Taasisi binafsi ili kudhibiti biashara hiyo (biashara ambayo pia inahusisha usafirishaji haramu wa watoto); kuendelea kuwatunza na kuwahudumia watoto waliopo katika nyumba ya Serikali ya kulelea watoto Mazizini kwa kuwapatia elimu, michezo, lishe bora, huduma ya afya na mazingira yanayowajenga kimwili, kiakili na kimaadili. Ilani imetekelezwa kwa kuanzisha na kuendeleza kamati za wazazi katika Shehia za Unguja na Pemba na kuzijengea uwezo juu ya malezi bora, kujikinga na vitendo vya ukatili na udhalilishaji pamoja na kuchukua hatua ya kuripoti matukio hayo; na kuandaa mwongozo wa mafunzo ya walimu wa ushauri nasaha katika maskuli.[64]

Aidha, Ilani katika kuhakikisha mtoto wa Zanzibar anakuwa katika mazingira salama, imeweka mikakati inayotakiwa kutekelezwa kupitia Serikali kwa

[63] Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020-2025 (**mazingatio maalum ya ilani**) Namba 208, uk.264
[64] Ibid,kuyaendeleza makundi mbalimbali Namba 207

kipindi cha miaka mitano (2020-2025).[65] Miongoni mwa mikakati hiyo ni kama ifuatayo:-

(a) Kuhamasisha na kuelimisha jamii juu ya kuimarisha malezi bora na upigaji vita udhalilishaji wa watoto kupitia vyombo vya habari;

(b) Kuendeleza na kuunda mabaraza mapya ya watoto pamoja na kuratibu vikao vya mabaraza hayo. Aidha, Ilani pia imeeleza kuwa mabaraza yote ya vijana yataimarishwa kwa kujengewa uwezo juu ya kujikinga na kuripoti matukio ya ukatili na udhalilishaji wa watoto;

(c) Kutoa huduma katika kituo cha kurekebisha tabia kwa watoto wanaofanya makosa kilichopo Madema;

(d) Kutoa huduma kwa watoto wanaolelewa katika kituo cha Watoto cha Mazizini na kutayarisha na kuendesha nyumba salama kwa wahanga wa udhalilishaji wenye kuhitaji hifadhi; na

(e) Kusimamia uendeshaji wa vituo binafsi vya kulelea watoto ili kutoa malezi bora kwa mujibu wa sheria.

[65] Ibid, kuyaendeleza makundi mbali mbali Namba 208, uk 264-265

Hivyo, Ilani ya Chama Cha Mapinduzi imezingatia umuhimu wa makundi maalum wakiwemo watoto katika kuhakikisha kundi hilo linaangaliwa kwa karibu na kulindwa katika kusimamia ustawi wao.

### 3.2.2. Dira ya Maendeleo Zanzibar ya 2050

Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2050 katika msingi wake wa pili ambao unazungumzia kuhusu rasilimali watu na huduma za kijamii, [66] umejiwekea mkakati wa kukuza jamii yenye furaha na utulivu iliyoimarishwa kwa ustawi wa jamii, kuishi pamoja kwa amani na ajira yenye staha, iliyojikita katika kulinda makundi hatarishi. [67] Matarajio ya Dira kupitia mkakati huo yamejikita katika mambo mbali mbali ambayo yamegusa katika maeneo muhimu ya kumlinda mtoto.[68]

Miongoni mwa matarajio ya Dira ni kuwa na jamii yenye usawa inayolinda na kuwawezesha wanawake, watoto, watu wenye ulemavu na watu wengine walio katika mazingira magumu. Eneo jengine muhimu linalotarajiwa na Dira katika kumlinda mtoto ni kuwa na mfumo wa huduma za usaidizi wa kijamii, ikijumuisha kituo cha mkono kwa mkono, vituo vya matibabu, huduma za

---

[66] Zanzibar Development vision 2050, pillar II(Human capital and social services)

[67] Ibid, Ulinzi wa Jamii na Ajira, namba 2.5 uk. 39

[68] Ibid, uk.40-41

kisheria, urekebishaji wa huduma za kisaikolojia na huduma nyengine kwa waathirika wa unyanyasaji wa kujinsia na waathirika wa matumizi ya dawa za kulevya. Eneo jengine linalotarajiwa na Dira ni kuwa na wafanyakazi wa ustawi wa jamii waliofunzwa vya kutosha kutoa huduma, usimamizi wa kesi za udhalilishaji wa watoto na ufuatiliaji.

Aidha, Dira ina matarajio ya kutoa ulinzi dhidi ya vitendo viovu, kama vile vurugu dhidi ya wanawake, watoto na watu wenye ulemavu pamoja na ajira za watoto za kulazimishwa, kupitia utekelezaji wa mipango husika ya kitaifa

## 3.3. Sera

### 3.3.1. Sera ya Uhakika wa Chakula na Lishe ya Zanzibar ya mwaka 2008

Sera hii inasistiza na inafuata mwelekeo utakaohakikisha kwamba kunakuwepo na upatikanaji na matumizi endelevu ya chakula bora kwa watu wote. Mwelekeo huu unaenda sambamba na matamko mbali mbali ya kimataifa na kikanda ambayo yanahakikisha mtoto miongoni mwa haki zake za msingi ni kupata chakula bora na matunzo ya afya na kinga.[69]

[69] Sera ya Uhakika wa Chakula na Lishe ya Zanzibar, ( IV dhamira ya mkakati wa Sera ) UK. 26

Lengo kuu la Sera ya Uhakika wa Chakula na Lishe ni kujenga mazingira bora ambayo yatawawezesha wananchi wote wa Zanzibar (wakiwemo watoto) kuwa na uwezo wa kupata chakula bora na cha kutosha na ambacho kinakubalika katika mazingira yaliyopo kwa muda wote.[70] Pamoja na hayo, Sera inalenga pia kutoa hifadhi maalum kwa makundi ya watu walio katika hatari ya kutokuwa na uhakika wa kupata chakula, ambapo kupitia watu hao, Serikali inaweza kutoa msaada kwa mtu ambaye ana jukumu la kumtunza mtoto, pindi atakaposhindwa kupata chakula kutokana na uwezo wake mdogo ili kumpatia mtoto huyo lishe bora.

Sera pia inaeleza kuwa kila mtu ana haki ya kupata chakula bora na cha kutosha kwa ajili ya maisha bora na afya njema kama ilivyoelezwa na Azimio la Kimataifa la Haki za Binaadamu, Azimio la kimataifa la haki za Kiuchumi, kijamii na kiutamaduni na maazimio mengine ya kimataifa.[71]

### 3.3.2. Sera ya Michezo ya Mwaka 2018

Sera hii imeweka misingi ya usawa, ambapo watu wote wana fursa sawa katika michezo na haki zao zinatambuliwa na kuthaminiwa.[72] Vile vile Sera inaeleza

[70] Ibid,(shabaha kuu ya Sera ya uhakika wa chakula na lishe) uk. 26

[71] Ibid, (mikakati ya kufikia malengo ya utekelezaji wa misingi ya Sera) uk. 27

[72] Sera ya Michezo, 2018 (2.2 misingi ya michezo) uk.13

kuwa kila mtu ana fursa sawa katika michezo na atathaminiwa kwa uwezo na kipaji chake bila ya ubaguzi wa aina yoyote.[73] Kwa masharti hayo ya Sera, ni dhahiri kuwa kundi la watoto ambalo limekuwa likijihusisha sana na masuala ya michezo, limewekewa ulinzi wa kutosha katika kuitumia haki hiyo ya michezo.

Lengo kuu la Sera hii ni kuweka utaratibu wa kitaifa wa kuwawezesha watu wote kushiriki katika michezo kwa maendeleo ya kijamii, kielimu, kiuchumi na kiafya, pamoja na kuibua, kukuza na kuendeleza vipaji vya wanamichezo, kuimarisha miundombinu ya michezo na kutoa mafunzo ili waweze kushirikiana na kushindana katika michezo ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa.[74]

Sera ya Michezo imetayarishwa ili kuhakikisha kunakuwepo na mafunzo na mashindano mengi ya timu za watoto, watu wenye mahitaji maalum, watu wenye ulemavu, vijana wa kike na kiume kuanzia ngazi ya Shehia hadi Taifa kupitia vyama vyote vya michezo katika kuinua vipaji nchini; kukinga na kupinga matumizi ya dawa za kulevya na kuongeza nguvu michezoni.[75] Mwelekeo huu wa Sera unaonesha wazi kuwa unawajali watoto katika

---

[73] ibid

[74] Ibid uk. 14 (2.5 lengo kuu)

[75] Ibid, (2.6 malengo mahsusi) uk. 15

kuimarisha afya zao na kuburudika kupitia michezo na kupata ulinzi dhidi ya kujiingiza katika makundi mabaya ambayo mara nyingi yanapelekea matumizi ya madawa ya kulevya na kufanyika vitendo vyengine viovu.

### 3.3.3. Sera ya Hifadhi ya Jamii Zanzibar ya mwaka 2014

Sera hii imeanzishwa kwa lengo la kuweka mfumo utakaojitosheleza ambao utahakikisha unailinda jamii katika usalama wa kipato, udhibiti wa majanga au hali zinazopelekea watu kuingia katika umasikini na kuhakikisha upatikanaji wa huduma za kimsingi kwa wazanzibari wote.[76]

Miongoni mwa malengo mahsusi ya Sera hii ni kupanua hatua kwa hatua upatikanaji wa huduma za kimsingi za kijamii kama vile elimu, huduma za afya, ustawi wa jamii na huduma za ulinzi wa watoto na kuhakikisha kuwa ubora wao hautohatarishwa.[77] Aidha, katika kulinda maslahi ya mtoto, Sera imeweka mikakati kwamba Serikali na wadau wengine watahakikisha kwamba watoto wote wanaozaliwa wanapata fursa ya kusajiliwa mara tu watakapozaliwa. Mikakati mengine iliyowekwa na Sera ni kupunguza gharama za elimu kwa watoto wote wa Zanzibar ili kupunguza idadi ya watoto wanaokatisha shule

---

[76] Sera Ya Hifadhi Ya Jamii Zanzibar2.4 malengo. Uk. 16

[77] Ibid, (1.6 haja ya kuwa na Sera ya Hifadhi ya jamii) uk. 14

miongoni mwa watoto walio katika mazingira magumu hususan watoto wenye ulemavu na kutokomeza aina zote za ukatili dhidi ya watoto Zanzibar.[78]

Vile vile mapambano dhidi ya udhalilishaji yamewekwa kama ni sehemu katika Sera hii. Mkakati wa mapambano hayo ni wa kuimarisha mifumo ya Serikali na jamii kwa ajili ya kupambana na udhalilishaji na ukatili dhidi ya watoto; kuimarisha upatikanaji wa huduma za hifadhi ya mtoto na kushajihisha elimu kwa umma kwa ajili ya kupambana na udhalilishaji na ukatili kwa watoto.[79]

### 3.3.4 Sera ya Ajira Zanzibar ya mwaka 2009

Sera ya Ajira Zanzibar ya mwaka 2009 imejikita katika kutokomeza ajira mbaya za watoto ambazo zinasababisha watoto kupata athari kiakili, kimwili, kijamii, kiroho na kimaadili.[80] Dhamira hii nzuri ya Serikali inalenga kuwawekea watoto mazingira bora ambayo yatapelekea makuzi yao kuwa mazuri na salama.

---

[78] Ibid uk. 18-21

[79] Ibid,3.3.2.2 vitendo vya udhalilishaji na ukatili wa kijinsia, uk.22

[80] Sera ya Ajira Zanzibar, 2009 uk.35

Tamko la Sera hii limeonesha kuwa Serikali na wadau wengine watatoa miongozo na programu za utekelezaji wa shughuli za kutokomeza ajira za watoto,[81] hasa katika ajira mbaya za watoto. Hii inaonesha kwamba watoto hawakatazwi kufanya kazi ila kazi hizo zisiwakoseshe watoto hao fursa ya kupata elimu, kucheza na haki zao nyengine zote kama zilivyoainishwa katika Sheria na mikataba mbali mbali.

Miongoni mwa mikakati ya Sera katika kutokomeza ajira za watoto ni kuwezesha familia kiuchumi ili kupunguza ajira za watoto; kuelimisha jamii kuhusu tatizo la ajira za watoto na athari zake; kuingiza mada inayohusu ajira za watoto katika mitaala ya skuli; na kusambaza kwa wadau wa kazi na ajira miongozo ya kitaifa na kimataifa inayohusu hatua za kutokomeza ajira za watoto.[82]

Hivyo, Sera hii inatekeleza mikataba ya kimataifa na kikanda katika kuhakikisha mtoto anaishi katika mazingira salama ili kulinda maslahi bora ya mtoto wa Zanzibar.

---

[81] ibid

[82] Ibid kif. 35-36

### 3.3.5 Sera ya Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2018

Sera hii inaonesha kuwa Wanaume na wanawake, vijana na watoto wenye ulemavu wametengwa kwa kiasi kikubwa kwa sababu ya ulemavu wao na pia wako katika hatari kubwa ya unyanyasaji wa kingono.[83]

Aidha, Sera imeainisha uwepo wa kiwango cha chini cha ujumuishaji wa masuala yanayohusiana na ulemavu katika Taasisi za Serikali. Sera hii imeweka mkakati wa kuimarisha kinga, ulinzi, kutoa taarifa na kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia dhidi ya wanaume, wanawake na watoto wenye ulemavu.[84] Hivyo, Sera inaonesha dhamira ya Serikali ya kuwalinda watoto wenye ulemavu kutokana na unyanyasaji wa kijinsia kwa kuweka mikakati madhubuti ambayo imo katika kuhakikisha mtoto huyo hafanyiwi vitendo viovu kutokana na ulemavu wake na badala yake ustawi wa mtoto mwenye ulemavu unazidi kuimarika.

### 3.3.6 Sera ya Afya ya mwaka 2011

Sera hii imejiegemeza zaidi katika kuimarisha huduma za afya za kinga na tiba na kuendeleza ustawi wa watu wa Zanzibar kwa kutilia mkazo zaidi wanawake,

---

[83] Sera ya watu wenye ulemavu Zanzibar, 2018 uk.39

[84] Ibid uk.40

watoto pamoja na makundi mengine yanayoishi katika mazingira magumu.[85] Sera hii katika utoaji wa huduma za afya imeonesha jinsi Serikali inavyoiwezesha sekta ya afya kufikia malengo na shabaha za Sera za Taifa na kimataifa kwa kuweka msisitizo katika upatikanaji wa huduma za mama na mtoto, upatikanaji wa matibabu ya maradhi ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza. Lengo la Sera ni kutoa fursa sawa ya upatikanaji wa huduma za msingi za kinga na tiba zilizo bora kama vile huduma za afya ya uzazi na mtoto, uchunguzi wa mapema, urekebishaji, magonjwa ya muda mrefu na huduma za dharura. Miongoni mwa mikakati[86] ya Sera katika kutekeleza lengo lake hilo ni:

a. Kuimarisha huduma za afya kwa wanaobakwa na pia kwa makosa mengine ya jinai wanayofanyiwa wanawake na watoto.
b. Upatikanaji wa huduma za afya ya uzazi na mtoto katika hali ya usawa, ubora na zenye kufikika.

## 3.4. Sheria

### 3.4.1. Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984

Katiba ya Zanzibar imeingiza haki za binadamu kwa ujumla bila ya kutenganisha baina ya makundi kama ya watoto, watu wenye ulemavu na watu

[85] Sera ya Afya Zanzibar, 2011, uk. 18

[86] Ibid uk.20-21

wengine. Haki za binadamu zinachukuliwa kama zimejumuisha mtoto kwa sababu ni sehemu ya binadamu. Sura ya Tatu ya Katiba imeweka kinga ya haki za msingi, wajibu, na uhuru wa mtu binafsi. Miongoni mwa haki na wajibu uliowekwa katika Katiba ni usawa wa binaadamu,[87] haki ya kuwa hai,[88] haki ya uhuru wa mtu binafsi,[89] haki ya faragha ya mtu na usalama wake,[90] kinga ya uhuru wa kwenda[91]uhuru wa kutoa maoni[92] na uhuru wa mtu kuamini dini aitakayo.[93] Haki na wajibu mwengine ulioainishwa katika sehemu hiyo ya Katiba ni uhuru wa kushiriki shughuli za umma, haki ya kufanya kazi na kupata ujira,[94] wajibu wa kushiriki kazini,[95] wajibu wa kutii Sheria za nchi, kulinda mali za umma na ulinzi wa Taifa.[96] Katiba pia imetaka kuhakikisha uwepo wa huduma za kutosha za kiafya kwa watu wote, fursa sawa za elimu kwa madaraja

---

[87] Ibid, kifungu cha 11 kinaeleza kuwa binaadamu wote huzaliwa huru, na wote ni sawa.

[88] Ibid, kifungu cha 13

[89] Ibid, kifungu..14

[90] Ibid, kifungu cha.15

[91] Ibid, kifungu cha.16

[92] Ibid, kifungu cha.18

[93] Ibid, kifungu cha. 19

[94] Ibid, kifungu cha. 21

[95] Ibid, kifungu cha.22

[96]Ibid, kifungu cha 23

yote na uhakika wa kulindwa kwa utamaduni wa mzanzibari. Vilevile Katiba imetoa fursa kwa kila anaeweza kufanya kazi afanye kazi na kuhakikisha msaada unatolewa kwa wasiojiweza, wazee, wagonjwa, watoto na watu wenye ulemavu.[97] Kama ilivyoelezwa awali, haki hizi zilizoelezwa katika Katiba ya Zanzibar, pia zinamgusa mtoto kama sehemu ya watu katika jamii.

### 3.4.2. Sheria ya Watoto Nam. 6 ya Mwaka 2011

Sheria hii imetungwa pamoja na mambo mengine, kuweka haki muhimu za watoto zinazotokana na mikataba ya kimataifa na kikanda iliyozingatia maslahi bora ya mtoto. Sheria katika kuzingatia maslahi bora ya mtoto, imemuwekea mtoto huyo mahitaji maalum ambayo kupatikana kwake kutapelekea kumkuza mtoto katika mazingira mazuri. Baadhi ya mambo muhimu yaliyomo katika Sheria hii ni :

#### (a) Haki na ustawi wa mtoto

Sheria hii imeainisha haki za mtoto ambazo ni muhimu. Miongoni mwa haki hizo muhimu ni pamoja na maslahi bora ya mtoto,[98] matunzo, ulinzi, na ustawi

[97] kifungu cha 10 (f) &(g)

[98] Sheria ya Watoto Nam.6 ya Mwaka 2011, k ifungu cha 3

wa mtoto, kanuni ya kutobaguliwa,[99] na ushiriki wa mtoto[100] katika mambo yanayowahusu kupitia Mabaraza ya Watoto. Vilevile Sheria imeweka[101] vifungu vinavyohusiana na usajili wa vizazi,[102] ulezi,[103] usimamizi,[104] upatikanaji wa matunzo,[105] kuasili watoto,[106] huduma za afya kwa watoto,[107] na vituo maalum vilivyoanzishwa kwa watoto.[108] Pia Sheria imetoa wajibu kwa taasisi za kitaifa na wataalam, katika kumlinda mtoto, na kukabiliana na matukio ya watoto wanaohitaji matunzo na ulinzi.

Sheria katika kifungu cha 10, imeweka haki, masharti na taratibu za utekelezaji wa haki ya mtoto kuishi katika mazingira mazuri ya ukuaji[109] kama vile lishe,

---

[99] Kifungu cha 6

[100] Kifungu cha 5

[102] Kifungu cha 8

[103] kifungu cha 58

[104] Kifungu cha 59

[105]Kifungu cha 61 na 63

[106] Kifungu cha 72 na 77

[107] Kifungu cha 111

[108] Kifungu cha 123

[109] Ibid, Kifungu cha 10

elimu (ikiwa ni pamoja na elimu ya dini), malazi, matibabu, michezo, mavazi yanayofaa, na matunzo na ulinzi ambapo ni wajibu wa mzazi kumlinda mtoto kulingana na uwezo wa mzazi huyo.

Mbali na hayo, Sheria imetoa katazo kwa wasimamizi na walezi kuwanyanyasa watoto kwa hali yoyote.[110] Sheria hii pia imetoa ulinzi kwa watoto wenye ulemavu kwa kuweka jukumu kwa watu wote pamoja na taasisi kuwajali na kuwapatia huduma sawa watoto hao, bila ya kuwabagua.[111]

### (b) Matunzo na ulinzi wa mtoto

Sheria imeweka vifungu vya kumlinda mtoto ambaye anahitaji ulinzi kutokana na sababu ambazo zimeainishwa ikiwemo mtoto yatima, maskini au aliyetelekezwa na wazazi au walezi wake, kufanya kazi katika mazingira hatarishi au kuombaomba.[112] Sheria imeweka jukumu kwa watu maalum ambao inaaminika wanaweza kujua kuhusu ukiukwaji wa haki za mtoto, kutoa taarifa kwa Mkurugenzi wa Ustawi wa Jamii, Afisa Ustawi wa Jamii, Jeshi la Polisi au Sheha.[113] Sheria pia imeeleza hatua ambazo Afisa ustawi atazifuata

---

[110] Ibid, kifungu cha 15

[111] Ibid, kifungu cha 11

[112] Ibid, Kifungu cha 19

[113] Ibid kifungu cha 20

baada ya kupokea taarifa za ukiukwaji wa haki za mtoto na kama itaonekana inafaa, ataomba amri ya ulinzi wa dharura.[114]

**(c) Watoto wanaofanya makosa**

Sheria imeweka msingi wa kisheria wa mbinu bora na tofauti za kushughulikia kesi za watoto waliofanya makosa, na inaelezea ulinzi maalum kwa watoto kwa kuweka utaratibu katika hatua zote za mchakato wa haki jinai [115] (kukamatwa,[116] uchunguzi,[117] dhamana,[118] kesi, hukumu[119] na urekebishaji).

Sheria pia imeanzisha kanuni ya njia za kushughulikia makosa ya watoto kwa kuwapa Jeshi la polisi mamlaka ya kutahadharisha na kuruhusu waendesha mashtaka kutatua makosa madogo madogo kwa njia ya onyo; msamaha wa mdomo au maandishi; tahadhari rasmi; kumpeleka mtoto aliyefanya makosa kupata ushauri au matibabu; au kulipa fidia kwa mwathirika. [120] Sheria

[114] Kifungu cha 21 & 22

[115] Ibid, Kifungu cha 43

[116] Ibid, Kifungu cha 37

[117] Ibid, Kifungu cha 46

[118] Ibid, Kifungu cha 45

[119]Ibid, Kifungu 47

[120]Ibid Kifungu cha 42

inawahakikishia watoto haki ya kuwakilishwa kisheria na kuungwa mkono na mzazi au mlezi wakati wote wa kesi.[121]

### (d) Mahakama ya watoto

Sheria ya Watoto pia inaanzisha Mahakama maalum ya watoto yenye mamlaka ya kusikiliza na kutoa maamuzi juu ya mashauri yanayohusiana na ulinzi na uangalizi wa mtoto, maombi yanayohusu matunzo ya mtoto, ulezi na usimamizi wa mtoto na kusikiliza na kuamua makosa yote ya jinai yaliyofanywa na mtoto isipokua makosa ya kuua, uhaini, na kubaka.[122] Mahakama ya Watoto imeanzishwa kisheria ili kuhakikisha mashauri yote yanayohusu watoto yanasikilizwa na kuamuliwa kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa Sheria hii.

Sheria ya Watoto pia inajumuisha kifungu cha ushahidi wa mtoto alieathiriwa katika kesi za jinai.[123] na imeruhusu kuchukuliwa ushahidi huo kama mashahidi wengine ikiwa mtoto huyo atakidhi masharti ya kifungu hicho.

### (e) **Ulinzi kwa watoto katika ajira**

---

[121] Ibid kifuungu cha 38

[122] Ibid kifungu cha 18

[123] Ibid, kifungu cha 49

Sheria imetoa nafasi kwa mtoto kufanya kazi kwa masharti maalum.[124] Ili mtoto aweze kufanya kazi kwa mujibu wa Sheria hii, ni lazima awe ametimiza umri wa miaka 15 au zaidi na kazi hiyo iwe ni nyepesi na ambayo haitoathiri afya au mahudhurio yake ya shule au kumkosesha fursa za kucheza.[125] Vile vile mtoto hatakiwi kuajiriwa kufanya kazi ambazo zitamnyima haki zake[126] ikiwemo kumfanyisha kazi zaidi ya masaa sita au zaidi ya saa mbili usiku au kumfanyisha kazi za hatari.[127] Sheria hii pia imeainisha haki ya mtoto kupata malipo kwa kazi alizozifanya,[128] kutolazimishwa kufanya kazi[129] na kutofanyishwa kazi au biashara za kingono.[130]

---

[124] Ibid, kifungu cha 97

[125] Ibid, kifungu cha 98

[126] Ibid, kifungu cha 99

[127] Ibid, kifungu cha 100

[128] Ibid, kifungu cha 101

[129]Ibid, kifungu cha 102

[130] Ibid, kifungu cha 110

### 3.4.3. Sheria ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar, Nam.3 ya mwaka 2018

Sheria hii imeanzisha Wakala wa Serikali inayojulikana kama Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar.[131] Miongoni mwa kazi za Wakala huu ni pamoja na kutengeneza, kusimamia, kutunza na kuendeleza rejista la matukio ya kijamii ikiwemo tukio la kizazi cha mtoto, kutoa cheti cha kuzaliwa cha mtoto na kuhakikisha uhifadhi, ulinzi na usalama wa taarifa ya mtoto na taarifa nyengine yoyote au taarifa zilizokusanywa, zilizopatikana au zilizohifadhiwa katika rejista.[132]

Mkurugenzi Mtendaji au mtu aliyekasimiwa madaraka, atasajili vizazi na ataingiza katika rejista au ataagiza kuingizwa taarifa za vizazi zilizomo katika tangazo.[133] Mzazi, mlezi au mtu aliyekuwa na dhamana ya mtoto, mara tu baada ya kuzaliwa mtoto au kumpata mtoto, atamjulisha Afisa wa Usajili au Sheha kwa ajili ya kusajili kizazi hicho.[134]

---

[131] Sheria ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar Nam.3 ya 2018, Kifungu cha 3

[132] Ibid, kifungu cha 4

[133] Ibid, kifungu cha 21

[134] Ibid, kifungu cha 22

Vile vile, Sheria imeweka jukumu kwa watu maalum la kutoa taarifa ya kizazi[135] kwa nia ya kutoa taarifa muhimu zinazohusu kizazi hicho kwa muhusika, Usajili wa mtoto aliyeokotwa,[136] na kubadilisha jina la mtoto.[137] Sheria imemtaka Mkurugenzi Mtendaji au mtu aliyekasimiwa madaraka kutoa cheti cha kuzaliwa[138] kwa mtoto aliyezaliwa mara baada ya kujiridhisha na taarifa zilizotolewa kuhusu mtoto huyo. Vifungu hivi vyote vinaweka utaratibu wa utekelezaji wa moja ya haki muhimu za mtoto za kupewa jina na kusajiliwa rasmi.

#### 3.4.4. Sheria ya Kuwalinda Wari na Watoto wa Mzazi Mmoja, Nam. 4 ya 2005

Sheria hii imemlinda mtoto wa kike ambaye amepata ujauzito kwa kuweka masharti yanayobainisha mtoto huyo kupata haki yake ya elimu baada ya kujifungua.[139] Vile vile, Sheria hii imeweka kifungu cha kumlinda mtoto aliyezaliwa kwa kumtaka baba aliyesababisha ujauzito huo kwa binti huyo,

---

[135] Ibid, Kifungu cha 22

[136] Ibid kifungu cha 24

[137] Ibid kifungu cha 25

[138] Ibid kifungu cha 26

[139] Sheria ya Kuwalinda Wari na Watoto wa Mzazi Mmoja Nam. 4 ya Mwaka 2005. kifungu cha 4

mwari au mtalaka wake kutoa matunzo ya mtoto[140] wakati akiwa tumboni na baada ya kuzaliwa, ikiwa mtoto huyo hajatimiza umri wa miaka 18 au hajaanza kujikimu mwenyewe. Pia Sheria imeipa mahakama uwezo wa kumpa amri baba kutoa matunzo ya mtoto[141] ikiwa baba huyo atakataa kutoa matunzo hayo, Mahakama pia imepewa uwezo wa kuamuru mali ya baba kuwekwa kama dhamana kwa ajili ya kupata huduma za mtoto kupitia mali hiyo ya baba mtoto.[142]

### 3.4.5. Sheria ya Adhabu Nam. 6 ya Mwaka 2018

Sheria imeeleza kuwa mtu wa umri chini ya miaka kumi na mbili (12) hatowajibika kijinai.[143] Kwa mujibu wa kifungu hiki, mtoto yeyote mwenye umri wa chini ya miaka kumi na mbili, hatoweza kufunguliwa mashtaka kwa kosa lolote. Aidha, Sheria hii imeendelea kueleza kuwa mtoto mwenye umri wa chini ya miaka kumi na nne (14) hatowajibika kijinai kwa kosa alilofanya isipokuwa kama itathibitishwa kwamba wakati wa kutenda au kuacha kutenda

---

[140] Ibid kifungu cha 5 na 8

[141] Ibid kifungu cha 9

[142] Ibid kifungu cha 10

[143] Sheria ya Adhabu Nam.6 ya mwaka 2018, kifungu cha 13

kitendo hicho, alikuwa na uwezo wa kujua kwamba hapaswi kukitenda au kuacha kukitenda kitendo hicho.

Sheria katika sehemu yake ya Kumi na Tatu imeeleza kuhusu makosa dhidi ya maadili ambayo yanakusudia kulinda ustawi wa mtoto Zanzibar. Sheria imeeleza wazi kuwa ni kosa mwanaume kumbaka mtoto wa kike au mwanamke.[144] Mtu yeyote ambaye atabaka atapewa adhabu[145] ya kifungo cha maisha, au atapewa adhabu ya kutumikia Chuo cha Mafunzo kwa muda usiopungua miaka thelathini pamoja na faini, na zaidi ya adhabu hizo, ataamriwa alipe fidia kwa kiwango kitakachoamuliwa na Mahakama (isipokua kama kosa hilo kalifanya mtoto wa kiume, adhabu ya mtoto huyo itakua kama ilivyoelezwa katika Sheria).

Sheria hii pia imekataza kutorosha watoto wa kike na kiume[146] ambao wapo chini ya uangalizi wa wazee au chini ya dhamana ya mtu mwengine na ikaweka adhabu kwa mtu yoyote ambaye bila ya halali, anamchukua mtoto huyo. Pia

---

[144] Ibid kifungu cha 108

[145] Ibid kifungu cha 109

[146] Ibid kifungu cha 113

Sheria imetoa katazo kuvunjiwa heshima au kumfanyia shambulio la aibu mwanamke, au mtoto wa kike.[147]

Aidha, kunajisi mtoto wa kiume ni kosa chini ya Sheria hii na atakayefanya kosa hilo atapewa adhabu ya kifungo cha maisha.[148] Vilevile kunajisi mwanamke, mwanamme, mtoto wa kike au mtoto wa kiume mwenye ulemavu wa akili ni kosa chini ya Sheria hii.[149].

Sheria pia imetaja baadhi ya makosa likiwemo kosa la kuwezesha kufanyika ukahaba kwa njia yoyote ile ikiwa ni kuwezesha au kujaribu kuwezesha mtu au mtoto chini ya miaka kumi na nane kuwa kahaba ndani au nje ya Zanzibar,[150] kuwezesha ngono haramu kwa watoto au mwanamke.[151] Makosa mengine dhidi ya mtoto yaliyoainishwa katika Sheria hii ni mwenye nyumba kuruhusu mtoto wa kiume[152] au mtoto wa kike[153] kuingiliwa, kumzuia mwanamke, mtoto

[147] Ibid, kifuncu cha 114

[148] Ibid kifungu cha 115

[149] Ibid kifungu cha 116

[150] Ibid kifungu cha 117

[151] Ibid kifungu cha 118

[152] Ibid kifungu cha 119

[153] Ibid kifungu cha 120

wa kike au mtoto wa kiume katika danguro au katika jengo Iolote kwa nia ya kuingiliwa na mwanaume bila halali.[154]

Sehemu ya 14 ya Sheria hii inaelezea kuhusu makosa yanayohusiana na ndoa na mahusiano ya kifamilia. Sheria inaendelea kupinga ukatili dhidi ya watoto ambapo mtu yeyote mwenye mamlaka ya uhifadhi, uangalizi au utunzaji wa mtoto akibainika anamnyanyasa, anampuuza au anamtelekeza mtoto huyo na kumsababishia madhara, atawajibika kwa makosa hayo.[155]

Vile vile Sheria hii inawataka wote wenye majukumu ya kuwatunza watoto wasiwatelekeze [156] au kuwakosesha chakula watoto au mtu mwenye ulemavu[157] na atakayefanya hivyo, atakua ametenda kosa. Pia kuiba mtoto[158] na kusafirisha binaadamu[159] ni kosa chini ya Sheria hii.

[154] Ibid, kifungu cha 121

[155] Ibid kifungu cha 149

[156] Ibid kifungu cha 150

[157] Ibid kifungu cha 151

[158] Ibid kifungu cha 154

[159] Ibid kifungu cha 153

Sheria pia imeweka wajibu wa kiongozi wa familia kumhudumia mtoto chini ya umri wa miaka 18 hata kama mtoto huyo anaweza kujihudumia au vyenginevyo.[160]

### 3.4.6. Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Nam. 7 ya mwaka 2018

Sheria hii imetungwa kwa lengo la kuweka utaratibu bora wa kufanya upelelezi wa makosa ya jinai na usikilizaji wa kesi za jinai na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Sheria inaeleza kwamba mtu aliyekamatwa hatotendewa jambo Iolote dhidi ya heshima yake wala hatodhalilishwa kimwili au kimaadili.[161] Aidha, mtu huyo atakuwa na haki ya kuipa taarifa familia yake, au taasisi ambayo yeye anahusika nayo kuhusu kukamatwa huko. Ikitokea mtu aliyekamatwa ni mtoto, au mwenye ugonjwa wa akili, au maradhi yoyote ambaye hawezi kuwasiliana na familia yake, au taasisi ambayo mtu huyo anahusika nayo, Polisi, Mwendesha Mashtaka au Mahakama, kwa jitihada zake yenyewe, itaijulisha familia au taasisi husika.[162]

---

[160] Ibid kifungu cha 189

[161] Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Nam. 7 ya mwaka 2018, kifungu cha 13

[162] Ibid, kifungu cha 13

Sheria pia katika kufanya upekuzi wa pahala alipoingia mtu anayetafutwa ili akamatwe, ukamataji hautofanywa isipokuwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii na, isipokuwa katika mazingira maalum, na mtoto au mwanamke hatokamatwa baada ya kuchwa kwa jua au kabla ya kuchomoza jua. Kwa mujibu wa Sheria hii, ukamataji wowote wa mtoto unaofanywa ni lazima ufuate masharti ya Sheria ya Watoto.[163]

Aidha, Sheria imewapa jukumu maafisa Polisi kutoa taarifa kwa wazazi au walezi wa watoto waliokinzana na Sheria kuhusiana na kosa alilofanya mtoto huyo ambalo limesababisha awekwe kizuizini.[164] Masharti haya ya Sheria ya Mwenendo wa Jinai imewazingatia watoto kwa hali yao na kutofautisha na mazingira ya watu wazima katika mchakato wa ukamataji na haki zinazoambatana na ukamataji huo, na mwenendo mzima wa uendeshaji wa mashauri ya jinai dhidi ya watoto hao.

### 3.4.7. Sheria ya Ushahidi Nam.9 ya mwaka 2016

Sheria hii katika sehemu ya Kumi na Nane, inaelezea kuhusu mashahidi wanaofaa kutoa ushahidi mahakamani. Sheria hiyo inaeleza kwamba watu

---

[163] Ibid, kifungu cha 14

[164] Ibid, kifungu cha 41

wote watakuwa na uwezo wa kutoa ushahidi katika mahakama.[165] Sheria inaendelea kwa kueleza mazingira ambayo mtu hatoweza kutoa ushahidi ikiwemo mtu huyo kutoelewa masuala anayoulizwa, au kutoa majibu ya msingi ya maswali hayo, ikiwa ana umri mdogo, uzee sana, maradhi yakiwa ya kimwili au ya kiakili, au sababu nyengine yoyote ya aina hiyo. Pale ambapo mtoto mwenye umri mdogo (mtoto ambaye umri wake hauzidi miaka kumi na nne) ataitwa kama shahidi kama haelewi maana ya kiapo, ushahidi wake utapokelewa ikiwa anafahamu wajibu wa kusema ukweli.[166]

Vilevile, Mahakama inaweza, baada ya kuchukua tahadhari juu ya hatari ya kutumia ushahidi huo (wa mtoto) kama haukuungwa mkono na ushahidi mwengine wowote, kumtia hatiani mshtakiwa kama itathibitika kikamilifu kwamba mtoto huyo anasema ukweli.[167] Pia ushahidi huo wa mtoto unaweza kutumiwa na Mahakama kama ushahidi wa msingi wa kuunga mkono ushahidi wa mtoto mwengine mwenye umri mdogo uliotolewa kabla au ushahidi uliotolewa na mtu mzima ambao unahitaji kuungwa mkono.[168] Mahakama

[165] Sheria ya Ushahidi ya Nam.9 ya Mwaka 2016, kifungu cha 133

[166] Ibid, kifungu cha 133(3)

[167] Ibid, kifungu cha 133(4)

[168] Ibid, kifungu cha 133(5)

katika kesi za kujamiiana itapokea ushahidi wa mtoto mdogo bila ya kujali kwamba ushahidi huo haukuungwa mkono ikiwa mtoto huyo au muathirika wa makosa ya kujamiiana hasemi chochote isipokuwa ukweli.[169]

Pia, Sheria imetoa maelezo kuhusu uchukuaji wa ushahidi kwa kutumia njia maalum kwa mashahidi ambao wapo katika mazingira hatarishi. Ushahidi huo unaweza kuchukuliwa kwa siri au moja kwa moja kwa njia ya mtandao au kurikodiwa kwa njia ya video au shahidi kutoa ushahidi bila kuwepo mshtakiwa.[170]

#### 3.4.8. Sheria ya Msaada wa Kisheria Nam. 13 ya mwaka 2018

Sheria hii imetungwa kwa lengo la kuweka masharti yanayosimamia utoaji wa huduma za msaada wa kisheria, kurahisisha upatikanaji wa haki na kuweka masharti mengine yanayohusiana na hayo.

Katika Sehemu ya Nne, Sheria inaelezea kuhusu huduma za msaada wa kisheria ambapo imeanzia kwa kutaja huduma hizo ikijumuisha utoaji wa ushauri wa kisheria, msaada au uwakilishi wa kisheria, elimu ya kisheria na taarifa kwa

[169] Ibid, kifungu cha 133(7)

[170] Ibid kifungu cha 134

watu wasiokuwa na uwezo na uwakilishi katika Mahakama au kwenye Baraza la Maamuzi.

Sheria imemtaka mtoa huduma za kisheria kuhakikisha anatoa huduma zenye ubora wa hali ya juu na kwa wakati kwa watu wasiokuwa na uwezo ambazo zinajumuisha ushughulikiaji wa watoto kitaalamu na kwa unyeti, watu wenye ulemavu, wazee, au watu wa makundi maalum.[171]

Sheria imeweka jukumu kwa mtu aliyepewa dhamana ya kusimamia ustawi wa mtoto ambaye anakinzana na Sheria, kumuwezesha mtoto huyo kupata msaada wa kisheria.[172] Vilevile, Sheria imewapa jukumu Jeshi la Polisi, Chuo cha Mafunzo au nyumba ya mahabusu ya watoto, kutengeneza utaratibu wa utoaji wa huduma za msaada wa kisheria kwa watoto na watu wengine walio kizuizini na kuhakikisha kwamba mtu aliyepo kizuizini, anajulishwa, katika lugha ambayo mtu huyo anaifahamu, kuhusu upatikanaji wa msaada wa kisheria wakati anawekwa kizuizini.[173]

---

[171] Sheria ya Msaada wa Kisheria INam. 13 ya Mwaka 2018, kifungu cha 21

[172] Ibid, kifungu cha 34

[173]Ibid, kifungu 35

### 3.4.9. Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu Nam. 6 ya mwaka 2008

Sheria hii ni ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na inatumika katika pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maana ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Sheria hii imebainisha vitendo vya usafirishaji haramu wa binaadamu,[174] na mtu anayehamasisha, kununua au kuwezesha usafirishaji haramu wa binadamu atakuwa ametenda kosa chini ya Sheria hii.[175] Sheria hii pia imeonesha baadhi ya vitendo ambavyo vitachukuliwa kuwa ni usafirishaji haramu wa watu ambao ni hatari zaidi ikiwa mtu aliyesafirishwa kwa njia haramu ni mtoto au mtu mwenye ulemavu.[176]

Sheria pia imebainisha kuwa fidia italipwa kwa aliyesafirishwa kwa njia haramu, mbali na adhabu aliyopewa aliyetenda kosa hilo, na kama ilitokea madhara yeyote kwa mtu yeyote katika usafirishaji huo, atalipwa kutokana na madhara hayo aliyoyapata.[177] Kwa masharti ya kifungu hiki, mtoto aliyesafirishwa kwa njia hiyo ya haramu naye atapaswa kulipwa fidia.

---

[174] Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu Nam.6 ya Mwaka 2008, kifungu cha 4

[175] Ibid kif. 5

[176] Ibid kifungu cha 6

[177] Ibid kifungu cha 15

Aidha, Sheria katika kifungu cha 17 inaelezea kuwa maslahi ya mtoto au mtu mwenye ulemavu yatakuwa muhimu katika usaidizi wowote utakaotolewa ili kuokoa, kumrekebisha, kumshauri au kumuunganisha tena mtoto ambaye ni mwathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu. Vile vile, msaada au ulinzi wa mtoto na mtu mwenye ulemavu utaendelea kutolewa na Serikali kuanzia pale sababu za kuaminika zinapojitokeza kuwa mtoto au mtu mwenye ulemavu ni mwathirika wa biashara hiyo haramu ya usafirishaji wa binaadamu mpaka pale kutakapokuwa na uthibitisho wa kupona kamili kwa mtoto huyo.[178] Ikitokea mtoto ambaye ni mwathirika wa usafirishaji haramu wa binaadamu anatakiwa kurejeshwa nyumbani kwao nje ya Tanzania, atarejeshwa ikiwa mzazi au mlezi au jamaa ameridhia au Wakala wa Serikali au wakala wa kuwalinda watoto wa nchi hiyo wameridhia na watakuwa tayari kuchukua majukumu kuhusu mtoto huyo.[179]

### 3.4.10. Sheria ya Elimu Nam.6 ya mwaka 1982

Sheria ya Elimu ilitungwa kwa lengo la kuhakikisha maendeleo bora katika nyanja ya elimu Zanzibar. Kwa mujibu wa Sheria hii, uandikishaji wa lazima wa

[178] Ibid kifungu cha 19

[179] Ibid, kifungu cha 22

mtoto[180] ni kuanzia miaka 7 mpaka miaka 13. Pia, Sheria imeweka jukumu kwa wazazi na walezi wa watoto kuhakikisha wanahudhuria skuli baada ya kuandikishwa mpaka pale watoto hao watakapomaliza elimu ya Msingi.[181] Kifungu hicho cha Sheria kikaendelea kutoa maelezo kwamba elimu ya Msingi iliyokusudiwa kwenye kifungu cha 20 ni elimu ya Msingi na Sekondari ya chini ambayo kila mtoto wa Zanzibar anastahiki kupata. Vile vile, Sheria inaendelea kueleza kwamba mtoto anaesoma elimu ya lazima ya Msingi na Sekondari ya chini hataolewa na ikitokea ataolewa, basi anatakiwa kufukuzwa skuli.

Aidha, Sheria imetoa wajibu kwa mzazi kutoa taarifa kwa mtoto anayetimiza umri wa kwenda skuli.[182] Taarifa hizo ambazo zinakua katika mfumo wa maandishi, zinatakiwa kupelekwa kwa Afisa elimu Mkoa kipindi ambacho mwaka unaofuata mtoto huyo atatimiza umri wa kupata elimu ya lazima. Hivyo, masharti ya vifungu hivi yameweka mkazo katika elimu ya mtoto kama moja ya haki za msingi zinazoimarisha ustawi wa mtoto.

[180] Sheria ya Elimu, Nam.6 ya Mwaka 1982, kifungu cha 19

[181] Ibid kifungu cha 20

[182] Ibid kifungu cha 22

### 3.4.11. Sheria ya Mahakama ya Kadhi Nam. 9 ya mwaka 2017

Kifungu cha 5 cha Sheria hii, kinaipa Mahakama ya Kadhi mamlaka ya kusikiliza kesi juu ya masuala yote ya kimadai na kesi zote ambazo wadaawa ni Waislam kuhusiana na mambo mbali mbali yakiwemo masuala ya matunzo na malezi ya watoto, wasia na urithi. Hivyo, Sheria hii nayo inasimamia masuala ya mtoto kwa kuzingatia matunzo ya mtoto hasa pale kunapokuwa na mgogoro unaosababisha wazazi kuwa na mgogoro juu ya matunzo ya mtoto huyo.

### 3.4.12. Sheria ya Makosa ya Mtandao Nam. 14 ya mwaka 2015

Sheria hii imetungwa kwa lengo la kuweka masharti ya makosa ya jinai yanayohusiana na mifumo ya kompyuta na Teknolojia ya mawasiliano ya habari na kuainisha makosa na adhabu zake zinazohusiana na matumizi ya mfumo wa kompyuta na teknolojia ya habari na mawasiliano. Sheria hii inatumika Tanzania kwa ujumla (Tanzania Zanzibar na Tanzania Bara).[183]

Sheria katika kifungu cha 13 imeelezea juu ya kosa la kuweka picha au video za ngono (Ponografia) za watoto na adhabu yake. Sheria imeeleza kwamba mtu ambaye atachapisha picha au video za ngono ponografia ya watoto kupitia mfumo wa kompyuta au kusaidia upatikanaji au kuwezesha ufikiaji wa

---

[183] Sheria ya Makosa ya Mtandao Nam.14 ya Mwaka 2015, kifungu cha 2

ponografia kwa watoto kupitia mfumo wa kompyuta, atakuwa ametenda kosa na atakapotiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni 50 au mara tatu ya thamani ya faida iliyopatikana kinyume cha Sheria au kifungo kisichopungua miaka 7 au vyote kwa pamoja.

### 3.4.13. Sheria ya Ajira Nam.11 ya mwaka 2005

Sheria katika Sehemu ya Pili imetaja haki za msingi na ulinzi kwa waajiriwa wote ikiwemo katazo juu ya ajira za watoto. Watoto kwa mujibu wa Sheria hii hawatakiwi kufanya kazi za aina yoyote isipokua kazi za nyumbani. Kazi hizo za nyumbani pia hazitakiwi kuathiri haki ya mtoto ya kupata elimu na kupata mapumziko.[184]

Aidha, Sheria imepiga marufuku kuwafanyisha au kuwaajiri watoto katika ajira mbaya. Ajira mbaya kwa madhumuni ya Sheria hii inajumuisha utumwa au njia yoyote inayofanana na utumwa, kuwasafirisha watoto kwa njia haramu, kuwatumia watoto katika kufanya ukahaba, ponografia za watoto au kuwatumia watoto kufanya vitendo viovu kama kusafirisha madawa ya

[184] Sheria ya Ajira, Namb. 11 ya Mwaka 2005, kifungu cha 6

kulevya.[185] Pia Sheria imeweka adhabu kwa mtu ambaye atakwenda kinyume na kifungu hiki cha Sheria.

Aidha, Sheria imeruhusu ajira kwa watoto kwa masharti maalum ikiwa mtoto husika ameshamaliza kusoma elimu ya lazima.[186] Vile vile, kwa watoto na vijana ambao wapo katika mafunzo katika skuli za Serikali au skuli za ufundi au vituo vya mafunzo ya amali, wanaweza kuajiriwa.[187]

---

[185] Ibid, kifungu cha 7

[186] Ibid, kifungu cha 8

[187] Ibid, kifungu cha 9

# SURA YA NNE

## 4.0 MAONI YA WADAU

### 4.1. Utangulizi

Sura hii inaainisha maoni, ushauri na mapendekezo ya wadau mbali mbali yaliyotolewa wakati wa vikao vilivyoandaliwa kwa madhumuni ya kukusanya taarifa kuhusiana na utafiti wa Sheria hili ya Watoto. Msingi wa Tume kukusanya maoni kwa wadau unatokana na kifungu cha 10 cha Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar, Nam. 16 ya Mwaka 1986 kinachoitaka Tume kukusanya maoni ya wadau wengi kwa kadri inavyowezekana wakati wa ufanyaji tafiti au mapitio ya Sheria.

Kwa msingi huo, maoni ya wadau mbali mbali yalikusanywa kwa madhumuni ya kuimarisha usimamizi wa Sheria hiyo na  kubaini changamoto za kuzifanyia kazi ili Sheria hii iweze kutekelezwa kwa mazingira ya sasa na iendane na wakati kwa maslahi ya mtoto hapa nchini. Tume imeyagawa maoni hayo katika makundi mawili ambayo ni maoni ya kisheria na maoni ya kiutendaji.

## 4.2. Maoni ya Kisheria

Katika upande wa maoni ya kisheria, wadau walipendekeza mambo mbali mbali yawekwe kisheria. Sehemu hii inabainisha maeneo hayo yaliyopendekezwa na wadau kuzingatiwa kisheria, kama ifuatavyo:

### 1. Kuanzishwa kwa Taasisi ya Usimamizi wa Huduma za Watoto

Wadau wamependekeza kuanzishwa kwa taasisi maalum kisheria ambayo itakua na jukumu la usimamizi wa huduma za watoto na kulinda ustawi wao. Wadau walitaka taasisi hiyo iwekewe majukumu ya utekelezaji wa usimamizi, utoaji wa huduma na ulinzi wa watoto ili waweze kupata haki zao kwa mujibu wa Sheria. Wadau walipendekeza Sheria iweke sifa za maafisa ambao watakuwa na kazi ya kusimamia ustawi wa watoto.

### 2. Kuanzishwa Baraza la Taifa la Huduma la Watoto

Wadau wamependekeza Sheria iliyopo ifanyiwe marekebisho kwa kuongezwa kifungu cha kuanzishwa Baraza la Taifa la Huduma la watoto. Baraza hilo liundwe kwa kushirikisha taasisi za Serikali na binafsi ambazo zinashughulikia masuala ya usimamizi wa haki, maslahi na ustawi wa watoto kwa namna moja au nyengine.

Aidha, wadau hao walipendekeza Baraza litakaloundwa liwe na jukumu la kuratibu na kusimamia taasisi zinazosimamia haki, maslahi, ustawi wa watoto na mambo yote yanayohusiana na watoto katika ngazi ya kitaifa; pamoja na kuziweka pamoja na kuziunganisha taasisi katika masuala maalum yenye maslahi na mtoto

## 3. Kuweka makosa yote ya watoto katika mamlaka moja ya mahakama ya watoto.

Wadau wamependekeza kifungu cha 18 (b) cha Sheria ya Watoto kifanyiwe marekebisho na kuipa mamlaka mahakama ya watoto kusikiliza mashauri yote yanayohusu makosa yatakayofanywa na watoto isipokua kuua. Wadau wameonesha changamoto iwapo mkosaji ni mtoto ambaye amefanya makosa katika mtiririko mmoja ambayo Mahakama ya Watoto haiwezi kuyasikiliza baadhi ya makosa hayo. Hivyo mtoto huyu inabidi kesi yake isikilizwe katika mahakama mbili (Mahakama ya kawaida na Mahakama ya watoto). Wadau wameeleza kuwa mara nyingi mashahidi hushindwa kutoa ushahidi katika mahakama tofauti kwa shauri linalomuhusu mtoto mmoja.

## 4. Udhalilishaji wa watoto katika mitandao

Wadau wameelezea changamoto inayojitokeza katika masuala ya udhalilishaji uliopo katika kifungu kinachohusiana na udhalilishaji wa watoto . Kifungu hicho kwa sasa hakikujumuisha udhalilishaji unaoweza kufanyika kupitia mitandao ya kijamii kwa njia tofauti ikiwemo matumizi ya simu za mkononi au vifaa vyengine vya kielektroniki. Kifungu hicho hakijazingatia mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia na njia za sasa zinazotumika kudhalilisha watoto. Hivyo, wadau wamependekeza kifungu hicho kifanyiwe marekebisho kwa kuongezwa kipengele kitakachojumuisha ulinzi wa watoto kutokana na makosa ya udhalilishaji wa njia ya kimtandao.

## 5. Wajibu wa Jamii kumlinda mtoto dhidi ya ukiukwaji wa haki zake.

Wadau wamependekeza kufanyiwa marekebisho kifungu cha 20 cha Sheria kwa kuongeza wigo wa utoaji wa adhabu na uwajibishaji kwa wanajamii wote na sio kwa baadhi ya watu. Kifungu hicho kwa sasakimetoa adhabu na kuwawajibisha baadhi ya watu kutokana na majukumu yao katika usimamizi wa haki za watoto kulingana na mwenendo wa maadili na taaluma zao pindi watakaposhindwa kuripoti ukiukwaji wa haki za mtoto lakini kuna jukumu kubwa kwa jamii ambayo ina wajibu wa kusimamia haki hizo.

## 6. Wazazi kuwekewa majukumu ya kisheria kusimamia watoto.

Wadau wamependekeza Sheria iliyopo iweke kifungu maalum cha majukumu ya wazazi katika kuwasimamia watoto wao. Kifungu hicho kitasaidia kuwawajibisha wazazi ambao kwa sasa imebainika matatizo mengi ya watoto yanasababishwa na wazazi kutosimamia watoto wao. Wamependekeza kifungu kitakachowekwa kifafanue wajibu wa wazazi kufuatilia mwenendo wa mtoto katika makuzi yake ikiwemo maadili na mambo mengineyo yanayohusiana na usimamizi wa watoto.

Aidha, imependekezwa kipengele hicho kiwekewe adhabu kwa wazee, wazazi au walezi watakaoshindwa kuwasimamia watoto kuwajibishwa kisheria.

## 7. Upokeaji wa malalamiko

Wadau wamependekeza Sheria iliyopo iweke kifungu cha upokeaji wa malalamiko yanayohusu masuala ya watoto na kiainishe utaratibu wa kusimamia malalamiko na kuweza kuyasikiliza malalamiko hayo kwa ajili ya ustawi wa watoto. Wadau hao wameeleza kuwa utaratibu huo utasaidia kuwa na uratibu mzuri wa malalamiko na kuyafanyia kazi malalamiko hayo kwa kuzingatia mamlaka ya kisheria kushughulikia malalamiko hayo. Imependekezwa kifungu kibainishe utaratibu wa malalamiko kutoka kwa

watoto wenyewe na hatua za kuchukuliwa kufuatilia ukweli wa malalamiko hayo; na utaratibu kwa wazazi, walezi na jamii kwa ujumla.

**8. Uanzishwaji wa Vituo vya ushauri kwa watoto**

Wadau wamependekeza kuanzishwa vituo vya ushauri nasaha kwa watoto hasa walio na umri wa kuanzia miaka 15 hadi 18 ambapo imegundulika katika kipindi hiki, watoto wengi huanza kubadilika tabia zao kutokana na mabadiliko ya kimwili. Vituo hivyo imependekezwa visajiliwe ili kutambulika rasmi na viwe na watu wenye ujuzi na uzoefu wa masuala ya maendeleo na ustawi wa watoto.

**9. Kuwepo kwa kanuni**

Wadau wamependekeza Sheria ya Watoto iliyopo itungiwe Kanuni, miongozo na taratibu za kurahisisha utekelezaji wa Sheria hii, kama ilivyopendekezwa katika Sheria ya Watoto. Aidha kuwekwe Miongozo ya kutoa ufafanuzi wa maeneo ya misingi ya ulinzi wa haki za mtoto.

**10. Ulinzi wa Haki za Binaadamu kwa Watoto**

Wadau walipendekeza kuimarishwa ulinzi wa haki za binaadamu hasa kwa watoto wenye ulemavu na wenye mazingira magumu ya kimaisha. Aidha,

wadau wamependekeza Serikali kuanzisha programu mbalimbali na kuzisimamia kuhusu kuwalinda watoto ikiwemo kustawisha huduma za ustawi wa jamii, kutoa matunzo maalum ya watoto wanaoathirika na uvunjwaji wa haki zao ikiwemo watoto mayatima, watoto wanaotupwa baada ya kuzaliwa na kuwapatia usaidizi wanawake wenye watoto walio na hali ngumu ya kimaisha pamoja na kutoa msaada kwa watoto waliozaliwa nje ya ndoa.

Wadau pia wamependekeza kulindwa na kuheshimiwa haki za binadamu kwa kila mtoto bila ya ubaguzi wa aina yoyote, bila kujali rangi, jinsia, au ubaguzi wa aina nyengine yoyote.

## 11. Ulinzi Maalum wa Watoto

Wadau wamependekeza kuwekwa utaratibu maalum wa ulinzi wa watoto, kabla na baada ya mama zao kujifungua. Aidha, katika kipindi hicho, imependekezwa kina mama kuwekewa mazingira mazuri ya utunzaji wa watoto walio tumboni ili waweze kuzaliwa wakiwa salama na kupatiwa huduma na uangalizi wa karibu kutokana na hali zao kwa lengo la kujilinda na hatari zitakazopelekea kuathirika kwa mtoto alie tumboni. Imeelezwa kwamba kwa sasa ulinzi uliopo ni watoto baada ya kuzaliwa, ingawa kuna udhalilishaji mkubwa wa mama wajawazito, ambao unaathiri ustawi wa mtoto katika kuzaliwa kwake.

## 12. Ulinzi wa Watoto Njiti

Wadau wamependekeza kuwekwa utaratibu wa kisheria kwa wanawake waliojifungua watoto njiti ambao ni waajiriwa, ili likizo yao ya uzazi iwe ya muda mrefu zaidi kuliko muda uliopo sasa kisheria, hadi watoto wao wawe katika hali ya kuridhisha. Wadau wameeleza kuwa hatua hii itasaidia kuwalinda watoto hao ambao kwa sasa imeonekana kuna changamoto ya utunzaji na ulezi kwa watoto hao ambao wanahitaji muda zaidi wa utunzwaji wao wakati wa kuzaliwa na baada ya kuzaliwa ili wawe katika hali na viwango vinavyokubalika.

## 13. Kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Mtoto

Wadau wamependekeza kuanzishwa kisheria, Mfuko wa Maendeleo ya Mtoto ambao utawekewa misingi ya usimamizi na utaratibu wa upatikanaji wa fedha za Mfuko huo ili kuleta ustawi wa mtoto hapa nchini. Aidha imependekezwa kuwa Mfuko huu pia uainishe upatikanaji wa fedha, matumizi yake, pamoja na shughuli zake ikiwemo kuendeleza watoto wenye mazingira magumu, waliotelekezwa na wazee wao, wasio na makaazi ya kudumu, walioathirika na madawa ya kulevya, wanaonyanyaswa kijinsia na kisaikolojia na watoto wengineo wanaofanana na hao.

## 14. Wajibu wa lazima wa kutoa taarifa kwa mtoto alie na mazingira hatarishi

Wadau wapendekeza kuwepo na utaratibu wa kisheria wa lazima kwa kila mtu mwenye ujirani na mtoto mwenye mazingira hatarishi katika eneo hilo, au mtu yeyote ambaye anaamini kuwa mtoto aliyekutana nae ameathiriwa au kuna uwezekano wa kuathiriwa kwa mtoto huyo, kutoa ripoti kwa Sheha, Polisi au mamlaka zinazosimamia masuala ya watoto zitakazoainishwa kwa mujibu wa Sheria. Aidha, wadau wamependekeza kuwekwa adhabu kwa mtu yeyote aliyeshindwa kutekeleza wajibu huu wa kutoa taarifa.

Aidha, wadau wamependekeza kuwekwa kinga dhidi ya mtoa taarifa za mtoto aliye hatarini kwa kutowekwa wazi utambulisho wake na kinga nyenginezo. Ili utaratibu huu utekelezeke vyema, Sheria iitake mamlaka husika kufanya mikutano na masheha au jamii ili kupata changamoto za watoto katika maeneo yao.

### 4.3. Maoni ya kiutendaji

## 1. Usimamizi wa Utekelezwaji wa sheria iliyopo.

Wadau wamependekeza kutokana na changamoto kubwa ya tabia na kuharibika kwa watoto wengi ambao ndio Taifa la kesho, kuna haja ya

kusimamiwa ipasavyo Sheria hii kwa kutekeleza uanzishwaji wa vituo rasmi vya marekebisho ya tabia kwa watoto kama ilivyoainishwa katika Sheria. Aidha, wadau wamependekeza kuwekwa utaratibu wa kikanuni wa kuviendesha vituo hivyo kama ilivyokusudiwa.

## 2. Maslahi na Vitendea kazi kwa Maafisa Ustawi

Wadau wamependekeza kuongezwa maslahi na kupatiwa vitendea kazi vya ufuatiliaji kwa Maafisa Ustawi wanaofanya tathmini ya kesi za watoto na kuhakikisha tathmini wanazozifanya hazichukui muda mrefu na kuziwasilisha kunakohusika kwa hatua zinazoendelea, ili haki ya mtoto ipatikane kwa mujibu wa Sheria.

Aidha, wadau wameeleza kuwa suala la tathmini linahitaji ufuatiliaji wa karibu ambao unatumia gharama, hivyo wamependekeza kitengo cha ustawi wa jamii kinachohusika na ulinzi wa watoto kiekewe bajeti inayojitosheleza ili kifikie malengo, kuondoa changamoto zilizopo na kukidhi mahitaji yanayowakabili maafisa ustawi.

## 3. Utolewaji wa Elimu kwa Jamii

Wadau wamependekeza kutolewa kwa elimu ya kutosha kuhusu umuhimu wa kutunza watoto, kuishi kifamilia, utoaji wa huduma za watoto hata kama wazee au walezi wa watoto wametengana au kuachana. Wadau hao wemesisitiza juu

ya uimarishaji wa utoaji wa ushauri nasaha kwa wazee au walezi katika jamii na familia kwa ujumla. Aidha, wadau hao wamependekeza kutolewa elimu zaidi kwa watoto na walezi wao juu ya namna ya kujilinda dhidi ya vitendo vya ukatili dhidi ya watoto. Vile vile imependekezwa elimu hiyo ipelekwe hadi mahabusu na Magereza ili watoto wanaotoka hukowasaidiwe kubadilika.

**4. Mafunzo kwa Maafisa Ustawi**

Kwa kuzingatia ongezeko la masuala ya udhalilishaji na mambo mengine yanayowaathiri watoto hapa nchini kwa ujumla, wadau walipendekeza maafisa ustawi wapatiwe mafunzo ya mara kwa mara ili kujenga uwezo wao na kuwawezesha kufanya kazi zao ikiwemo kufanya tathmini na upelelezi wa makosa wanayofanya au kufanyiwa watoto na mienendo ya maisha ya watoto utakaozingatia uhalisia.

Miongoni mwa maeneo yaliyopendekezwa kutolewa mafunzo ya kina kwamaafisa ustawi ni pamoja na mafunzo juu ya miongozo na misingi ya ustawi wa jamii, maeneo yenye viashiria hatarishi (risk) na mafunzo yatakayopelekea kuthibitishwa kuwa maafisa ustawi wanaotambulika kitaaluma.

**5. Mwamko wa Usimamizi wa Watoto**

Wakati wa vikao vya wadau, ilielezwa kuwa kumekuwa na changamoto ya uelewa mdogo wa wanajamii kuhusu wajibu na majukumu ya jamii katika

kusimamia haki, ulinzi, matunzo, upatikanaji wa elimu kwa watoto, maslahi, fursa za watoto na umuhimu wa kuwasimamia watoto katika mienendo yao na shughuli wanazozifanya. Hivyo kutofahamika kwa majukumu ya jamii, wazazi na walezi kwa watoto waliopo katika jamii hizo kunapelekea kufanyika vitendo viovu kwa watoto, kujiingiza katika maadili yasiokubalika na jamii, watoto hao kuanza kutumia madawa ya kulevya na vitendo vyenginevyo vya hatari.

Kutokana na udhaifu huo, wadau wamependekeza kutolewa kwa elimu ya mara kwa mara kwa makundi mbali mbali ya kijamii ikiwemo viongozi wa Dini ili kulitilia mkazo suala la usimamizi wa watoto.

# SURA YA TANO

## 5.0 MIKATABA YA KIMATAIFA NA UZOEFU KATIKA NCHI NYENGINE

### 5.1 Utangulizi

Sura hii inazungumzia Mikataba ya Kimataifa na Kikanda pamoja na uzoefu wa nchi mbali mbali ambazo Tume imepitia kwa lengo la kuangalia uzoefu wa nchi hizo kuhusiana na taratibu za kisheria zilizowekwa juu ya ustawi wa watoto ikiwemo haki pamoja na ulinzi wa watoto.

### 5.2 MIKATABA YA KIMATAIFA

Utafiti huu umezingatia mikataba mbali mbali ya kimataifa na mikataba ya kikanda inayofafanua masuala ya ustawi wa watoto yakiwemo masuala ya haki za watoto, viwango vya kuzingatiwa na nchi wanachama katika ulinzi wa watoto na masuala mengine muhimu kwa ustawi wa watoto. Mikataba hiyo inafafanuliwa hapa chini kama ifuatavyo:

#### 5.1.1. Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu la Mwaka 1948.

Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu lilipitishwa mwaka 1948 na Umoja wa Mataifa kwa lengo la kuweka ulinzi wa haki za msingi za binadamu ambazo zilivunjwa kwa kiasi kikubwa wakati wa Vita Vikuu vya Pili vya Dunia. Azimio

hili linajumuisha aina zote za haki za binadamu yaani haki za Kiraia na Kisiasa pamoja na haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni.

Ibara ya 25 (2) ya Azimio hili inawataka nchi wanachama kutoa haki ya matunzo maalum na kuwapatia usaidizi wanawake wenye watoto pamoja na watoto. Aidha, Azimio hili limewataka nchi wanachama kuwapatia ulinzi sawa wa Kijamii, watoto wote waliozaliwa ndani au nje ya ndoa.[188]

### 5.1.2. Mkataba wa Haki za Mtoto wa Mwaka 1989

Mkataba huu wa Haki za Mtoto ulipitishwa na Umoja wa Mataifa mnamo mwaka 1989 na kuanza kutumika Septemba 1990. Mkataba huu ndio uliokubalika zaidi duniani katika mikataba ya haki za binadamu.[189] Mkataba huu una vifungu ambavyo vinaweka wazi haki za Kiraia, Kisiasa, Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni kwa watoto.[190] Mkataba huu unaainisha haki za binadamu zinazopaswa kuheshimiwa na kulindwa kwa kila mtoto aliye chini ya umri wa miaka 18.[191]

---

[188] Ibara ya 25(2) ya Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu linapatikana Universal Declaration of Human Rights | United Nations

[189] Council of Europe, Manual for Human Rights Education with Young People, *Convention on the Rights of the Child,* inapatikana Convention on the Rights of the Child - Manual for Human Rights Education with Young people (coe.int)

[190] Ibid

[191] Ibid

Aidha, Mkataba unazitaka nchi wanachama kuheshimu haki zilizoorodheshwa katika Mkataba bila ya ubaguzi wa aina yoyote, bila kujali rangi, jinsia, lugha, dini, maoni ya kisiasa, taifa, kabila au asili ya mtu, mali, ulemavu, kuzaliwa au hali nyenginezo.[192] Mkataba pia unamlinda mtoto kutokana na aina zote za unyanyasaji wa kimwili au kiakili ikiwa ni pamoja na unyanyasaji wa kijinsia, kutelekezwa au unyonyaji.[193] Vile vile, Mkataba huu unalinda haki za watoto wenye ulemavu.[194] Aidha, katika kuhakikisha ustawi wa watoto, Mkataba huu unazitaka nchi wanachama kuhakikisha huduma ya afya kwa akina mama kabla na baada ya kujifungua.[195]

### 5.1.3. Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa wa Mwaka 1966

Mktaba huu ni miongoni mwa Mikataba muhimu ya haki za binadamu ambayo inatoa ulinzi wa haki za Kiraia na Kisiasa.[196]Mkataba huu ulipitishwa na Umoja wa Mataifa mnamo mwaka 1966 na kuanza kutumika mwaka 1976. Kama ilivyo

---

[192] Ibid, Ibara ya 2

[193] Ibid, Ibara ya 19 (1)

[194] Ibid, Ibara ya 23

[195] Ibid, Ibara ya 24 (2) (d)

[196] Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa wa Mwaka 1966 unapatikana International Covenant on Civil and Political Rights | OHCHR

mikataba mengine ya haki za binadamu, Mkataba huu pia umegusa haki za watoto.

Katika Ibara ya 24, Mkataba umezitaka nchi wanachama kutoa ulinzi kwa kila mtoto bila ya ubaguzi wowote wa rangi, kabila, jinsia, dini, utaifa, mali au kuzaliwa kwake. Haki hii ya kutobaguliwa inatakiwa kupatikana kwa kila mtoto katika ngazi za familia, jamii na hata Taifa. Aidha, Mkataba unazitaka nchi wanachama kuwasajili watoto na kuwapatia majina mara baada ya kuzaliwa.[197] Vile vile, Mkataba umetoa haki kwa kila mtoto kuwa na utaifa wake.[198]

#### 5.1.4. Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni wa Mwaka 1966.

Mkataba huu ulipitishwa na Umoja wa Mataifa mnamo mwaka 1966 na kuanza kutumika tarehe 3 Januari, 1976.[199] Mkataba huu ulianzishwa kwa lengo la kuhakikisha nchi wanachama wanasimamia upatikanaji wa haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni kwa wananchi wao.

---

[197] Ibid, Ibara ya 24

[198] Ibid

[199] Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni wa Mwaka 1966 unapatikana UN General Assembly, *International Covenant on Economic, Social and Cultural Rights*, 16 December 1966, United Nations, Treaty Series, vol. 993, p. 3, Refworld | International Covenant on Economic, Social and Cultural Rights

Mkataba unazitaka nchi wanachama kuhakikisha ulinzi maalum unatolewa kwa akina mama katika kipindi kinachofaa kabla na baada ya kujifungua na katika kipindi hicho kina mama wanaofanya kazi wanapaswa kupatiwa likizo yenye malipo au kupatiwa likizo ambayo inaambatana na manufaa kutoka katika mfuko wa hifadhi ya jamii.[200] Bila ya shaka, masharti haya ya Mkataba huu yanalenga kumpa nafasi mama kumuhudumia vizuri mtoto ili apate ustawi mzuri.

Aidha, Mkataba huu unazitaka nchi wanachama kuwalinda watoto na vijana kutokana na ukandamizaji unaosababishwa na sababu za kiuchumi na kijamii katika nchi zao.[201] Mkataba unaelekeza kuwa sheria za nchi ziwalinde watoto kutokana na kazi hatari ambazo zitawadhuru kiafya na tabia zao au kupelekea kushindwa kukua vyema watoto hao.[202] Nchi wanachama zimetakiwa kuweka mipaka ya umri wa chini ambao watoto wanaweza kuanza kufanya kazi na ziweke adhabu kwa waajiri watakaokiuka mipaka hiyo.[203]

---

[200] Ibid, Ibara ya 10 (2)

[201] Ibid, Ibara ya 10 (3)

[202] Ibid

[203] Ibid

### 5.1.5. Mkataba wa Ajira Mbaya zaidi kwa Watoto, wa Shirika la Kazi Duniani (ILO) Nam. 182 wa Mwaka 1999.

Shirika la Kazi Duniani (ILO) limepitisha Mkataba wa ajira mbaya zaidi kwa Watoto Nam. 182 mnamo mwaka 1999 na kuanza kutumika mwaka 2000. Mkataba huu ulianzishwa kwa lengo la kutokomeza ajira mbaya zaidi na zisizofaa kwa watoto.[204]

Nchi zilizoridhia Mkataba huu zinatakiwa kuchukua hatua za dharura kuhakikisha zinakataza na kutokomeza aina zote za ajira mbaya kwa watoto katika nchi zao.[205] Vile vile, Mkataba huu umemtafsiri mtoto kuwa ni mtu mwenye umri wa chini ya miaka 18.[206]

Aidha, Mkataba huu umezitambua ajira mbaya zaidi kwa watoto ni kama ajira zote zenye aina ya utumwa, kusafirisha watoto kwa njia ya haramu, kazi za kulazimishwa au kuwaingiza na kuwatumia watoto katika migogoro ya kivita. Ajira nyengine mbaya ni kuwatumia au kuwaingiza watoto katika ukahaba, kutengeneza picha za ngono, vitendo viovu hususan usafirishaji haramu wa

---

[204] Mkataba wa Ajira Mbaya kwa Watoto wa ILO Nam. 182 wa Mwaka 1999 ambao unapatikana Convention C182 - Worst Forms of Child Labour C onvention, 1999 (No. 182) (ilo.org)

[205] Ibid, Ibara ya 1

[206] Ibid, Ibara ya 2

dawa za kulevya na kazi za hatari, kuwatumia watoto katika kazi ambazo zitawapatia madhara ya kiafya, kitabia (morals) au madhara ya usalama wao.[207]

### 5.1.6. Mkataba wa Umri wa Chini wa Shirika la Kazi Duniani (ILO) Nam. 138 wa Mwaka 1973.

Mkataba huu uliopitishwa na Shirika la Kazi Duniani (ILO) Nam. 138 wa Mwaka 1973 una lengo la kuhakikisha kuwa watoto hawaanzi kufanya kazi wakiwa wadogo sana. Hivyo, Mkataba huu unaweka umri ambao watoto wanaweza kuanza kufanya kazi na kuajiriwa kisheria.[208]

Aidha, Mkataba huu unazitaka nchi zilizouridhia, kukomesha ajira za watoto katika nchi zao na kuzitaka nchi hizo kuweka umri wa chini wa mtoto kuanza kazi au kuajiriwa.[209] Vile vile, nchi wanachama zimetakiwa kuanzisha Sera za Kitaifa za kutokomeza ajira za watoto pamoja na kueleza umri wa chini wa mtoto anayeweza kuajiriwa.[210] Kwa mujibu wa Mkataba huu, umri wa chini utakaowekwa na nchi wanachama, hautokuwa chini ya umri wa kumaliza

[207] Ibid, Ibara ya 3

[208] Mkataba wa Umri wa Chini wa Shirika la Kazi Duniani (ILO) Nam. 138 wa Mwaka 1973 unapatikana Convention C138 - Minimum Age Convention, 1973 (No. 138) (ilo.org)

[209] Ibid, Ibara ya 2

[210] Ibid, Ibara ya 1

masomo ya lazima na kwa vyovyote vile, hautokuwa chini ya umri wa miaka 15.[211]

## 5.2. MIKATABA YA KIKANDA

### 5.3.1. Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu wa Mwaka 1981

Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu ambao unajulikana kama Mkataba wa Banjul, ulipitishwa na Umoja wa Afrika mnamo Mwaka 1981 kwa lengo la kutoa ulinzi wa Kimataifa wa haki za Msingi za Binadamu na kukuza Misingi ya Uhuru kwa Binadamu Barani Afrika.[212]

Ibara ya 18 (3) ya Mkataba huu inazitaka nchi wanachama kuhakikisha zinaondoa ubaguzi dhidi ya wanawake pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa ulinzi wa haki za wanawake na watoto kama inavyotakiwa kwa mujibu wa Mikataba ya Kimataifa.

### 5.3.2. Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto wa Mwaka 1990.

[211] Ibid, Ibara ya 2(3)

[212] Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu wa Mwaka 1981 unapatikana 36390-treaty-0011 - african charter on human and peoples rights e.pdf (au.int)

Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto umeweka na kufafanua haki za msingi za mtoto barani Afrika. Mkataba huu ulipitishwa na Umoja wa Afrika mnamo mwaka 1990 na kuanza kutumika 1999.[213]

Mkataba unazitaka nchi wanachama kutambua haki, uhuru na wajibu ulioainishwa katika Mkataba pamoja na kuchukua hatua za lazima katika kuhakikisha Sheria za ndani za nchi wanachama zinasimamia haki, uhuru na wajibu uliotolewa katika Mkataba huu.[214] Ibara ya 2 ya Mkataba huu inamtambua mtoto kuwa ni mtu aliye chini ya umri wa miaka 18. Vile vile, Mkataba huu unazitaka nchi wanachama kuwapatia watoto haki na fursa zilizotolewa katika Mkataba huu bila ya ubaguzi wa aina yoyote.[215] Miongoni mwa haki zilizotolewa na Mkataba huu ni haki ya kuishi na kukua,[216] kuwa na jina na uraia,[217] uhuru wa kujieleza,[218] uhuru wa kutoa mawazo, kufikiri na

[213] Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto wa Mwaka 1990 unapatikana 36804-treaty-african_charter_on_rights_welfare_of_the_child.pdf (au.int)

[214] Ibid, Ibara ya 1

[215] Ibid, Ibara ya 3

[216] Ibid, Ibara ya 5

[217] Ibid, Ibara ya 6

[218] Ibid, Ibara ya 7

kuabudu,[219] haki ya ulinzi wa faragha,[220] haki ya elimu[221] na haki ya kuwa na afya pamoja na kupatiwa huduma za afya.[222]

Aidha, Mkataba umetoa haki maalum kwa watoto wenye ulemavu wa akili au kimwili kupatiwa haki maalum ya ulinzi wao kulingana na mahitaji yao pamoja na kuwahakikishia ulinzi wa utu wao na kuwawezesha kujitegemea na kuwapa fursa kushiriki katika masuala ya Kijamii.[223] Mkataba pia unamlinda mtoto dhidi ya mila na desturi za Kijamii na Kiutamaduni zenye madhara kama vile ndoa za utotoni ambapo nchi wanachama zinatakiwa kutunga Sheria ambazo zitaeleza kuwa umri unaofaa kuolewa ni kuanzia miaka 18.[224]

Aidha, katika kupiga vita masuala ya unyanyasaji wa kingono kwa watoto, Mkataba huu unamlinda mtoto dhidi ya unyanyasaji na udhalilishaji huo katika Ibara ya 27 ambapo mtoto hatakiwi kutumika katika kufanya ukahaba na

---

[219] Ibid, Ibara ya 9

[220] Ibid, Ibara ya 10

[221] Ibid, Ibara ya 11

[222] Ibid, Ibara ya 14

[223] Ibid, Ibara ya 13

[224] Ibid, Ibara ya 21

kuhusishwa na masuala ya ngono. Vile vile, Mkataba unamlinda mtoto dhidi ya masuala ya kuuzwa, kusafirishwa na kutekwa nyara.[225]

Sambamba na hayo, Mkataba unazitaka nchi wanachama kutunga Sheria maalum ambazo zitasimamia hatua za kiutawala, kijamii pamoja na kutoa elimu ya kumlinda mtoto kutokana na aina zote za mateso, unyama au udhalilishaji, unyanyasaji, kutelekezwa, unyanyasaji wa kijinsia wakati akiwa chini ya uangalizi wa mzazi, mlezi, skulini au chini ya mtu yeyote ambaye amepewa jukumu la kumtunza mtoto huyo.[226]

Aidha, Mkataba huu katika Sehemu ya Pili umeanzisha Kamati ya Haki na Ustawi wa Mtoto[227] ambayo imepewa majukumu mbali mbali yakiwemo jukumu la kulinda haki zilizoainishwa katika Mkataba na kufuatilia utekelezaji wa haki zilizoainishwa na kutafsiri vifungu vya Mkataba kwa ombi la nchi wanachama, Taasisi ya Umoja wa Afrika au mtu mwengine yeyote au taasisi inayotambuliwa na Jumuiya ya Umoja wa Afrika.[228]

---

[225] Ibid, Ibara ya 29

[226] Ibid, Ibara ya 16

[227] Ibid, Ibara ya 32

[228] Ibid, Ibara ya 42

### 5.3.3. Mkataba wa Baraza la Ulaya juu ya Ulinzi wa Watoto dhidi ya Unyanyasaji na Udhalilishaji wa Kijinsia wa Mwaka 2007

Baraza la Ulaya limepitisha Mkataba wa Ulinzi wa Watoto Dhidi ya Unyanyasaji na Udhalilishaji wa Kijinsia mwaka 2007 kwa lengo la kuwalinda watoto dhidi ya unyanyasaji na udhalilishaji wa kijinsia, kuandaa chombo cha ufuatiliaji pamoja na kutoa msaada kwa waathirika.[229]

Mkataba huu katika Sura ya Sita, umezitaka nchi wanachama kuweka Sheria madhubuti za jinai ambazo zitayafanya makosa ya udhalilishaji kijinsia na unyanyasaji kuwa ni miongoni mwa makosa ya jinai pamoja na kuweka adhabu kwa makosa hayo. Miongoni mwa makosa hayo ni kosa la udhalilishaji kijinsia, [230] makosa yanayohusu ukahaba kwa watoto, [231] makosa yanayohusiana na kutengeneza, kusambaza, na kumiliki picha na video za ngono za watoto.[232]

[229] Mkataba wa Ulinzi wa Watoto dhidi ya unyanyasaji na Udhalilishaji Kijinsia wa Mwaka 2007 (Convention on the Protection of Children against Sexual Exploitation and Sexual Abuse) unapatikana CETS 201 - Council of Europe Convention on the Protection of Children against Sexual Exploitation and Sexual Abuse (coe.int)

[230] Ibid, Ibara ya 18

[231] Ibid, Ibara ya 19

[232] Ibid, Ibara ya 20

Katika kuweka kinga dhidi ya unyanyasaji na udhalilishaji wa kijinsia kwa watoto, Mkataba huu umezitaka nchi wanachama kutunga Sheria ambazo zitalazimisha watendaji wote ambao wana ukaribu na watoto katika utendaji wa kazi zao kupata mafunzo na kuajiri wale ambao wana uelewa na ufahamu juu ya ulinzi wa haki za watoto. Watendaji wanaoguswa na Mkataba huu ni kama vile waajiriwa katika sekta ya elimu, afya, maendeleo ya jamii, mahkama, maeneo ya michezo, utamaduni na shughuli za burudani.[233] Aidha, nchi wanachama wanatakiwa kuhakikisha waajiriwa wote katika sehemu zinazohusiana na watoto hawajawahi kutiwa hatiani kwa vitendo vya unyanyasaji wa kingono au unyanyasaji wa kijinsia kwa watoto.[234]

## 5.4 UZOEFU KUTOKA NCHI NYENGINE

### 5.4.1 JAMHURI YA KENYA

#### 5.4.1.1 Sheria ya Mtoto Nam.29 ya Mwaka 2022.

Nchi ya Kenya imetunga Sheria ya Mtoto Nam. 29 ya mwaka 2022 kwa lengo la kuweka mfumo wa kisheria ambao utasimamia jukumu la Serikali juu ya ustawi

---

[233] Ibid, Ibara ya 5

[234] Ibid

wa watoto kwa mujibu wa Sheria za Kimataifa pamoja na mikataba ya Kimataifa ambayo imeridhiwa na Kenya.[235] Katika kuhakikisha haki za watoto na kuweka maslahi bora ya watoto nchini humo, Sheria hiyo imebainisha mambo muhimu yaliyomo katika Sheria hiyo kama ifuatavyo:

**(a) Usimamizi na ulinzi wa haki za watoto pamoja na maslahi bora ya watoto.**

Sehemu ya Pili ya Sheria hii imezitambua haki muhimu za watoto na kuitaka Serikali kuzisimamia haki zote za watoto zinazotolewa na Sheria. Aidha, Sheria imemuelekeza Waziri anayehusika na masuala ya watoto kuhakikisha maendeleo, mapitio na utekelezaji wa Sera, Sheria na Mipango ya kutekeleza majukumu ya Serikali katika kusimamia haki za watoto kisheria.[236]

Katika kusimamia haki za watoto, Sheria hii imezitaja haki maalum za watoto ambazo zinahitajika kulindwa kisheria. Miongoni mwa haki hizo ni haki ya kuishi na kukua, haki ya kuwa na jina na utaifa pamoja na kusajiliwa na iwapo mtoto atapatikana ndani ya Kenya akiwa na umri wa chini ya miaka 8 na hajui uraia wake, basi Sheria hii imetoa haki kwa mtoto huyo kusajiliwa kama

---

[235] Sheria ya Mtoto ya Kenya Nam.29 ya Mwaka 2022, kifungu cha 3 (b).

[236] Ibid, kifungu cha 5

Mkenya.[237] Vile vile, mtoto ana haki ya kutokubaguliwa, haki ya kupatiwa ulinzi na malezi kutoka kwa wazazi, haki ya afya, elimu na haki ya kupata fursa ya kucheza na kufurahi pamoja na haki ya kulindwa dhidi ya ajira za watoto.[238]

Vile vile, Sheria hii imetoa haki kwa watoto wenye ulemavu, kuthaminiwa, kupatiwa matibabu na kupatiwa elimu bila ya malipo. Katika kulisimamia hili, Serikali inatakiwa kuanzisha taasisi mbali mbali ikiwemo taasisi za elimu, vituo vya kulelea watoto na vituo vya afya kwa kadri inavyohitajika katika kufikia walemavu kupata haki zao zote za msingi.[239] Sheria hii pia imeweka haki ya faragha kwa watoto[240] na kinga dhidi ya udhalilishaji kwa watoto.[241]

### (b) Mfuko wa Ustawi wa Mtoto

Sheria hii imeipa uwezo Serikali ya Kaunti kuanzisha Mfuko wa Ustawi (welfare schemes) wa mtoto baada ya kushauriana na Baraza la Kaunti kwa lengo la kuwasaidia watoto hasa katika upatikanaji wa huduma za watoto na kuanzisha

---

[237] Ibid, kifungu cha 6,7,9,11,13,14,16 na 18

[238] Ibid

[239] Ibid, kifungu cha 20

[240] Ibid, kifungu cha 27

[241] Ibid, kifungu cha 22

programu mbali mbali za watoto ikiwa ni pamoja na programu za watoto wenye ulemavu.[242]

**(c) Mamlaka ya mahakama ya watoto.**

Kwa mujibu wa Sheria hii, Jaji Mkuu anaweza kuanzisha Mahakama ya watoto. Mahkama hiyo ya watoto itakuwa na uwezo wa kusikiliza kesi zote za watoto zikiwemo za madai na jinai isipokua kesi za mauaji ya kukusudia.[243]

Mahkama ya watoto inaweza kutembelea na kufanya tathmini ya hali ya mazingira katika maeneo yote au taasisi zote ambazo mtoto anawekwa na kutoa amri yoyote ambayo Mahkama itaona inafaa kwa maslahi ya watoto.[244]

**(d) Muundo wa Usimamizi wa huduma za watoto**

Sheria hii imeweka muundo au mfumo mzima katika usimamizi wa utoaji wa huduma za watoto nchini Kenya. Taasisi za usimamizi zilizoanzishwa chini ya Sheria hii ni:

**(i) Ofisi ya Huduma za Watoto**

[242] Ibid, kifungu cha 62

[243] Ibid, kifungu cha 90 na 91

[244] Ibid, kifungu cha 91 (8)

Ofisi hii itasimamiwa na Katibu wa huduma za watoto ambaye ataajiriwa kwa kutumia njia ya ushindani na kisha kuteuliwa na Tume ya Utumishi wa Umma.[245]

Katibu atakuwa msimamizi wa Ofisi hii na atakuwa na majukumu mbali mbali yakiwemo uanzishwaji, usimamiaji pamoja na utunzaji wa vituo vya kuwalinda watoto, skuli na mahabusu za watoto.[246] Vile vile, Katibu ana jukumu la kuchunguza, kufuatilia na kuripoti kesi zote za watoto wanaokabiliana na shida na matatizo mbali mbali.[247]

Aidha, kwa kutumia njia ya ushindani, Tume ya Utumishi wa Umma itaajiri na kuteua maafisa wakuu, maafisa wa watoto na maafisa wengine kama inavyohitajika, ili kumsaidia Katibu katika kutekeleza majukumu yake aliyopewa katika Sheria hii.[248]

### (ii) Baraza la Taifa la Huduma za Watoto

[245] Ibid, kifungu cha 37

[246] Ibid, kifungu cha 38

[247] Ibid

[248] Ibid, kifungu cha 40

Sheria imeanzisha Baraza la Taifa la Huduma za Watoto[249] ambalo limepewa majukumu mbali mbali yakiwemo jukumu la kumshauri Waziri anayehusika na masuala ya watoto juu ya masuala ya ulinzi wa watoto. Aidha, Baraza hilo limepewa majukumu ya kushirikiana na Idara husika za Serikali, uongozi wa majimbo na taasisi binafsi katika kufuatilia na kutathmini programu zilizoanzishwa nchini Kenya kwa lengo la kuangalia maslahi ya watoto pamoja na kuwezesha, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Sheria, Kanuni na Mikataba ya Kimataifa ambayo inasimamia maslahi ya watoto.[250]

Baraza hili lina wajumbe mbali mbali akiwemo Mwanasheria Mkuu au mwakilishi wake, Katibu Mkuu wa Wizara ambayo inasimamia masuala ya watoto, Katibu Mkuu wa Wizara inayosimamia masuala ya fedha, mwakilishi wa Gavana wa Serikali ya jimbo, watu binafsi watatu kutoka katika jamii akiwemo mwakilishi wa taasisi ya dini na katibu wa huduma za watoto.[251] Aidha, Mwenyekiti wa Baraza hili anateuliwa na Rais.[252]

### (iii) Kamati ya ushauri na kamati ndogo ndogo za Kaunti

---

[249] Ibid, kifungu cha 41

[250] Ibid, kifungu cha 42

[251] Ibid, kifungu cha 43

[252] Ibid,

Baraza linaweza kuanzisha Kamati za ushauri ili Baraza hilo liweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi katika ngazi ya Kaunti.[253] Aidha, Baraza linaweza kuanzisha Kamati ndogo ndogo za Kamati kuu ya ushauri ambazo kazi zake zitakuwa ni kushauri Kamati ya Ushauri juu ya utekelezaji wa mapendekezo ya mpango wa ustawi kama itakavyohitajika katika kuimarisha ulinzi wa haki za watoto katika maeneo yao.[254]

### (e) Vituo vya uokoaji watoto

Sheria hii imempa uwezo Waziri husika wa masuala ya watoto kwa kushauriana na Baraza la Taifa la Huduma za Watoto, kuanzisha vituo vya uokoaji watoto katika ngazi za chini, ambavyo vitawapatia kwa muda matunzo na ulinzi watoto ambao wanasubiria hatua nyengine za kuwasimamia kuchukuliwa kwa mujibu wa sheria.[255] Vituo hivyo vitaweka watoto kwa muda usiozidi miezi sita kabla ya hatua nyengine kuchukuliwa juu ya watoto hao. Vituo hivi hutumika iwapo tu hakuna mbadala wa sehemu nyengine au hatua nyengine ya kuchukuliwa kwa wakati huo.[256]

---

[253] Ibid, kifungu cha 54

[254] Ibid, kifungu cha 55

[255] Ibid, kifungu cha 63

[256] Ibid, kifungu cha 63 (7)

**(f) Vituo maalum vya Polisi kwa ajili ya watoto**

Sheria hii inamtaka Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini kenya, kutenga maeneo maalum (child security units) yenye usalama na mazingira yasiyo hatarishi kwa mtoto katika kila kituo cha Polisi kwa ajili ya kuwaweka watoto ambao wanakinzana na Sheria.[257] Vile vile, Sheria imempa uwezo Katibu wa huduma za watoto kufanya ukaguzi katika vituo hivyo vya watoto ndani ya Polisi na kuangalia iwapo vituo hivyo vimeweza kukidhi viwango vinavyotakiwa vya ulinzi wa haki za watoto vimetimia kama vinavyotakiwa kisheria.[258]

**(g) Mahabusu za watoto**

Sheria imempa uwezo waziri anayehusika na masuala ya watoto, kuanzisha mahabusu za watoto (remand homes) ambazo zitatoa huduma muhimu kama vile malazi, matunzo na ulinzi wa haki za watoto kwa watoto ambao wamekinzana na Sheria.[259] Aidha, Katibu anatakiwa kuzingatia na kuweka mazingira kwa watoto ambao wana mahitaji maalum. Lengo la kuanzishwa mahabusu ni kuwatunza na kuwalinda watoto waliokinzana na Sheria wakati

[257] Ibid, kifungu cha 64

[258] Ibid, kifungu cha 64

[259] Ibid, kifungu cha 77

wakisubiri hukumu za kesi zao au watoto wanaosubiri kupatiwa makazi mapya.[260]

**(h) Skuli za kurekebisha tabia**

Waziri anayehusika na masuala ya watoto anaweza kuanzisha skuli za kurekebisha tabia kwa watoto na akiona inafaa, anaweza kuwapatia watoto hao, huduma za marekebisho ya tabia, malazi, elimu, mafunzo na vifaa kwa ajili ya kuwatunza watoto hao.[261]

Aidha, Sheria imetoa fursa kwa watu binafsi kuanzisha skuli za kurekebishia tabia baada ya kupata ruhusa kutoka kwa Waziri anayehusika na masuala ya watoto.[262] Vile vile, Sheria hii imeweka utaratibu mzima wa kufuatwa katika kuziendesha skuli za kurekebisha tabia za watoto.[263]

**(i) Ulinzi dhidi ya ulimwengu wa kimtandao**

Sheria ya Mtoto inaeleza kwa uwazi hitaji na wajibu wa kuwalinda watoto dhidi ya madhara katika ulimwengu wa mtandao. Sheria inawalinda watoto

---

[260] Ibid

[261] Ibid, kifungu cha 78

[262] Ibid

[263] Ibid

dhidi ya aina yoyote ya unyanyasaji mtandaoni. Unyanyasaji huu wa mtandaoni unajumuisha uenezaji wa picha zozote chafu na unyanyasaji wa mtandaoni unaotokea kupitia mfumo wowote wa kielektroniki, mtandao, au teknolojia nyengine ya mawasiliano.[264]

[264] Ibid kif. 22(3),(4),(5) &(6)

### 5.4.2 MAURITIUS

#### 5.4.2.1 Sheria ya Watoto Nam.13 ya Mwaka 2020

Mauritius imepitisha Sheria ya Watoto Nam. 13 ya Mwaka 2020 kwa lengo la kutoa huduma bora zaidi za utunzaji, ulinzi na msaada kwa watoto nchini humo. Mambo muhimu yaliyomo katika Sheria hii ni kama yanavyofafanuliwa hapa chini:

#### (a) Baraza la kuratibu Huduma za watoto

Sheria hii imeanzisha Baraza la kuratibu huduma za watoto (Child Services Coordinating Panel) [265] ambalo lina kazi ya kuratibu shughuli zote zinazohusiana na utekelezaji wa Sheria hii, Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki ya Mtoto na Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto.[266]

Baraza hili lina majukumu mbali mbali katika kusimamia haki za watoto nchini Mauritius ikiwemo kuratibu huduma za umma zinazohusiana na watoto katika ngazi ya Wizara na kusimamia katika ngazi ya Kitaifa, utaratibu wowote wa masuala ya utawala kwa lengo la kusaidia Serikali katika shughuli

---

[265] Sheria ya Watoto ya Mauritius Nam.13 ya Mwaka 2020, kifungu cha 8 (1)

[266] Ibid

zinazohusiana na  watoto.[267] Vile vile, Baraza hili linashirikiana na wadau wa masuala ya watoto kuimarisha utoaji wa ulinzi bora kwa watoto; na kutoa mapendekezo kwa Wizara yoyote au Shirika lolote linalojihusisha na watoto.[268]

Aidha, Baraza limepewa uwezo wa kuanzisha kamati ndogo ili kuweza kusaidia kutekeleza majukumu ya Baraza kwa ufanisi.[269]

### (b) Muundo  wa Baraza la Kuratibu Huduma kwa Watoto

Baraza la Kuratibu Huduma za Watoto linaundwa na afisa msimamizi ambaye atakuwa Mwenyekiti; mwakilishi wa Wizara inayoshughulikia ustawi wa mtoto; mwakilishi wa Wizara ya elimu; mwakilishi wa Wizara ya fedha; mwakilishi wa Wizara ya afya; na mwakilishi wa Wizara yenye dhamana ya kufanya mageuzi katika taasisi.  Wajumbe wengine wa Baraza hili ni mwakilishi wa Wizara yenye dhamana ya Hifadhi kijamii; mwakilishi wa Wizara yenye dhamana ya vijana; mwakilishi wa Kamishna wa Polisi mwenye cheo si chini ya

[267] Ibid kifungu cha 8 (2)

[268] Ibid

[269] Ibid

cheo cha Mrakibu wa Polisi; na Wajumbe wengine wawili (2) ambao watateuliwa na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya watoto.[270]

**(c) Utekelezaji wa mapendekezo ya Baraza la Huduma za Watoto:**

Sheria imetaka mapendekezo yanayotolewa na Baraza la Huduma za Watoto kwa Wizara yoyote au Asasi yoyote ya kiraia inayojihusisha na masuala ya watoto, kufanyiwa kazi kwa muda uliotolewa na Baraza na kuwasilisha ripoti ya utekelezaji wa mapendekezo hayo kwenye Baraza.[271] Iwapo Asasi au Wizara imeshindwa kuyafanyia kazi mapendekezo yaliyotolewa na Baraza ndani ya muda waliopewa, inatakiwa taasisi hiyo iwasilishe sababu za kushindwa kutekeleza mapendekezo waliyopewa na Baraza.[272]

**(d) Makosa dhidi ya watoto**

Sehemu ya Tatu ya Sheria hii imeorodhesha na kufafanua makosa ambayo anaweza kufanyiwa mtoto pamoja na adhabu zake.[273] Baadhi ya makosa hayo ni ubaguzi dhidi ya watoto ukiwemo ubaguzi wa rangi, tabaka, mahali

---

[270] Ibid

[271] Ibid, kifungu cha 8 (3)

[272] Ibid

[273] Ibid,kifungu cha 11

anapotoka, kisiasa, imani ya dini, lugha au ulemavu. Adhabu ya kosa hili ni kulipa faini isiyozidi rupianLaki Mbali (200,000) na kifungo kisichozidi miaka mitano 5.[274]

Aidha, kosa jengine ni kufunga ndoa ya kiserikali au kidini na mtoto au kuishi pamoja na mtoto kama wanandoa ambapo adhabu ya kosa hili ni faini isiyozidi rupia Milioni moja (1,000,000) na kifungo kisichozidi miaka 10.[275] Makosa mengine yaliyoainishwa katika Sheria hii ni kutumia adhabu ya viboko au yenye kudhalilisha kwa watoto,[276] kutelekezwa kwa mtoto,[277] kumteka nyara mtoto,[278] na kumuondoa mtoto kutoka kwenye sehemu ya usalama.[279] Aidha, Sheria hiyo imebainisha makosa mengine dhidi ya watoto ikiwemo kusababisha, kuchochea au kuruhusu mtoto chini ya miaka 16 kufanya ngono au kudhalilishwa kingono kwa njia yoyote ikiwemo ya kufanya au kuangalia

---

[274] Ibid

[275] Ibid, kifungu cha 12

[276] Ibid, kifungu cha 14

[277] Ibid, kifungu cha 15

[278] Ibid, kifungu cha 17

[279] Ibid, kifungu cha 18

picha chafu (ponography),[280] kufanya ukahaba kwa watoto na kumuweka mtoto katika madanguro.[281]

### (e) Wajibu wa lazima wa kutoa taarifa kwa mtoto aliye hatarini

Sheria hii imeweka wajibu wa lazima kwa kila mtu ambaye anafanya kazi za kitaalamu au kazi rasmi ambazo zinamuhusisha mtoto katika utendaji wa kazi zake au mtu yeyote ambaye anaamini kuwa mtoto aliyekutana nae ameathiriwa au kuna uwezekano wa kuathiriwa kwa mtoto huyo, kuripoti suala hilo kwa mkuu wake wa kazi au kwa polisi.[282] Aidha, Sheria hii imeweka adhabu kwa mtu yeyote aliyeshindwa kutekeleza wajibu huu wa kutoa taarifa na akitiwa hatiani, atalazimika kulipa faini isiyozidi rupia 200,000 na atatumikia adhabu ya kifungo kisichozidi miaka mitano (5).[283]

Aidha, Sheria hii imeweka kinga dhidi ya mtoa taarifa za mtoto aliye hatarini kwa kutokushtakiwa kwa mashtaka ya jinai au madai hata kama taarifa hizo

---

[280] Ibid, kifungu cha 19 na 21

[281] Ibid, kifungu cha 20

[282] Ibid, kifungu cha 34

[283] Ibid,

zinamhusisha mtu mwengine au shahidi isipokuwa iwapo taarifa hizo ziwe zimetolewa kwa nia mbaya.[284]

### (f) Mpango wa Ushauri kwa Mtoto

Sheria imeanzisha Mpango wa Ushauri wa Watoto[285] wenye lengo la kusaidia watoto wenye umri kati ya miaka 8 mpaka miaka 16 ambao ni waathirika wa kutelekezwa, wanaokabiliwa na matatizo ya tabia, wako katika dhiki au walio kwenye matatizo ya kushindwa kwenda sambamba na hali ya jamii inayowazunguka.[286] Mpango huu unasimamiwa na Afisa msimamizi kwa kushirikiana na Kamati ya Ushauri ya Mtoto.[287]

### (g) Kamati ya Ushauri kwa Mtoto

Sheria hii imeanzisha Kamati ya Ushauri ya Mtoto ambao wajumbe wake ni Afisa Msimamizi wa Mpango wa Ushauri wa Mtoto, Mwakilishi wa Wizara, Mwakilishi kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mwakilishi wa Kamishna wa Polisi na Mwakilishi kutoka Wizara ya Elimu. Wajumbe wengine

[284] Ibid, kifungu cha 35 (3)

[285] Ibid, kifungu cha 43(1)

[286] Ibid, kifungu cha 43(2)

[287] Ibid, kifungu cha 43 (3)

wa Kamati hiyo ni Mwanasaikolojia atakayeteuliwa na Afisa Msimamizi wa Mpango wa Ushauri kwa mtoto, wawakilishi watatu kutoka katika Asasi za kiraia zinazojishughulisha na masuala ya afya ya uzazi, dawa za kulevya na wanaojishughulisha na masuala ya watoto ambao watateuliwa na Waziri.[288] Jukumu kubwa la Kamati hii ni kumsaidia Afisa Msimamizi katika kusimamia na kutekeleza Mpango wa Ushauri wa Mtoto.[289]

### (h) Kuhudhuria mzazi Mahkamani

Pia Sheria hii inamtaka mzazi ahudhurie mahakamani itakapotokea mtoto wake amefanya kosa na kupelekwa mahakamani.[290] Kwa madhumuni ya kutekeleza mahudhurio ya mzazi na kumwezesha kushiriki katika shauri na kuwezesha amri kutolewa dhidi yake, Mahakama inaweza kutoa wito kwa mzazi kumtaka afike mbele ya Mahakama kwa wakati na mahali palipotajwa, na pale mzazi anaposhindwa kufika kwa kutii wito, Mahkama inaweza kutoa hati ya kukamatwa kwake.[291]

---

[288] Ibid, kifungu cha 44

[289] Ibid

[290] Ibid, kifungu cha 59

[291] Ibid

**(i) Mtoto ambaye hakusajiliwa kuwa Raia**

Sheria hii imekataza mtoto kunyimwa fursa yoyote au huduma yoyote inayotolewa na umma kutokana na kuwa mtoto huyo hajasajiliwa kuzaliwa kwake chini ya Sheria ya Uraia.[292] Msajili wa Raia anaweza kutoa hati ya Kiraia kwa mtoto yeyote ambaye hakusajiliwa kwa lengo la kupata huduma za umma kama Waziri atakavyoidhinisha.[293]

### 5.4.3 NEPAL

#### 5.4.3.1 Sheria inayohusiana na Watoto Nam.23 ya Mwaka 2018.

Katika usimamizi wa masuala ya watoto, nchi ya Nepal imepitisha Sheria inayohusiana na Watoto Nam. 23 ya Mwaka 2018, kwa lengo la kudumisha maslahi bora ya watoto, kwa kuheshimu, kulinda, kukuza na kutimiza haki za mtoto. Mambo muhimu yaliyomo kwenye Sheria hii ni kama yanavyofafanuliwa hapa chini:

**(a) Wajibu wa taasisi kwa Watoto.**

---

[292] Ibid,kifungu cha 67

[293] Ibid

Sehemu ya Tatu ya Sheria imeeleza kuhusu wajibu wa taasisi mbali mbali kwa watoto. Wajibu huo umewekwa kwa kuzingatia maslahi bora ya mtoto kwa kuzitaka taasisi na maafisa wote wanaojishuhulisha na watoto kutumia njia za kirafiki zenye lengo la kuwasaidia watoto; wajibu wa familia au mlezi ambapo wazazi wote au walezi wana wajibu wa kumlinda na kumtunza mtoto kwa kumpatia huduma zote za msingi. Aidha, sehemu hii imeweka jukumu la nchi kwa watoto ambalo litaweka mipango itakayoweza kuwapatia huduma muhimu watoto ikiwemo elimu, afya na ulinzi kwa watoto wanaohitaji ulinzi maalum; Wajibu wa sekta ya habari, jukumu la vyombo vya habari ambalo ni kuchapisha na kusambaza habari, bila kukiuka haki za mtoto na kusababisha athari mbaya kwa maslahi ya mtoto.

### (b) Uanzishaji wa chumba au sehemu ya uchunguzi

Sheria hii imeanzisha chumba au eneo la uchunguzi (observation chamber) kwa lengo la kumuweka mtoto chini ya udhibiti katika kipindi ambacho shtaka lake linaendelea kwa kipindi chote cha uchunguzi.[294] Mtoto aliye chini ya udhibiti kwa uchunguzi atapewa ushauri nasaha na mwanasaikolojia wa watoto pamoja na usaidizi katika masuala ya kisaikolojia ya kijamii kama

[294] Sheria inayohusiana na Watoto ya Nepal Nam. 23 ya Mwaka 2018, kifungu cha 22.

itakavyohitajika.[295] Aidha, Sheria hii imetoa ruhusa (kwa kuzingatia masharti yatakayowekwa) kwa mtu yeyote wa familia ya mtoto anayetaka kukaa pamoja na mtoto ambaye amewekwa katika chumba cha uchunguzi kwa ajili ya kumsaidia mtoto huyo.[296]

**(c) Haki za mtoto aliyeathirika**

Sheria hii imempa haki mbali mbali mtoto aliyeathirika ikiwemo mtoto huyo kupatiwa haki yake katika mazingira rafiki wakati wa hatua za kiuchunguzi, uendeshaji wa kesi pamoja na taratibu za kimahkama kama vile kupata taarifa za lugha anayoielewa na kupata fidia inayostahiki kutoka kwa mshtakiwa.[297] Kupatiwa fidia kutoka kwa mshtakiwa hakutomzuia muathirika kukosa fursa ya kulipwa fidia anayostahiki kutoka Serikalini kama itahitajika kufanya hivyo.[298]

**(d) Viwango vya ulinzi wa watoto**

[295] Ibid

[296] Ibid

[297] Ibid, kifungu cha 25

[298] Ibid

Sheria hii imezitaka taasisi zote zinazojishughulisha na masuala ya watoto kama vile skuli, taasisi za umma, sekta binafsi, na asasi zote za kiraia ambazo zinafanya kazi moja kwa moja na watoto, kuzingatia viwango vya ulinzi wa mtoto katika ngazi ya taasisi ili kuzuia ukatili dhidi ya watoto. Aidha, Sheria imebainisha wajibu wa taasisi hizo za watoto kuzingatia ulinzi dhidi ya unyanyasaji wa kijinsia kwa watoto; kuhakikisha juu ya ulinzi wa watoto na kuchukua hatua mara moja pale ambapo yatawasilishwa malalamiko kuhusu watoto.[299] Aidha, Sheria hii imempa jukumu mwalimu mkuu wa skuli, kiongozi wa taasisi ya umma, mkuu wa sekta binafsi na mashirika ya kijamii kusimamia utekelezaji wa viwango vya ulinzi wa watoto vilivyowekwa katika Sheria hii.[300]

### (e) Baraza la Taifa la Haki za Mtoto:

Sheria hii imeanzisha Baraza la Taifa la Haki za Mtoto ambalo linasimamiwa na Serikali ya Nepal, kupitia Waziri anayesimamia masuala ya wanawake. Watoto na wazee kwa lengo la kulinda na kuendeleza haki na maslahi ya mtoto.[301]

### (f) Kamati ya Haki za Mtoto kwa ngazi ya Mkoa na Mtaa:

[299] Ibid, kifungu cha 57

[300] Ibid

[301] Ibid, kifungu cha 59

Sheria hii imeanzisha Kamati ya Haki za Mtoto kwa ngazi ya Mikoa na Mitaa.[302] Kwa upande wa Mikoa, Kamati hizi zitakuwepo katika kila Mkoa na zitasimamiwa na Mwenyekiti wake ambaye ni Waziri anayesimamia masuala ya watoto katika Mkoa huo.[303] Kamati za Mtaa zitakuwepo katika kila Mtaa na zitasimamiwa na mjumbe wa Manispaa ya Vijijini.[304]

### (g) Mfuko wa Mtoto

Sheria hii imeanzisha Mfuko wa Mtoto kwa ajili ya kusaidia uokoaji wa haraka unapohitajika, kumpatia unafuu mtoto, kulipia gharama za kumrejesha mtoto katika hali ya kawaida baada ya kuathiriwa na unyanyasaji au madhara mengine pamoja na kutumika kumlipa fidia mtoto.[305]

Aidha, Sheria hii imeeleza vyanzo vya fedha vya Mfuko wa Mtoto ambavyo ni Fedha kutoka Serikali Kuu, Serikali za Mkoa na ngazi za Mtaa; fedha zitakazotoka Serikali za Kigeni, Mashirika ya Kimataifa au watu binafsi, fedha

---

[302] Ibid, kifungu cha 60

[303] Ibid

[304] Ibid

[305] Ibid, kifungu cha 63

kutoka kwa wazawa, mashirika ya ndani, fedha zilizopatikana kutoka Mahkama ya watoto, na fedha kutoka chanzo chengine chochote.[306]

**(h) Utekelezaji wa Haki za Mtoto**

Sheria hii imeweka utaratibu wa kuhakikisha upatikanaji wa haki za mtoto na utekelezaji wa wajibu wa mtu kwa mtoto, Aidha, Sheria hii imempa uwezo mtoto au mdau husika kuwasilisha ombi moja kwa moja katika Mahkama Kuu inayohusika ili kuhakikisha haki za mtoto zilizotajwa zinatekelezwa.[307]

**(i) Kufukuzwa kazi, kutokufaa kuteuliwa na kutokuwa na mawasiliano ya karibu na Watoto**

Sheria hii imeweka adhabu ya kumuondolea stahiki mtu aliyetenda kosa lolote dhidi ya mtoto. Sheria hii inataka mtu huyu afukuzwe kazi kwa hatua ya awali iwapo anafanya kazi katika taasisi yoyote ya umma au binafsi.[308] Aidha, kulingana na ukubwa wa kosa alilofanya mtu huyo, anaweza kukatazwa au kuzuiliwa kwa kipindi cha miaka 10 kufanya jambo lolote linalohusiana na

[306] Ibid

[307] Ibid, kifungu cha 65

[308] Ibid, kifungu cha 67

mawasiliano ya moja kwa moja na mtoto, pia hatochaguliwa, hatoteuliwa au kupewa nafasi yoyote katika taasisi na mashirika binafsi.[309]

**(j) Wajibu wa kutoa taarifa**

Sheria hii imeweka ulazima kwa mzazi, mlezi au mtendaji yeyote ambaye kazi zake zinahusiana na mtoto moja kwa moja kama vile mwalimu, wataalamu wa afya, wahudumu au mtu yeyote mwengine ambaye atajua kuwa kuna mtu anafanya au anatarajia kufanya vitendo vya ukatili, unyanyasaji au udhalilishaji wa kijinsi kwa mtoto kutoa taarifa Polisi haraka.[310] Aidha, Polisi baada ya kupokea taarifa hizo wataziwasilisha Ustawi wa Jamii kwa ajili ya kupata ushirikiano kutoka huko.[311]

Vile vile, Sheria hii imemlinda dhidi ya kushtakiwa kwa kutoa taarifa, mtoa taarifa yeyote ambaye ametoa taarifa hizo kwa lengo la kumlinda mtoto.[312]

### 5.4.4 LESOTHO

#### 5.4.4.1 Sheria ya Ulinzi na Ustawi wa Watoto Nam.7 ya Mwaka 2011

---

[309] Ibid

[310] Ibid, kifungu cha 68

[311] Ibid

[312] Ibid

Sheria ya Ulinzi na Ustawi wa Watoto imetungwa kwa lengo la kusimamia, kuendeleza haki za mtoto na kutekeleza matakwa ya mikataba ya kimataifa inayotoa haki na ulinzi na usalama wa mtoto.[313] Maeneo mbali mbali ambayo yanafafanuliwa katika Sheria hii kama ifuatavyo:

**(a) Mamlaka ya mahakama ya mtoto**

Kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto ya nchini Lesotho, kila Mahakama ya Chini ni Mahakama ya Mtoto katika eneo lake na itakuwa na mamlaka ya kusikiliza na kuamua kesi za watoto wanaohitaji matunzo, ulinzi, kurekebishwa kitabia na waliofanya makosa yote yaliyotajwa katika Jedwali la I na la II la Sheria hii.

Kifungu cha 134 (1) kimeendelea kueleza kuwa Mahakama ya Mtoto haina mamlaka ya kusikiliza kesi ya mtoto aliyeshitakiwa kwa kosa la mauaji, uhaini au uasi pamoja na makosa ambayo adhabu yake inazidi mamlaka ya mahakama ya mtoto au ikiwa mtoto ameshtakiwa kwa makosa mengi kwa pamoja yakiwemo yanayohusiana na mahakama nyengine.

**(b) Wajibu wa kutoa taarifa**

Sheria imeweka majukumu kwa Afisa anayehusika na kutoa matibabu, wanafamilia, mtu mwenye kuwahudumia watoto na jamii, kutoa taarifa kwa

---

[313] Sheria ya Ulinzi na Ustawi wa Watoto ya Lesotho Nam. 7 Ya Mwaka 2011, kifungu cha 2

Afisa Polisi au mfanyakazi wa jamii ikitokea mtoto amefanyiwa vitendo vibaya, kutelekezwa, au kunyanyaswa kingono. Mbali na majukumu hayo, Sheria hii pia imeweka adhabu (kifungo, faini au vyote kwa pamoja na kutoa huduma kwa jamii) kwa wote ambao wamepewa wajibu huo pindi wakishindwa kuutekeleza wajibu wao.

**(c) Kuhudhuria Mahakamani kwa mzazi au mlezi**

Sheria katika kifungu cha 136 inamtaka mzazi au mlezi aliyeonywa kuhudhuria katika shauri linalomuhusu mtoto wake mahali na wakati ambao amejulishwa. Sheria pia imetoa adhabu kwa mzazi au mlezi ambaye ameonywa kuhudhuria katika shauri linalomhusu mtoto wake akishindwa kutimiza jukumu lake hilo, akitiwa hatiani, atalazimika kulipa faini au kifungo kisichozidi mwezi mmoja.

**(d) Watoto walio katika hatari ya kufanya makosa**

Sheria imeweka fursa ya mzazi au mlezi wa mtoto kumlinda mtoto wake kutokana na kufanya makosa. Kifungu cha 173 cha Sheria hiyo kinaeleza kwamba mzazi au mlezi anaweza kupeleka katika mahakama ya mtoto, maombi ya kuzuiliwa kwa mtoto katika skuli za marekebisho au hosteli za majaribio ikiwa ataona hawezi kumdhibiti vizuri mtoto wake. Hivyo mahakama baada ya kuangalia mambo mbalimbali ambayo yametajwa kwenye Sheria hii,

itaamrisha kuwekwa mtoto huyo chini ya udhibiti wa skuli za marekebisho au vyenginevyo.

**(e) Wajibu na majukumu ya Serikali**

Sheria hii imeipa Serikali wajibu wa kutengeneza sera ambazo zitahakikisha zinasimamia ulinzi wa watoto na kuondoa aina zote za ubaguzi dhidi ya watoto; zitasaidia ulezi wa watoto pale ambapo wazee au walezi watashindwa kumlea mtoto wao; zitaleta muamko juu ya haki za watoto wenye ulemavu, mahitaji yao na mchango wao katika jamii n.k.[314]

**(f) Wajibu wa jamii kutoa taarifa**

Sheria hii imeipa jamii wajibu wa kutoa taarifa iwapo mwanajamii ataona haki za mtoto zinavunjwa au hazitekelezwi, na hivyo, mwanajamii anatakiwa atoe taarifa kwa kiongozi wa kijadi (chief), polisi au Idara ya Ustawi wa Jamii.[315]Aidha, Sheria hii imeweka adhabu kwa mwanajamii kutumikia jamii (community service) iwapo atashindwa kutekeleza wajibu wake huo.[316]

**(g) Makosa wanayotendewa watoto**

---

[314] Sheria ya Ulinzi na Ustawi wa Watoto ya Lesotho Nam. 7 Ya Mwaka 2011, kifungu cha 22

[315] Ibid, kifungu cha 36

[316] Ibid

Sehemu ya Sita ya Sheria hii imeyatambua makosa mbali mbali ambayo anaweza kufanyiwa mtoto sambamba na adhabu zake. Makosa hayo ni kama makosa yote yanayohusiana na afya na ustawi wa jamii wa mtoto kama vile kosa la kumsababishia mtoto kudhalilishwa, kumyanyasa, kumuacha mtoto bila ya uangalizi na huduma na kumfanya mtoto kuwa omba omba. Aidha, baadhi ya makosa yametambulika katika Sehemu ya Tisa ya Sheria hii ambayo ni makosa ya kuwateka nyara watoto na kusafirisha watoto kwa njia za haramu (trafficking).

# SURA YA SITA

## 5.0 MATOKEO YA UTAFITI

### 6.1. Utangulizi

Sura hii inaelezea matokeo yaliyopatikana katika utafiti huu unaojielekeza katika kuangalia utekelezaji wa malengo ya kuanzishwa Sheria ya Watoto na mikataba ya kimataifa ya watoto katika kufikia ustawi wa watoto nchini. Matokeo haya yamejumuisha maeneo muhimu yaliyobainika katika maoni ya wadau, sera na sheria mbalimbali za ndani ya Zanzibar zinazohusiana na usimamizi wa watoto katika uwajibikaji wa kuwalinda, haki na maslahi ya watoto, pamoja na uzoefu wa sheria zinazohusiana na watoto za nchi mbali mbali pamoja na mambo muhimu yaliobainika katika miongozo mbali mbali ya kimataifa.

### 6.2. Makundi ya Wadau (Sampuli ya utafiti) na Uchambuzi wa Takwimu

Kufikia malengo ya utafiti huu, makundi mbali mbali yalihusishwa. Makundi hayo yalijumuisha Taasisi za Serikali, Taasisi binafsi zinazohusiana na masuala ya watoto, asasi za kiraia zinazoshughulikia masuala ya watoto, na wadau wengine wa masuala ya watoto. Wadau hao ni kama wafuatao:

1. (OR), Katiba, Sheria Utumishi na Utawala Bora,
2. Mahakimu hasa wanaohusika na Kesi za Watoto,
3. Mawakili wa Serikali na Binafsi,
4. Jumuiya ya Wajane Zanzibar,
5. Jumuiya ya Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA),
6. Wasaidizi wa Sheria,
7. Jumuiya ya Maimamu Zanzibar (JUMAZA),
8. Chama cha Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA),
9. Asasi ya Utoaji wa Elimu ya Sheria (UPAU),
10. Kituo cha Huduma za Kisheria Zanzibar (ZLSC),
11. Jumuiya ya Watu Wenye Ulemavu Zanzibar,
12. Jumuiya ya Mawakili,
13. Mimi na Wewe Foundation,
14. Mabaraza ya Watoto Zanzibar,
15. Jeshi la Polisi,
16. Makadhi wa Wilaya,
17. Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar,
18. Wanafunzi wa Skuli za Sekondari na Msingi,
19. Vituo vya Kulelea Mayatima,
20. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto,

21. Walimu wa Madrasa na Skuli,
22. Wizara ya Habari, Vijana Utamaduni na Michezo,
23. Ofisi ya Rais, Kazi na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi,
24. Waandishi wa Habari,
25. Chuo cha Mafunzo,
26. Dawati la Kijinsia,
27. Maafisa Ustawi wa Jamii,
28. Masheha wa Shehia,
29. Wapelelezi wa Makosa ya Jinai (hasa makosa ya Udhalilishaji),
30. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali,
31. Wakala wa Serikali Mtandao,
32. Kituo cha Kurekebisha Tabia za Watoto,
33. Baraza la Vijana,
34. Wanajamii, na
35. Madaktari.

Vikao vya wadau vilifanyika katika maeneo tofauti ya Unguja na Pemba. Jumla ya wadau waliohudhuria katika vikao hivyo ni **612** sawa na **asilimia 90.4** ya wadau walioalikwa.  Katika idadi hii ya wadau, makundi yaliyoshirikishwa kwa

idadi kubwa ni pamoja na Mabaraza ya watoto, wajane, wanafunzi wa Sekondari na Ssingi na wanajamii kutoka maeneo tofauti.

Wawakilishi kutoka makundi mbalimbali ya wadau ambao wameshiriki katika utafiti huu wametoa maoni, ushauri na mapendekezo tofauti kuhusu mahitaji ya kufanyiwa marekebisho Sheria hii kwa lengo la kuimarisha usimamizi,uwajibikaji, haki na maslahi ya watoto hapa nchini. Kama ilivyoelezwa na wadau, haja ya kufanywa marekebisho ya Sheria hii inatokana na kuongezeka kwa matumizi mitandao ya kijamii na mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia yaliyopo Duniani hivi sasa.

Uchambuzi wa wadau walioshiriki katika utafiti huu ni kama inavyooneshwa katika majadueli namba 1, na chati namba 1 hadi namba 4.

**Jadueli Nam. 1: Idadi ya washiriki wote wa Utafiti.**


| Taasisi za Wadau Walioshiriki | Waliohudhuria | Walioalikwa | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Mahakimu | 9 | 10 | 90.0 |
| Mawakili wa Serikali na Binafsi | 13 | 15 | 86.7 |
| Jumuiya ya Wajane Zanzibar | 150 | 170 | 88.2 |
| Jumuiya ya Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) | 2 | 2 | 100.0 |
| Wasaidizi wa Sheria | 12 | 14 | 85.7 |
| Jumuiya ya Maimamu Zanzibar (JUMAZA) | 6 | 8 | 75.0 |
| Chama cha Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA) | 3 | 4 | 75.0 |
| Asasi ya Utoaji wa Elimu ya Sheria (UPAU) | 2 | 2 | 100.0 |
| Kituo cha Huduma za Kisheria (ZLSC) | 6 | 6 | 100.0 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Jumuiya ya Watu Wenye Ulemavu Zanzibar | 14 | 18 | 77.8 |
| Jumuiya ya Mawakili (ZALHO) | 4 | 4 | 100.0 |
| Mimi na Wewe Foundation | 2 | 2 | 100.0 |
| Mabaraza ya Watoto Zanzibar | 140 | 150 | 93.3 |
| Jeshi la Polisi | 16 | 20 | 80.0 |
| Makadhi wa Wilaya | 10 | 10 | 100.0 |
| Ofisi ya Mufti wa Zanzibar | 4 | 4 | 100.0 |
| Wanafunzi wa Sekondari na Msingi | 50 | 50 | 100.0 |
| Vituo vya Kulelea Mayatima | 12 | 14 | 85.7 |
| Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto | 4 | 4 | 100.0 |
| Walimu wa Madrasa na Skuli | 11 | 14 | 78.6 |
| Wizara ya Habari, Vijana Utamaduni na Michezo | 4 | 4 | 100.0 |
| Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji | 4 | 4 | 100.0 |
| Waandishi wa Habari | 8 | 8 | 100.0 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Chuo cha Mafunzo | 2 | 2 | 100.0 |
| Dawati la Kijinsia | 16 | 20 | 80.0 |
| Maafisa Ustawi wa Jamii | 8 | 8 | 100.0 |
| Masheha wa Shehia | 24 | 24 | 100.0 |
| Wapelelezi wa Makosa ya Udhalilishaji | 6 | 6 | 100.0 |
| Ofisi ya Mufti wa Zanzibar | 2 | 2 | 100.0 |
| Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali | 4 | 4 | 100.0 |
| Wakala wa Serikali Mtandao | 2 | 2 | 100.0 |
| Kituo cha Kurekebisha Tabia za Watoto | 4 | 4 | 100.0 |
| Baraza la Vijana | 4 | 4 | 100.0 |
| Wanajamii | 50 | 60 | 83.3 |
| Madaktari | 4 | 4 | 100.0 |
| JUMLA | 612 | 677 | 90.4 |

***Chanzo: Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar***


**Chati Nam 1: Mchanganuo wa Washiriki Kijinsia**




***Chanzo: Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar***

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa, **asilimia 32.7** ya washiriki walikuwa wanaume na **asilimia 67.3** walikuwa wanawake. Washiriki wanawake walikuwa wengi kutokana na ukweli kwamba masuala ya watoto yanawakabili wanawake zaidi katika maisha ya jamii iliyopo Zanzibar na baadhi ya mikutano ilishirikisha makundi ya wanawake pekee katika utafiti tulioshirikiana na Jumuiya ya Wajane Zanzibar.

**Chati Nam. 2: Idadi na Asilimia ya Washiriki kwa Mujibu wa Kiwango cha Elimu**





***Chanzo: Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar***

Matokeo yanaonesha kuwa **asilimia 13.4** ya washiriki wana elimu ya msingi, **asilimia 46.7** walikuwa na elimu ya sekondari, **asilimia 24.3** walikuwa na elimu baada ya Sekondari na **asilimia 15.5** walikuwa na elimu ya juu kuanzia shahada ya kwanza na kuendelea. Lengo kubwa la kufanya

uchambuzi huu, ni kuonesha kwamba maoni katika utafiti huu yamezingatia wadau wenye elimu tofauti kwa lengo la kupata michango yao kutokana na eneo hili kuwa na changamoto katika usimamizi wa watoto katika jamii na ulinzi wao, haki na maslahi ya watoto hapa nchini.

**Chati Nam.3: Idadi na Asilimia ya Washiriki kwa Mujibu wa Makundi ya Umri.**





***Chanzo: Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar***

Utafiti umezingatia kipengele muhimu katika uchambuzi cha eneo la umri wa wadau, ambapo kundi lenye umri kati ya **miaka 15** hadi **24** ambalo ni kundi la vijana limeshirikishwa kwa **asilimia 39.4,** kundi la watu wenye umri kati ya **miaka 25** hadi **60** ambalo linategemewa kwa kiasi kikubwa katika kukuza Uchumi na Maendeleo ya nchi limeshirikishwa kwa **asilimia 47.1** na kundi la mwisho ni kundi la wazee wenye umri kuanzia **miaka 60** na zaidi ambao ni watu wenye uzoefu na malezi ya watoto na wameishi muda mrefu ambao wameona makuzi na usimamizi wa watoto katika nyakati tofauti katika maisha yao ambalo limeshirikishwa kwa **asilimia 13.6** katika utafiti huu.

Aidha, utafiti umebainisha na kuonesha makundi yalioshirikishwa kutoka katika taasisi mbali mbali za Serikali na binafsi na taasisi nyengine katika masuala ya usimamizi wa watoto, wataalamu na wadau wengine kutoka Asasi za Kiraia.

**Chati Nam.4: Asilimia ya Washiriki kwa Mujibu wa Makundi ya Wadau.**




***Chanzo: Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar***

Katika utafiti huu, wadau kutoka taasisi za Serikali walishirikishwa kwa **asilimia 20.9,** wadau kutoka taasisi binafsi walishirikishwa kwa **asilimia 34.5**, wataalamu na wasimamizi wa watoto walikuwa **asilimia 13.9** na asasi za kiraia walikuwa **asilimia 30.7.**

## 6.3. Matokeo ya Utafiti

Baada ya utafiti huu na kuzingatia Mikataba ya Kimataifa na uzoefu wa Sheria za nchi mbalimbali, maoni ya wadau na Mipango ya nchi kama MKUZA, DIRA ya Maendeleo Zanzibar ya 2050, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha mapinduzi ya 2020 – 2025, na Sera mbalimbali zinazosimamia masuala ya Watoto nchini, mambo mbali mbali yamebainika. Mambo hayo yanapaswa kuzingatiwa kisheria na kiutendaji katika kuweka misingi ya usimamizi, haki, ulinzi, fursa na maslahi ya watoto. Matokeo ya Utafiti huo yanafafanuliwa hapa chini na yamegawanywa katika makundi mawili ambayo ni matokeo ya Kisheria na matokeo ya Kiutendaji.

### 6.3.1. Matokeo ya Kisheria.

**(a) Haja ya Marekebisho ya Sheria**

Kwa sasa kumejitokeza mabadiliko mengi ya Sayansi na Teknolojia pamoja na mifumo mbalimbali inayoathiri ustawi na ulinzi wa mtoto. Aidha, wahalifu wamekuwa wakiwatumia vibaya watoto pamoja na matukio ya unyanyasaji kutoka kwa wazee na walezi. Pamoja na Sheria ya Watoto, Nam.6 ya Mwaka 2011 kuwa ni miongoni mwa Sheria bora za Watoto na kupata tuzo ya Kimataifa, utafiti umebaini kuwepo kwa changamoto katika Sheria hii na hivyo kuathiri ulinzi wa haki za watoto na kuimarisha ustawi wa watoto nchini.

### (b) Kukosekana kwa Taasisi za usimamizi wa huduma za watoto

Kupitia maoni ya wadau walio wengi katika suala la usimamizi wa watoto ambao wameshiriki katika vikao mbali mbali, Utafiti umebaini kuwa kuna changamoto ya kutokuwepo taasisi maalum ya kisheria ambayo itakuwa na jukumu la kufuatilia, kulinda na kusimamia ustawi wa watoto. Aidha, imebainika kwamba kukosekana kwa taasisi za usimamizi kunafanya usimamizi wa watoto kukumbwa na changamoto mbali mbali zinazotokana na kutokuwepo mikakati na ufuatiliaji wa karibu katika maeneo yanayoathiri maslahi ya mtoto.

### (c) Kukosekana kwa Baraza la watoto

Utafiti umebaini kutokuwepo kwa Baraza la Taifa la watoto litakaloshirikisha taasisi zote ambazo kwa namna moja au nyengine zinashiriki katika kulinda haki za mtoto hapa nchini na kubeba jukumu la kuratibu mambo yote ya watoto katika ngazi ya Kitaifa. Imebainika kuwa kuna nchi zilizoanzisha Mabaraza ya watoto ambayo yamesaidia kupaza sauti za watoto, kuweka mikakati ya kukabiliana na changamoto, kutoa elimu, kufuatilia hatua na maendeleo ya watoto walioathirika n.k.

### (d) Usumbufu katika kusikiliza kesi za Watoto katika Mahakama tofauti

Utafiti umebaini kuwepo kwa mamlaka mbili, katika mashauri ya Watoto kunanyima fursa ya mtoto kushtakiwa na kusimamiwa kwa misingi ya Kisheria na Kimataifa, kama ilivyopendekezwa katika usikilizaji wa kesi za watoto.

Imebainika kwamba baadhi ya wakati hujitokeza mtoto mmoja kusikilizwa tuhuma au shauri lake katika mahkama zote mbili kwa maana mahakama ya watoto na Mahakama ya Mkoa, kutokana na mamlaka ya kila Mahkama zilizowekwa kisheria, hali inayoleta changamoto katika usikilizaji na kufuatwa misingi ya kusikiliza mashauri ya watoto.

**(e) Udhaifu katika udhibiti wa makosa ya Udhalilishaji wa watoto katika mitandao**

Imebainika kutokujumuishwa kwa baadhi ya makosa ya aina za udhalilishaji zilizopo katika ulimwengu wa sasa kunapelekea watoto kukosa haki zao na baadhi kudhalilishwa kupitia njia ambazo hazijaidhinishwa kisheria. Aidha, wakati wa utafiti huu, imebainika kuwepo kwa udhalilishaji kupitia mitandao ya kijamii na vifaa vya kielektroniki, makosa ambayo hayajajumuishwa katika kifungu cha 15 cha sheria ya sasa.

**(f) Wajibu wa Jamii kumlinda mtoto dhidi ya ukiukwaji wa haki zake.**

Imebainika kuwepo kwa majukumu ya usimamizi wa watoto kisheria kwa baadhi ya watu na taasisi na kutokuwekwa kwa majukumu hayo kwa jamii kwa ujumla, katika usimamizi wa watoto hao. Kundi hili muhimu la jamii limeachwa kujumuishwa katika kifungu cha 20 cha Sheria.

**(g) Wazazi kuwekewa majukumu ya kisheria kusimamia watoto.**

Utafiti umebaini kwamba hakuna masharti ya kisheria yanayoainisha moja kwa moja, majukumu ya wazazi katika kuwasimamia watoto wao, na kuhakikisha wanasaidia katika ustawi mzuri wa watoto. Aidha, imebainika kwamba hakuna masharti yaliyowekwa kwenye Sheria kubainisha adhabu kwa wazazi au walezi watakaoshindwa kuwasimamia watoto kuwajibishwa kisheria, au kutoa taarifa za udhalilishaji au unyanyasaji dhidi ya watoto walio chini ya mamlaka yao.

**(h) Upokeaji wa malalamiko**

Utafiti umebaini kuwa Sheria hii ya Watoto haikuweka masharti yanayobainisha utaratibu wa upokeaji wa malalamiko yanayohusu masuala ya watoto na utaratibu wa kusimamia upokeaji malalamiko na kuweza kuyasikiliza kwa hatua za awali kwa ajili ya kutatua changamoto zinazowakabili watoto.

### (i) Kuwepo kwa kanuni

Utafiti umebaini kwamba Sheria iliyopo haijatungiwa Kanuni, miongozo na taratibu za kurahisisha utekelezaji wa Sheria hii katika maeneo mengi yaliyoainishwa katika Kifungu cha 138 cha Sheria hii. Imebainika kuwa, kati ya maeneo saba yaliyotakiwa kutungiwa kanuni, ni eneo moja pekee lililotungiwa Kanuni ambalo linahusu nyumba zilizoruhusiwa.

### (j) Ulinzi Maalum wa Watoto

Utafiti umebaini kwamba, Sheria haikuzingatia utaratibu maalum wa ulinzi wa watoto walio tumboni kwa akina mama katika kipindi kinachofaa kabla ya kujifungua. Imebainika kuwa katika kipindi hicho, kina mama hao hawakuwekewa mazingira mazuri ya utunzaji wa watoto walio tumboni na kupatiwa huduma na uangalizi wa karibu kutokana na hali zao kwa lengo la kujilinda na hatari za kuathirika kwa mtoto alie tumboni.

### (k) Ulinzi wa Watoto Njiti

Utafiti umebaini kuwa Sheria haikuweka utaratibu wa kisheria wa kuwapatia msaada waliojifungua watoto njiti ambao ni waajiriwa, kwa kupatiwa likizo ya uzazi hadi mtoto awe katika hali ya kuridhisha. Kwa sasa imeonekana kuna changamoto ya utunzaji na ulezi kwa watoto hao ambao kuzaliwa kwao

kunapelekea kuhitajika muda zaidi wa utunzwaji wao wakati wa kuzaliwa na baada.

**(l) Kutokuwepo kwa Mfuko wa Maendeleo ya Mtoto**

Utafiti umebaini kwamba hakuna masharti ya kisheria ya kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Mtoto ambao utawekewa misingi ya usimamizi na utaratibu wa upatikanaji wa fedha za Mfuko wa Maendeleo ya mtoto ili kuleta ustawi wa mtoto hapa nchini. Aidha, imebainika kuwa, kutokuwepo kwa Mfuko huo na vyanzo na usimamizi wake, kunadhoofisha jitihada za ulinzi wa watoto na ustawi wao wakiwemo watoto walio katika mazingira magumu, waliotelekezwa na wazee wao, wasio na makaazi ya kudumu , walioathirika na madawa ya kulevya, wanaonyanyaswa na watoto wengineo wanaofanana na hao.

**(m) Kutokuwepo kwa Wajibu wa lazima wa kutoa taarifa kwa mtoto aliye na mazingira hatarishi**

Utafiti umebaini kutokuwepo kwa utaratibu wa kisheria wa lazima kwa makundi mbali mbali kutoa ripoti Polisi au mamlaka zinazosimamia masuala ya watoto pale wanapobaini kuathiriwa kwa mtoto au kuwepo kwa uwezekano wa kuathiriwa kwa mtoto huyo. Makundi hayo yanajumuisha kila mtu mwenye ujirani na mtoto mwenye mazingira hatarishi katika eneo hilo, mtu yeyote

anaefanya kazi za kitaalamu au kazi rasmi ambazo zinamuhusisha mtoto katika utendaji wa kazi zake au mtu yeyote ambae anaamini kuwa mtoto aliyekutana nae ameathiriwa au kuna uwezekano wa kuathiriwa. .

Aidha, utafiti umebaini kutokuwepo kwa adhabu kwa mtu yeyote aliyeshindwa kutekeleza wajibu huu wa kutoa taarifa. Pia utafiti umebaini kutokuwepo kwa kinga kwa mtoa taarifa za mtoto aliye hatarini kwa kutobainishwa utambulisho wake na Kinga nyenginezo.

### 6.3.2. Matokeo ya kiutendaji

**(a) Uwepo wa vituo vya Kurekebisha tabia**

Utafiti umebaini kwamba hadi hivi sasa bado suala la kuanzishwa rasmi kwa vituo vya marekebisho ya watoto kama ilivyo katika Sheria hii halijatekelezwa. Kutoanzishwa kwa vituo hivyo kumelalamikiwa na wadau mbali mbali kwamba inarudisha nyuma juhudi za Serikali katika usimamizi wa watoto wanaokiuka Sheria au wanaohitaji usaidizi zaidi katika kuwekwa sawa tabia zao.

**(b) Uhaba wa Rasilimali**

Utafiti umebaini kuwepo kwa ucheleweshwaji wa kesi za watoto kunakosababishwa na uhaba wa vitendea kazi na gharama za usimamizi katika Idara ya Ustawi wa Jamii. Uhaba huu unaleta ugumu katika ufuatiliaji na kufanya tathmini ya kesi hizo.

**(c) Elimu na Mafunzo kwa Maafisa Ustawi na Jamii**

Utafiti pia umebaini elimu haitolewi ya kutosha kuhusu umuhimu wa kutunza watoto, familia na utolewaji wa ushauri nasaha kwa wazee ambao wanatelekeza watoto na familia.

Aidha, imebainika kwamba hakuna mafunzo ya kutosha kwa Maafisa Ustawi kutokana na masuala ya udhalilishaji na mambo mengine yanayowaathiri watoto hapa nchini, hali inayopelekea kuporomoka kwa maadili na athari nyenginezo kwa watoto. Imebainika kuwa kutokuwepo mafunzo ya kutosha kunaathiri uwezo wa Maafisa hao kufanya kazi zao ikiwemo kufanya tathmini, upelelezi na kuweza kufuatilia maeneo yenye viashiria hatarishi.

**(d) Mwamko wa Usimamizi wa Watoto**

Utafiti umebaini kuwepo kwa changamoto ya uelewa mdogo wa wanajamii kuhusu wajibu na majukumu ya jamii katika kusimamia haki, ulinzi, matunzo, upatikanaji wa elimu kwa watoto, maslahi, fursa za watoto na umuhimu wa kuwasimamia watoto katika mienendo yao na shughuli wanazozifanya. Imebainika kutofahamika kwa majukumu ya jamii, wazazi na walezi kwa watoto waliopo katika jamii hizo na kupelekea kufanyika vitendo viovu kwa watoto, kujiingiza katika maadili yasiyokubalika, kuanza kutumia madawa ya kulevya na vitendo vyenginevyo vya hatari.

Aidha, utafiti umebaini taasisi husika hazijaweka mkazo wa kutoa elimu ya mara kwa mara kwa makundi mbali mbali ya kijamii ikiwemo viongozi wa Dini kulititilia mkazo suala la usimamizi wa watoto ili lieleweke na jamii kwa maslahi ya taifa.

# SURA YA SABA

## 6.0 MAPENDEKEZO NA HITIMISHO

## 7.1. Utangulizi

Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar imepitia maeneo mbali mbali ya utafiti wakati wa kufanya mapitio ya Sheria ya Watoto, Nam. 6 ya Mwaka 2011. Mapitio hayo yamezingatia Sera na Sheria mbali mbali zilizopo, uzoefu wa nchi mbali mbali na mikataba ya kimataifa na kikanda inayohusu masuala ya watoto, na kusikiliza maoni ya wadau mbalimbali wanaoguswa na masuala ya mtoto. Baada ya kukamilisha mapitio haya, Tume imeandaa mapendekezo yanayolenga kuimarisha usimamizi wa ustawi wa watoto nchini. Mapendekezo hayo yamegawika sehemu mbili ambayo ni mapendekezo ya kisheria na mapendekezo ya kiutendaji na yanaainishwa hapa chini kama ifuatavyo:

## 7.2. Mapendekezo ya Kisheria

Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Mtoto Nam. 6 ya mwaka 2011 katika maeneo yafuatayo:

### 1. Kujumuishwa kwa makosa ya udhalilishaji wa watoto kielektroniki

Tume inapendekeza kuwa kifungu cha 15 cha Sheria ya Watoto kirekebishwe ili kujumuisha suala la udhalilishaji na unyanyasaji wa watoto kingono kupitia mitandao. Kifungu hicho kinapendekezwa kiainishe aina zote za udhalilishaji zinazoweza kufanyika dhidi ya watoto kupitia njia za mawasiliano ya kielektroniki. Aidha, inapendekezwa kuwa kifungu hicho kiweke adhabu stahiki kwa watakaobainika kutenda makosa hayo kwa watoto ili kudhibiti vitendo hivyo viovu dhidi ya watoto.

## 2. Kuanzishwa kwa Mfuko wa Ustawi wa Mtoto

Tume inapendekeza kuwa Sheria ya Watoto irekebishwe ili kuingiza kifungu kipya kitakachoanzisha **Mfuko wa Ustawi wa Mtoto** kwa madhumuni ya kusaidia ustawi wa watoto wote wa Zanzibar. Mfuko huo unapendekezwa kuzingatia maeneo ya ustawi wa mtoto kama vile kusaidia watoto wenye uhitaji maalum katika jamii, kufanya utafiti wa masuala yenye changamoto kwa watoto, kuchangia katika maendeleo ya mtoto na maeneo mengine yanayoweza kuchangia katika maendeleo ya mtoto.

Aidha, Inapendekezwa kuwa Sheria ibainishe vyanzo vya fedha vya Mfuko huo ambavyo ni ruzuku kutoka Serikalini, mchango kutoka serikali za mitaa, misaada kutoka Mashirika ya Kimataifa, faini zinazotozwa na mahakama ya

watoto, michango kutoka kwa watu binafsi, mashirika ya ndani na fedha kutoka chanzo chengine chochote. Inapendekezwa kuwa Mfuko huo uwekewe misingi ya usimamizi mzuri ili utumike kwa manufaa ya watoto wa Zanzibar kama inavyotarajiwa.

### 3. Wajibu wa Mahakama ya Watoto katika kutembelea maeneo

Tume inapendekeza kuwa Sheria ya Watoto irekebishwe kwa kuwekwa kifungu kitakachoipa uwezo na wajibu Mahakama ya Watoto kutembelea na kufanya tathmini ya hali ya mazingira katika maeneo au taasisi zinazohusika na hifadhi ya mtoto na kutoa amri yoyote ambayo Mahkama itaona inafaa kwa maslahi ya watoto. Maeneo ambayo mahakama ya watoto inaweza kutembelea ni pamoja na mahabusu ya watoto, vituo vya kurekebisha tabia za watoto na maeneo mengine ambayo watoto wanawekwa, au kupatiwa huduma.

### 4. Kuanzishwa kwa Idara mahsusi ya Watoto

Tume inapendekeza Sheria irekebishwe ili kuweka kifungu kitakachotambua uanzishaji wa Idara maalum ya kusimamia maendeleo ya watoto, badala ya utaratibu wa sasa ambao watoto wanasimamiwa na Idara ya Ustawi wa Jamii yenye jukumu la kusimamia masuala mengine mbali mbali na hivyo, kutokuweka wazi mgawanyo wa masuala ya ustawi wa jamii na masuala ya

maendeleo ya mtoto. Idara mpya inayopendekezwa iwekewe bajeti inayojitegemea ili kuiwezesha kutekeleza majukumu ya usimamizi wa watoto kwa ufanisi pamoja na kuwa na watumishi wenye uwezo na ujuzi wa masuala ya watoto na watumishi wengine. Utaratibu huu inapendekezwa ufanyike kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya mwaka 2011.

Aidha, Idara hiyo inapendekezwa kuwa na majukumu mbali mbali yakiwemo majukumu ya uanzishwaji, usimamiaji, utunzaji wa vituo vya kuwalinda watoto, skuli na mahabusu za watoto, kuchunguza, kufuatilia na kuripoti kesi zote za watoto wanaokabiliana na shida na matatizo mbali mbali.

## 5. Wajibu wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa Ulinzi wa Watoto

Tume inapendekeza Sheria irekebishwe kwa kuweka masharti yatakayozipa wajibu Serikali za Mitaa kusaidia katika kulinda na kukuza ustawi wa watoto ndani ya mamlaka zao. Wajibu huo unaweza kutekelezwa na mamlaka ya serikali za mitaa kwa kushirikiana na taasisi nyengine likiwemo Jeshi la Polisi, taasisi zinazosimamia masuala ya watoto ikiwemo Idara ya Watoto inayopendekezwa kuundwa na Asasi za Kiraia zinazosimamia masuala ya watoto. Wajibu huo kwa Serikali za Mitaa unaweza kujumuisha uchunguzi wa maeneo yanayohifadhi watoto, kutunza Rejista ya watoto walio katika mazingira hatarishi katika eneo husika la serikali ya mtaa na kutoa msaada kwa

watoto hao, kuendeleza vipaji vyao na uwezo wa kujitegemea na kutenga maeneo yatakayosaidia ustawi wa watoto ikiwemo maeneo ya michezo na maktaba kwa watoto.

## 6. Wajibu wa Jamii katika ulinzi wa haki za mtoto

Inapendekezwa kuwa Sheria ya Watoto ijumuishe masharti ambayo yatawalazimu wanajamii kushiriki katika ulinzi wa haki za mtoto kwa kuripoti kwa Afisa anayesimamia ustawi wa mtoto au mamlaka ya Serikali ya Mtaa, ukiukaji wowote wa haki za mtoto. Utaratibu huu wa kisheria utaondoa utamaduni uliopo sasa wa wanajamii kuona kuwa hawana jukumu lolote katika ulinzi wa haki za mtoto ambaye hawana uhusiano naye wa moja kwa moja. Ili kutilia nguvu masharti hayo, inapendekezwa kuwa kifungu hicho cha Sheria kibainishe kosa na kuweka adhabu kwa mwanajamii ambaye hatoripoti ukiukwaji wa haki za mtoto kama itakavyoelezwa katika Sheria, na mwanajamii huyo akitiwa hatiani, atawajibika kwa adhabu.

## 7. Kuanzishwa Baraza la Taifa la Watoto

Tume inapendekeza Sheria irekebishwe kwa kuongeza kifungu cha Sheria kitakachoanzisha Baraza la Taifa la Watoto. Inapendekezwa kuwa Baraza hilo liundwe kwa kushirikisha taasisi za Serikali na binafsi ambazo zinashughulikia

masuala ya usimamizi wa haki, maslahi na ustawi wa watoto kwa namna moja au nyengine.

Aidha, Baraza litakaloundwa inapendekezwa liwe na jukumu la kuratibu na kusimamia taasisi zinazosimamia haki, maslahi, ustawi wa watoto na mambo yote yanayohusiana na watoto katika ngazi ya kitaifa. Baraza hilo pia linapendekezwa liwe na majukumu ya kuratibu huduma za watoto, kazi ya kuratibu shughuli zote zinazohusiana na utekelezaji wa Sheria hii, Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki ya Mtoto na Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto.

Inapendekezwa kuainishwe muda wa Baraza hilo kukutana na utaratibu wa kutoa taarifa zao katika ngazi ya Wizara, Serikali na vyombo vyengine vinavyohusika.

## 8. Kutiliwa Nguvu kwa Mapendekezo ya Baraza

Inapendekezwa kuwa Sheria iwe na kifungu kitakachotilia nguvu mapendekezo yanayotolewa na Baraza la Huduma za Watoto kwa Taasisi mbali mbali kwa kuwekwa utaratibu wa kuripotiwa namna mapendekezo haya yalivyotekelezwa na taasisi hizo. Utaratibu wa kuripoti taarifa hiyo ya utekelezaji wa mapendekezo ya Baraza hilo inapendekezwa kuwasilishwa

katika Baraza la Wawakilishi, sambamba na Ripoti ya Mtoto inayowasilishwa Baraza la Wawakilishi kila mwaka.

## 9. Wajibu wa lazima wa kutoa taarifa kwa mtoto aliye hatarini

Tume inapendekeza Sheria irekebishwe kwa kuongeza kifungu kitakachotoa wajibu kwa kila mtu anayefanya kazi ambazo zinazomuhusisha mtoto katika utendaji wa kazi zake au mtu yeyote ambae anaamini kuwa mtoto aliyekutana nae ameathiriwa au kuna uwezekano wa kuathiriwa kuripoti suala hilo Polisi au mamlaka nyengine ya Serikali. Aidha, inapendekezwa kifungu hicho kibainishe adhabu kwa mtu yeyote atakayeshindwa kutekeleza wajibu huu wa kutoa taarifa hizo.

Katika kuhakikisha kunakuwa na ushirikiano mkubwa katika utoaji wa taarifa kuhusu kuathiriwa kwa mtoto, inapendekezwa kifungu hicho kiweke ulinzi kwa mtoa taarifa za mtoto aliye hatarini kwa kuweka usiri juu ya utambulisho wa aliyetoa taarifa hizo na ulinzi mwengine ili wananchi waendelee kusaidia kutoa taarifa hizo.

## 10. Wajibu wa taasisi kwa Watoto.

Tume inapendekeza Sheria ibainishe wajibu wa taasisi za umma na binafsi na maafisa wote wanaojishughulisha na watoto, kuchukua hatua zitakazosaidia

kumlinda na kumtunza mtoto kwa manufaa ya mtoto ikiwemo kuweka Mipango itakayoweza kuwapatia huduma muhimu za elimu, afya na ulinzi kwa watoto wanaohitaji ulinzi maalum.

Aidha, kifungu hicho pia kibainishe namna ya taasisi hizo kuzingatia viwango vya ulinzi wa mtoto katika ngazi ya taasisi ili kuzuia ukatili dhidi ya watoto; unyanyasaji wa kijinsia kwa watoto; kuhakikisha kunakuwa na ulinzi wa watoto na kuchukua hatua mara moja pale ambapo yatawasilishwa malalamiko kuhusu watoto. Pia inapendekezwa kifungu hicho kiweke wajibu wa familia au walezi katika malezi bora ya mtoto. Mapendekezo haya yanakwenda mbali zaidi ya masharti ya kifungu 20 cha Sheria hii kinachoweka wajibu kwa watumishi wa taasisi zinazohusiana na mtoto kutoa taarifa pale inapotokea haki za mtoto kuvunjwa.

### 11. Kufukuzwa kazi na kutokufaa kuteuliwa kuwa karibu na mtoto

Ili kumlinda mtoto dhidi ya vitendo vya udhalilishaji, Tume inapendekeza Sheria iweke masharti ya taasisi ya umma au binafsi kumchukulia hatua za kinidhamu na kumfukuza kazi mfanyakazi wake aliyetenda kosa lolote dhidi ya mtoto. Aidha, inapendekezwa kuwa mfanyakazi huyo aliyetenda vitendo hivyo viovu dhidi ya mtoto, kuzuiliwa kwa kipindi kirefu kujihusisha na kazi yoyote

inayohusiana na mawasiliano ya moja kwa moja na mtoto, pia kutochaguliwa au kuteuliwa katika nafasi yoyote katika taasisi za umma na mashirika binafsi yanayojihusisha na shughuli yoyote inayomgusa mtoto.

**12. Watoto kushtakiwa katika mahakama moja kwa makosa tofauti**

Tume inapendekeza kuwa kifungu cha 18(1)(b) cha Sheria ya Watoto kifanyiwe marekebisho kwa kuipa mahakama ya watoto mamlaka ya kusikiliza kesi zote dhidi ya watoto isipokuwa kesi za mauaji na uhaini. Mapendekezo haya yanatokana na changamoto ya watoto kushtakiwa katika mahakama tofauti kwa baadhi ya makosa ikiwemo kubaka, kuingilia kinyume na maumbile na makosa mengine na hivyo kusababisha usumbufu kwa washtakiwa, mashahidi, wazazi na mawakili.

**13. Udhalilishaji wa watoto katika mitandao**

Tume inapendekeza kuwa Sheria ya Watoto irekebishwe katika kifungu cha 15 ili kujumuisha makosa ya udhalilishaji wa watoto kupitia njia ya mitandao. Mapendekezo haya yanatokana na kuwepo kwa vitendo hivyo vya udhalilishaji wa watoto katika mitandao na Sheria hii kutokuwa na masharti kwa makosa hayo.

**14. Upokeaji wa malalamiko**

Tume inapendekeza Sheria irekebishwe kwa kuweka utaratibu wa kupokea malalamiko yanayohusu masuala ya watoto kutoka kwa mtu yeyote na namna ya kushughulikia malalamiko hayo. Inapendekezwa kuwa malalamiko hayo yashughulikiwe na taasisi ya Serikali inayosimamia masuala ya watoto. Utaratibu huu utasaidia taasisi inayosimamia masuala ya watoto kubaini changamoto zinazowakabili watoto na usimamizi wa watoto kwa ujumla.

### 7.3. Mapendekezo ya kiutendaji

Mbali ya mapendekezo ya kisheria yaliyoainishwa hapo juu, Tume pia imeainisha mapendekezo mbali mbali ya kiutendaji ambayo yatasaidia kuimarisha ustawi wa watoto nchini. Mapendekezo hayo yanafafanuliwa hapa chini kama ifuatavyo:

**1. Kutungwa kanuni**

Tume inapendekeza kutungwa kwa Kanuni za Sheria ya Watoto, Nam. 6 ya mwaka 2011 kama ilivyoelekezwa katika kifungu cha 138 cha Sheria hiyo, ambacho kimeelekeza kutungwa kwa Kanuni katika maeneo mbali mbali ya Sheria hiyo na hadi sasa, maeneo mengi bado hayajatungiwa Kanuni zake, kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa Sheria hii. Eneo pekee lililotungiwa Kanuni ni suala la Nyumba za Makaazi zilizoruhusiwa na takriban maeneo sita yaliyoorodheshwa kutungiwa Kanuni bado hayajatungiwa Kanuni hizo.

## 2. Kuanzishwa kwa Skuli za Marekebisho

Tume inapendekeza kuanzishwa skuli za marekebisho ambazo zitatoa huduma kwa watoto wenye matatizo ya kitabia kama ilivyowekwa katika sehemu ya kumi na moja ya Sheria ya Watoto. Kutoanzishwa kwa Skuli hizo kunadhoofisha jitihada za kuleta ustawi mzuri wa watoto nchini kama ilivyokusudiwa wakati wa kutungwa kwa Sheria hii na kushindwa kufikia viwango vilivyoainishwa katika mikataba ya kimataifa.

## 3. Kutoa elimu kwa wazazi, watoto na wanajamii kwa ujumla.

Inapendekezwa elimu itolewe kwa watoto juu ya masharti ya Sheria ya Watoto zikiwemo haki za watoto, makatazo yaliyoainishwa katika Sheria, wajibu wa wazazi na wadau wanaoshughulikia masuala ya watoto. Elimu hiyo inaweza kutolewa katika skuli na kwa kutumia vyombo vya habari na njia nyenginezo.

Aidha, elimu kuhusu Sheria hii ya Watoto inapendekezwa itolewe kwa taasisi zote zinazosimamia masuala ya watoto na jamii kwa ujumla ili kukuza uelewa wa jamii katika kuwalinda watoto na kuhuisha haki zao.

## 7.4. Hitimisho

Sheria ya Watoto ya Zanzibar ya mwaka 2011 imeshinda tuzo ya sera za mustakabali yaani Future Policy Award. Tuzo hiyo imetolewa mjini Geneva, Uswisi na Shirika la World future Council pamoja na Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto UNICEF.

Sheria hiyo kwa kiasi kikubwa imesaidia kubadilisha mtazamo wa jamii kuhusu watoto na kuchangia katika kupambana na ukatili dhidi ya watoto.

Aidha, katika kuhakikisha tunapata taifa bora, ni vyema jamii ikahakikisha inawalea watoto katika mazingira yaliyo bora na salama kwao ili na wao waweze kusimamia taifa lao. Hii inatokana na mtoto kutakiwa kulelewa katika mazingira salama ambayo kila mtu anaemzunguka atahakikisha anatimiza wajibu wake ipasavyo na atakaposhindwa kufanya hivyo, masharti ya Sheria za nchi yaweze kumbana mtu huyo.

Hivyo Tume inapendekeza kufanyiwa marekebisho Sheria ya Mtoto kwa kuhakikisha inawawajibisha watu wote katika kusimamia haki za mtoto na atakaeshindwa kutoa taarifa za ukiukwaji wa haki za mtoto achukuliwe hatua kwa kupewa adhabu. Aidha, ni vyema mkazo ukawekwa katika utekelezaji wa Sheria hii, ili lengo lililokusudiwa la kuwa na ustawi mzuri wa watoto liweze kufikiwa.